Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Kumi na Mbili - Tarehe 24 Juni, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka 2004/2005.

**MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA - MHE. GEORGE M. LUBELEJE:**

Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Utekelezaji wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha uliopita pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka 2004/2005.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 109

**Barabara ya Kijiji cha Sayu**

**MHE. MHE. PAUL N. MAKOLO (k.n.y. MHE. ROBERT J. BUZUKA)** aliuliza: -

Kwa kuwa Kijiji cha Sayu kimezungukwa na mbuga pande zote na kwa kuwa nyakati za mvua barabara hazipitiki kabisa, hivyo wananchi wanakuwa wametengwa na kuwasababisha kuchelewa kupata huduma muhimu kama hospitali, masoko na kadhalika.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzifungua barabara za kuunganisha Kijiji cha Sayu na Vijiji jirani vya Shilabela, Ng'wang'osha, Bunambiyu, Ng'wasingu, Ng'wamadilanha na Ng'wang'hili?

(b) Kwa kuwa wananchi wako tayari kuchangia nguvu zao katika kutengeneza barabara hizo kwa awamu. Je, Serikali iko tayari kupeleka greda na wataalam ili kusaidia kazi hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Robert Buzuka, Mbunge wa Solwa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004 Halmashauri ya Shinyanga katika makisio yake ilipitisha mpango wa matengenezo ya barabara saba zenye jumla ya urefu wa kilometa 190 ambazo zinagharimiwa na fedha za Mfuko wa Barabara kwa awamu hadi zitakapokamilika. Katika barabara hizo, tatu ziko katika Wilaya ya Shinyanga na nne ziko katika Wilaya ya Kishapu. Kwa upande wa Wilaya ya Kishapu barabara hizo ni barabara ya Gimagi - Mwamalasa, kilometa 26, barabara ya Wishiteleje - Mipa, kilometa 12, barabara ya Mwamanota - Idushi, kilometa 5 na barabara ya Kishapu - Mwakipoya, kilometa 16.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa juhudi za Wilaya kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara ni kuimarisha barabara za Wilaya pamoja na *feeder roads,* zinazounganisha Kata/Tarafa na barabara kuu au barabara za Mkoa. Hivyo, kwa sasa Serikali haina mpango wowote kuhusu barabara inayounganisha Kijiji cha Sayu na Vijiji vya jirani vya Shilabela, Ng'wang'osha, Bunambiyu, Ng'wasingu, Ng'wamadilanha na Ng'wang'hili yeye urefu wa kilometa 40.8.

(b) Mheshimiwa Spika, tunawapongeza sana wanakijiji wa Sayu kwa moyo wao na nia yao nzuri ya kuwa tayari kujitolea kuchangia nguvu zao katika ujenzi wa barabara

hiyo. Hata hivyo, kwa kuwa barabara hii ni ya Kijiji, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga inatakiwa kuandaa mpango madhubuti utakaoshirikisha jamii na wataalam kwa kutumia nyenzo na zana zitakazopatikana ili kuboresha barabara hiyo ya Kijiji cha Sayu. Naamini jambo hili liko ndani ya uwezo wa Halmashauri ya Shinyanga.

**MHE. MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri.

Kwa kuwa Halmashauri nyingi za Wilaya ikiwemo hii ya Solwa na nyingine nyingi tu zina barabara ambazo ni *feeder roads* kama hizi ambazo Mheshimiwa Robert Buzuka amezitaja na zinaenda kwenye barabara kuu na kwa kuwa Halmashauri hizo hazina mitambo mikubwa kama ambavyo anataja Mheshimiwa Waziri na kwa kuwa Serikali imetoa magari mengi *hardtop* na mengine kwa ajili ya kufanikisha ujenzi.

Je, Serikali haioni ni busara sasa kutoa mitambo hiyo mikubwa angalau kwa Halmashauri mbili au tatu zika-*share* ili kuwezesha barabara ambazo ni *feeder roads* zikatengenezwa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo maana katika kueleza nimesema ni juu ya Halmashauri inayohusika kukaa chini kupanga mpango na kuona ni namna gani wanaweza wakatekeleza shughuli zao za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali Kuu kama Serikali Kuu haina huo uwezo wa kutafuta hayo magreda na makatapila mengine kwa ajili ya ujenzi huo, lakini Halmashauri inaweza ikakaa ikatazama ione itafanya nini.

Na. 110

**Mgogoro wa Mpaka Wilaya ya Manyoni na Sikonge**

**MHE. SAID J. NKUMBA** aliuliza: -

Kwa kuwa kwenye Mkutano wa Bajeti 2003/2004, Waziri kwenye hotuba yake alitoa maelekezo ya kumaliza mgogoro wa mpaka kati ya Wilaya ya Manyoni na Sikonge uliodumu kwa muda mrefu: -

(a) Je, baada ya maamuzi yale kutolewa, Serikali imechukua hatua gani kuhahikisha maamuzi yale yanatekelezwa?

(b) Je, kwa kuendelea kulichelewesha jambo hili kukitokea uvunjaji wa amani kwenye eneo hilo ni nani atastahili kulaumiwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Said Nkumba, Mbunge wa Jimbo la Sikonge, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Said Nkumba, Mbunge wa Sikonge kuwa mgogoro kati ya Wilaya ya Manyoni na Sikonge umedumu kwa muda mrefu. Aidha, ni kweli kwamba katika hotuba yangu ya mwaka 2003/2004 nilitamka hapa Bungeni kuwa mgogoro huo sasa umekwisha kufuatia maamuzi yaliyotolewa baada ya timu ya wataalam kutembelea eneo hilo na kuonana na uongozi wa ngazi zote za Mikoa ya Tabora na Singida. Mbali ya uamuzi huo na tamko hilo kuna hali inayoashiria kuwa mgogoro huo bado unaendelea.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupata maelezo kuwa kuna mwingiliano wa maelezo ya Mipaka kwa Wilaya hizo mbili tofauti na *GN* mbalimbali zilizotolewa na Serikali, Ofisi yangu ilichukua hatua zifuatazo:-

(i) Mwaka 2002 iliandikwa barua kwa viongozi kwa Mikoa ya Tabora na Singida kuwataka kushughulikia mgogoro huo kwa pamoja kwa madhumuni ya kuumaliza.

(ii) Mikoa hiyo iliomba wataalam wasiokuwa na upendeleo na upande wowote. Hivyo, wataalam kutoka Ofisi yangu wakishirikiana na wataalam wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi pamoja na wengine kutoka Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa ya Tabora na Singida walitembelea eneo lenye mgogoro ili kubaini kiini cha tatizo na kupendekeza ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, wataalam hao kwa pamoja walibaini kuwa wananchi na baadhi ya *GN* zilikuwa zinakiuka maelezo ya mipaka yaliyotamkwa katika Gazeti la Serikali *GN 217* ya mwaka 1950, *GN 27* ya mwaka 1961 na *GN 185* ya mwaka 1980.

Aidha, wataalam hao walibaini kuwa ni kweli kwamba Vijiji vya Kalangali, Kitunda na Zugimulole vipo katika Wilaya ya Sikonge na siyo Manyoni. Pia, walibaini kuwa kulikuwa na makosa wakati wa utayarishaji wa *GN 293* ya 1994 iliyotengenezwa kwa ajili ya uchaguzi wa Madiwani wa mwaka huo ambayo iliviorodhesha Vijiji hivyo kuwa vipo Wilaya ya Manyoni. Kwa misingi ya maelezo haya, wataalam hao walitoa maoni kuwa mipaka ya Mkoa wa Tabora na ule wa Singida haijawahi kubadilishwa na kwa sababu hiyo Vijiji vya Zugimulole, Kilumbina na Kalangali vipo kwenye Wilaya Sikonge na Vijiji vya Itagata, Kayui, Makale na Mihundu vipo Wilaya ya Manyoni.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoelezea hapo juu, Serikali ilikwishatoa maagizo kwa Mikoa na Wilaya husika mwaka 2002 na hatua zilichukuliwa ili kumaliza mgogoro wa mpaka. Aidha, Ofisi yangu itaitisha kikao wakati huu wa Bunge la Bajeti kitakachohusisha viongozi wa Mikoa yote miwili ili kuzungumzia mgogoro huo kwa mara nyingine na kuwapa maelekezo ya mwisho. Hivyo, Serikali haitarajii kutokea uvunjaji wa amani kwenye eneo hilo. Napenda kutoa wito kwa viongozi wa Wilaya ya Manyoni kutambua maamuzi yaliyokwishatolewa kuhusu mpaka wake na Wilaya ya Sikonge unaozingatia matangazo ya Serikali niliyokwishayataja.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri aliyoyatoa. Nina swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa kwenye jibu la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri amesema ataitisha kikao kitakachowahusisha viongozi wa Mikoa ya Tabora na Singida kuendelea kutoa maelekezo na mimi ninaamini kwamba siyo kujadili mgogoro. Je, isingekuwa vizuri kwa viongozi wa Wizara na kisiasa kwa maana ya Mheshimiwa Waziri au Mheshimiwa Naibu Waziri, kuja kwenye Kata ya Kipili na kutoa ufumbuzi wa mgogoro huu kwa Wananchi ili waachane na *agenda* hii ya mgogoro na waendelee kufanya kazi za maendeleo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, wakati nasimama nimenong'onezwa na viongozi hapa kwamba kubali yaishe. Kwa hiyo, tutajitahidi sana kuona kama tunaweza tukatekeleza hilo ombi lako mara tu baada ya Bunge hili litakapomalizika. *(Kicheko/Makofi)*

Na. 111

**Mpira wa Miguu**

**MHE. MARGARETH J. BWANA** aliuliza: -

Kwa kuwa suala la michezo linahusu zaidi mpira wa miguu ambao unapendwa sana nchini na siyo suala la *FAT* peke yake bali ni sera na mipangilio ya Serikali kuhusu jambo hilo: -

(a) Je, ni lini Serikali itaweka mikakati maalum kuwa na vikosi vya wachezaji vinavyofundishwa chini ya nidhamu ya hali ya juu kama vile JKT, Jeshi, Polisi, Shule za Sekondari, Vyuo vya Ualimu na kadhalika?

(b) Je, ni lini Serikali itaanzisha vyuo maalum hata vya kikanda kwa lengo la kuendeleza mpira wa miguu?

(c) Kwa kuwa Serikali ndiyo inayoandikisha Vyama kama vile *FAT* ambayo sasa imekuwa ni mgogoro mtupu, je, kwa nini isiifutilie mbali na badala yake tukabaki na Vyama vya Mpira ambavyo vitaunganishwa na kuwa chini ya Jeshi?

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margareth Bwana, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka wazi majukumu na wajibu wa kila mdau katika uendelezaji wa michezo. Majukumu hayo yameelezwa kwa uwazi katika

Sera ya Maendeleo ya Michezo. Endapo sote tutashirikiana kikamilifu naamini tutaweza kufanikiwa zaidi ikiwa ni pamoja na kupata wachezaji wenye nidhamu ya hali ya juu.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara inacho Chuo cha Michezo kilichopo Malya, Wilayani Kwimba ambacho hutoa mafunzo mbalimbali ya michezo kwa wanamichezo. Vile vile, katika ujenzi wa uwanja unaotarajiwa kuanza hivi karibuni katika awamu zitakazofuata imekusudiwa kujenga Chuo kipya cha Michezo ukiwemo na mchezo wa mpira wa miguu.

Pia, Serikali imeandaa mazingira bora yanayotoa fursa kwa wananchi wanaotaka kuwekeza katika shule za namna hiyo kama ilivyoainishwa katika Sera ya ya Maendeleo ya Michezo.

(c) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu haioni kama ni busara kufuta vyama vyenye migogoro kwa hivi sasa kwa kuwa kufanya hivyo kunaweza kuwaathiri wapenzi na wanachama wa michezo husika na ambao kwa namna moja au nyingine hawahusiki na migogoro. Tunachofanya ni kuendelea kuwaelimisha wanachama wa michezo husika kujaribu kutatua migogoro yao wenyewe kabla ya chombo kingine kuingilia kati. Aidha, tunajaribu kuelimisha wanachama na wadau wengine umuhimu wa kutekeleza shughuli za vyama vya msingi kwa kuzingatia Katiba zao.

**MHE. MARGARETH J. BWANA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza.

(a) Kwa kuwa Watanzania wengi wanapenda na kufurahia masuala mbalimbali ya michezo ikiwemo mpira wa miguu na kwa kuwa kumejitokeza utitiri mkubwa sana wa migogoro katika *FAT,* ukosefu wa mapato, nidhamu na kadhalika. Je, Serikali haioni kwamba umefika wakati muafaka kupitia Bunge hili kupitisha Azimio rasmi la uendeshaji mzima wa *FAT?*

(b) Kwa kuwa inavyoonekana ni kwamba katika *FAT* sehemu kubwa ya wanaoiendesha ni watu wa kuchaguliwa, hapo nyuma kulikuwa na watendaji ambao walikuwa wameajiriwa na Serikali na ambao walikuwa ni wataalam waliobobea katika masuala ya michezo, lakini baadaye walikuja kuondolea kama akina Mheshimiwa Joel Bendera. Je, kuwarudisha watu kama wale kuongoza suala la michezo Serikali inaona itakuwa imepata hasara gani au ni tatizo gani litakalokuja kujitokeza kama litawarudisha watu kama hao ambao wamebobea katika suala la michezo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** (a) Mheshimiwa Spika, kuna utitiri wa migogoro katika *FAT,* ni kweli tunakubali lakini chanzo chake ni kutokuwa na Katiba ambayo inaaminika, ndiyo maana hata *FIFA* imekuja kuungana na Serikali hapa kuwapa rasimu ya Katiba ili sasa tuwe na Katiba inayoeleweka vizuri na watu waweze kuishi kwa misingi ya Katiba hiyo. Kwa hiyo, haiwezekani kupitisha Azimio hapa la namna ya kuendesha *FAT,* hicho ni Chama cha hiari kitaendeshwa na Wanachama wenyewe. *(Makofi)*

(b) Kuhusu kwamba sehemu kubwa ya viongozi wa Chama waliopo katika *FAT* ni wale waliochaguliwa, zamani ni kweli walikuwepo waliokuwa wanaajiriwa, lakini *FAT* yenyewe ilifika mahali katika Katiba zao na Kanuni zao wakaona haina hiyo haja. Kwa hiyo, wanaoweza kubadili na kuweka nia hiyo ni Wanachama wa Chama hicho wenyewe waseme sasa wamefika mahali wanahitaji Katibu wa kuajiriwa, wengine tunaweza tukashauri. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Lakini kwanza nampongeza Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, leo kavaa suti safi ya rangi ya Yanga. Nampongeza sana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala la utaalam au la ufundishaji kwa maana ya makocha ni muhimu katika maendeleo ya mpira na kwa kuwa nchi nyingi za Kiafrika zinatumia makocha kutoka nje pamoja na jitihada za kuwapeleka makocha wa ndani kwenda kujifundisha. Je, Serikali haioni kwamba wakati umefika sasa wa kutupatia kocha kutoka nje akasaidiana na wa ndani ili kuinua kiwango cha mpira? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli mpira wa miguu ni moja ya michezo ambayo inahitaji utaalam wa hali ya juu, siyo tu katika Tanzania, hata katika nchi zingine nadhani sisi wote ni mashahidi. Hata Waingereza imebidi watafute kocha kutoka Sweden, sasa yuko Steven Golan Erickson. Serikali hiki kitu cha kwanza ilichokuwa inafanya, kwanza ilikuwa ni kujenga uwezo, sasa hivi uwezo unaanza kutoa matumaini na tumeishaanza mawasiliano. Hata jana nimepokea *e-mail* kutoka Ujerumani wakiniambia hatua za kuanza kututafutia kocha zinaendelea vizuri. Kwa hiyo, ilibidi kwanza tujenge uwezo wa kumpata kocha yule na kumlipa kwa sababu kama unavyofahamu Mheshimiwa Mohamed Missanga, makocha hasa wa mpira wa miguu ni ghali sana. *(Makofi)*

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa katika jibu la msingi Mheshimiwa Waziri amesema kwamba *FAT* ni Chama cha hiari na kwa kuwa timu za mpira zinapokwenda nje wanapewa bendera ya Taifa, je, haoni kwamba hiki Chama ambacho kina migogoro na kinapewa bendera ya Taifa halafu wanafanya vibaya ni kuiaibisha nchi ya Tanzania? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, katika vitu ambavyo vinajengwa au vinaamsha ari na hamasa ya uzalendo michezo ni kimojawapo na hasa mchezo unaopendwa sana na watu wengi katika nchi, katika nchi hii ni mpira wa miguu.

Kwa hiyo, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa kweli ni mchezo ambao ungepaswa ku-*reflect* heshima ya nchi. Lakini kutokana na migogoro tuliyonayo na vile vile na tatizo la msingi ambalo Mheshimiwa Mohamed Missanga

amekwishalitaja, kukosekana kwa makocha ambao wana uwezo wa kuweza kusukuma timu ya Taifa, ndiyo maana hatupati matokeo mazuri.

Mheshimiwa Spika, nitakupa mfano, vipo vilabu ambavyo kwa uwezo wake wameweza kutafuta makocha wa nchi za nje kwa mfano *Simba Sports Club* na mliona wenyewe na kwa bahati nzuri na vilabu vingine vimeiga sasa na wao siku hizi kidogo wanasikika. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Beatus Magayane, nataka nikushauri kwamba dawa hasa ni kuzingatia Katiba ambayo sasa tunaitengeneza ili iwe Katiba inayoweka msimamo wa kupata viongozi bora. Dawa hasa wakati wa uchaguzi na sisi Waheshimiwa Wabunge tuingie mitini huko kujaribu kuhamasisha viongozi bora wachaguliwe na dawa hasa ni kutafuta makocha ambao wana utaalam kuja kusimamia mchezo wa mpira wa miguu. *(Makofi)*

Na. 112

**Kuwasaidia Wazee**

**MHE. ALHAJ AHAMADI H. MPEME** aliuliza: -

Kwa kuwa Serikali imeamua kwa makusudi kuyasaidia makundi ya wanawake na vijana kwa kuwapa mikopo mbalimbali ili kuinua hali zao za maisha na kwa kuwa wazee nao wanajishughulisha sana na kazi na maendeleo na ni wazalishaji wakubwa wa mazao ya kilimo; je, Serikali inalisaidiaje kundi la wazee?

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Alhaj Ahamadi Mpeme, Mbunge wa Mtwara Mjini, swali lake kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, napenda kukubaliana na Mheshimiwa Alhaj Ahamadi Mpeme kuwa wazee wanajishughulisha sana na kazi za maendeleo na ni wazalishaji wakubwa na mazao ya kilimo. Kutokana na utafiti *(survey)* uliofanywa na Wizara yangu tumegundua kwamba kuna vikundi vya wazee zaidi ya 2000 vinavyoshirikisha wazee katika kazi za maendeleo ikiwa ni pamoja na kilimo.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 1999 hadi 2000 Wizara yangu ilikuwa inaandaa Sera ya Taifa ya Wazee. Uzoefu tuliopata katika majadiliano na Wilaya zote nchini unaonyesha kwamba wazee walio wengi wana ari na uwezo wa kushiriki kwa ukamilifu katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kuwaletea maendeleo yao wenyewe pamoja na Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua umuhimu wa Wazee katika uzalishaji wa mali kama ilivyoainishwa katika Sera ya Wazee iliyopitishwa na Baraza la

Mawaziri. Katika mikakati ya utekelezaji wa sera hii, Wizara itashirikiana na Wizara ya fedha kuandaa taratibu za kuwa na Mfuko wa Wazee ambao malengo yake yatakuwa kusaidia wazee katika shughuli za uzalishaji mali ikiwa ni pamoja na kilimo.

**MHE. ALHAJ AHMAD H. MPEME:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Sasa ninayo maswali mawili ya nyongeza: -

(a) Ili kuleta matumaini kwa wazee hao kwa jibu lake la msingi labda angefafanua kwa makini utekelezaji wake kwamba unaweza ukaanza lini uundaji wa Mfuko kwa ajili ya Huduma za Wazee? *(Makofi)*

(b) Wazee wastaafu wa Jimbo langu ambao waliajiriwa Serikalini kwa masharti ya *pensionable* na sasa baada ya kuchukua mafao yao kwa mkupuo Serikali imeamua kuwarudisha tena katika pensheni ili waendelee na utaratibu wa kupata pensheni tena, waliniagiza nitoe salaam za shukrani kwa Serikali ya Tanzania. Je, Serikali iko tayari kupokea salaam hizo za shukrani?

**SPIKA:** Hilo siyo swali, kabla hatujaendelea kwenye Wizara nyingine tuendelee na maswali ya nyongeza.

**MHE. PETER KABISA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona, nina swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika majumuisho yake Mheshimiwa Waziri kwenye Bajeti ya mwaka 2001/2002 tarehe 25 Julai, akijibu swali langu alisema kwamba, Mfuko huu ungeanza mwaka huo wa fedha 2001 na iko kwenye *Hansard* ya tarehe 25 Julai, ukurasa wa 135. Sasa ningependa kujua huo Mfuko utaanza lini rasmi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli nilizungumza hayo aliyoyanukuu katika hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka 2001/2002, lakini suala hili la sera na utekelezaji wake ni suala ambalo linahitaji kushirikisha wadau katika kila hatua. Wadau tulipokuwa tukizungumza nao ikaonekana vipo vipengele ambavyo ni lazima tuvitilie maanani. Kwa hiyo, sera ilibidi ichelewe kidogo ikaja ikapitishwa mwaka 2002 na baada ya hapo mikakati ya utekelezaji imeandaliwa na kusambazwa kwa wadau ili kupata maoni yao. Maoni hayo yamekwishapokelewa na tayari yamezingatiwa katika maandalizi ya utekelezaji. Hatua inayofuata sasa ni kuandaa programu ya utekelezaji ambayo itahusisha asasi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika hatua za utekelezaji ni pamoja na kuunda Mfuko huo. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira tena ili tuweze kuunda Mfuko huo kwa sababu unapounda Mfuko ni lazima uwe mwangalifu usije ukajikwaa na kuanguka kama jinsi Mifuko mingine ilivyoanza. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA M. WEJJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri napenda kuuliza kwamba, swali la msingi lilikuwa limehusisha akinamama na vijana kupewa mikopo, je, Wizara hii imejishughulisha vipi

kuwapa au kuwaombea hao wanaotoa mikopo punguzo la riba katika mikopo wanayoipata akinamama na vijana? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, tunayo Mifuko ya Serikali, kuna Mfuko wa Vijana na kuna Mfuko wa Akinamama. Mifuko ile haitozi riba. Tunazo taratibu nyingine za Mabenki, vijana wanakopa kutokana na taratibu zinazoendana na mabenki yenyewe na siku hizi wanaruhusu hata kujadiliana. Tunapohitajika tunakwenda kutoa ushauri, lakini haiwezekani sisi tuweke masharti.

Na. 113

**Idara ya Uhamiaji Kigoma**

**MHE. DR. AMANI W. A. KABOUROU** aliuliza: -

Kwa kuwa kumekuwepo na malalamiko mengi dhidi ya Idara ya Uhamiaji Mkoani Kigoma hususan Mjini Kigoma - Ujiji, kuhusu suala la uraia na kwa kuwa watu wengi wamekuwa wakifukuzwa nchini na aidha, kutupwa mpakani mwa nchi jirani: -

(a) Je, ni utaratibu gani unaofuatwa katika kutoa *Prohibited Immigrant Notice* na ni nani ana madaraka ya kisheria kuzitoa notisi hizo?

(b) Je, ni utaratibu upi halali inapotokea kwamba mtu aliyepewa *Prohibited Immigrant Notice* na kupelekwa nchi jrani na huko akakataliwa kuwa siyo raia wao, ni kuendelea kumfukuza nchini kwa kumrudisha tena katika nchi iliyomkataa na/au hata kumpeleka nchi nyingine?

(c) Je, Mahakama za Tanzania hazina nafasi katika kuamua masuala ya uraia na labda ndiyo maana watu hukamatwa na Idara ya Uhamiaji wakatuhumiwa na kuhukumiwa na Idara hiyo hiyo na yote hayo yakafanyika katika muda usiozidi saa 24 na kwamba utaratibu huu wa Idara kukamata, kutuhumu, kuhukumu, kuadhibu na kumfukuza mtu toka nchini haikiuki haki za binadamu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, Mbunge wa Kigoma Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kigoma kama ilivyo Mikoa mingine ya Mipakani, wananchi wake wana maingiliano makubwa na wananchi wa nchi za jirani. Mkoa wa Kigoma umeathirika sana na maingiliano haya kutokana na machafuko ya kisiasa katika nchi za Burundi na *DRC.* Machafuko haya yamesababisha wimbi kubwa la wakimbizi na wahamiaji haramu nchini mwetu. Kutokana na hali hii, Serikali hufanya misako ya mara kwa mara ili kuwabaini wale ambao si raia na wanaoishi nchini kinyume

cha sheria na kuwarudisha kwenye nchi zao kwa utaratibu wa kutoa *Prohibited Immigrant Notices. (PI)*

Kwa mujibu wa Kanuni namba 17 ya Kanuni za Uhamiaji za mwaka 1997, Mkurugenzi wa Uhamiaji ndiye aliyepewa madaraka ya kuwafukuza nchini watu hao kwa kutoa *PI.* Aidha, Sheria ya Uhamiaji Na. 7 ya mwaka 1995 kifungu cha 5, kimempa madaraka Mkurugenzi wa Uhamiaji kukasimu mamlaka kwa Maafisa wengine wa Uhamiaji. Hivyo, Mkurugenzi amekasimu mamlaka hayo kwa Maafisa Uhamiaji wa Mikoa. Hata hivyo, kila uamuzi wa Mkurugenzi wa Uhamiaji kuhusu utoaji wa *PI* lazima uthibitishwe na Waziri na uamuzi ya Waziri ndiyo wa mwisho.

(b) Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa *PI* Serikali hufanya uchunguzi wa kina kuhusu mgeni anayetuhumiwa, hii ikiwa ni pamoja na kupekua kwa makini kumbukumbu zilizopo. Hivyo, si rahisi kwa raia wa Tanzania kufukuzwa nchini. Wote wanaofukuzwa ni wageni ambao wamekiuka sheria za nchi. Ieleweke kuwa kuna baadhi ya wageni ambao wanatumia mbinu mbalimbali kujihalalishia Utanzania na ndiyo hao wanaotoa malalamiko na madai ya uongo dhidi ya Serikali.

(c) Mheshimiwa Spika, si kweli kwamba Mahakama za Tanzania hazina nafasi katika kuamua masuala ya uraia. Mahakama kama mhimili mmojawapo, ndicho chombo pekee kinachotafsiri sheria za nchi zikiwemo sheria za uraia na ndiyo maana kumekuwepo na kesi kadhaa Mahakamani zinazohusu uraia. Ieleweke kuwa kesi za Uhamiaji zinazofikishwa Mahakamani ni pale watuhumiwa wanapokataa kuwa wamevunja sheria. Wale wanaokubali makosa, Wizara imepewa uwezo wa kuwafukuza nchini bila kuwafikisha Mahakamani. Lakini pia kwa upande wa pili, walalamikaji wanayo haki ya kufikisha madai yao Mahakamani wanapoamini kuwa Serikali haikuwatendea haki. *(Makofi)*

**MHE. DR. AMANI W. A. KABOUROU:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri ningependa kujua je, Idara ya Uhamiaji hutumia vigezo gani kufikia uhakika kwamba wanayemtuhumu siyo raia na hivyo kumrudisha huko wanakodai kuwa ndiyo kwao? *(Makofi)*

Pili, je, bila vitambulisho vya Taifa tunawezaje kuwa na uhakika kwamba Idara ya Uhamiaji kwa kweli inaweza kuthibitisha ugeni wa hao inaowafukuzia nchi nyingine? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, Mbunge wa Kigoma Mjini, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Idara ya Uhamiaji inatumia vigezo mbalimbali katika kubaini watu ambao siyo raia, hata bila kuwepo na vitambulisho vya Kitaifa bado Idara ya Uhamiaji ina uwezo wa kuwang'amua. Kwanza Watanzania tumekaa katika vitongoji, vijiji na katika mitaa, kwa hiyo, yule mhusika kwanza anapekuliwa kuonyesha kwamba kazaliwa wapi, cheti cha kuzaliwa kama hana viongozi wa pale katika kijiji chake,

kitongoji chake au mtaa wake wanamfahamu vipi, ndugu, kwa hiyo, kwa kweli uchambuzi wa kina unafanyika katika kuwatambua hawa ambao siyo raia na vitambulisho vikija vya Taifa vitaturahishia kazi. Lakini hata bila vitambulisho bado tunawang'amua na tunawafukuza nchini. *(Makofi)*

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, baada ya majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza kuwa kwa kuwa wema ndiyo unaomponza mtu mwenyewe binafsi, hata Serikali inaponzwa na wema wake na kwa kuwa mkimbizi anapokuwa anatii taratibu na sheria zote za nchi na za wakimbizi ndiyo huwa mkimbizi. Je, Mheshimiwa Waziri, atanieleza nini kwa wale wakimbizi hasa waliotokea wiki iliyopita kutoroka katika kambi, kwa nini hawahesabiwi na wao kama ni wahamiaji haramu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Haroub Said Masoud, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ipo tofauti kati ya mkimbizi na mhamiaji haramu. Mhamiaji haramu ni yule ambaye anaingia nchini kinyemela bila kuwa na nyaraka muhimu zinazomruhusu kuwa nchini. Mkimbizi naye ni mgeni, lakini huyu akishaingia kama mkimbizi anaandikishwa chini ya Shirika la Wakimbizi la Kimataifa *(UNHCR)* na anakuwa analindwa sasa na sheria za Kimataifa kwa mujibu wa *Geneva Convention.*

Kwa hiyo, wale Wasomali wa juzi waliondoka kambini bila ruhusa kwa sababu kuna taratibu, mkimbizi anapoondoka katika kambi, lazima apate kibali cha Mkuu wa Kambi. Sasa wale waliondoka bila kibali cha Mkuu wa Kambi. Lakini kwa sababu wao wanalindwa na sheria za wakimbizi, hatukuwafukuza kama wahamiaji haramu, bali tumewakabidhi kwa *UNHCR* ambavyo utaratibu unavyosema ili warejeshwe tena kambini na wakitaka kuondoa sasa waondoke kwa kibali maalum kwa mujibu wa taratibu. *(Makofi)*

Na. 114

**Udhibiti wa Ajali za Barabarani**

**MHE. DR. LUCY S. NKYA** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali katika harakati zake za kupunguza matukio ya ajali barabarani iliwaagiza wamiliki wa mabasi ya abiria kufunga vidhibiti mwendo *(Speed Governors)* katika magari yao:-

(a) Je, tangu zoezi hilo lianze ni magari mangapi yamefungwa vidhibiti mwendo na ni asilimia ngapi ya hayo magari yenye vidhibiti mwendo, vidhibiti mwendo vyake vinafanya kazi?

(b) Je, Serikali inatoa tathmini gani kuhusu matumizi ya vidhibiti mwendo katika kupunguza ajali za barabarani?

(c) Je, magari yatokayo nchi jirani kuingia Tanzania yanalazimika kuwa na vidhibiti mwendo kwenye magari yao?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, sheria za kuwataka wamiliki wa magari ya abiria kufunga vidhibiti mwendo kwenye magari ilianza kutumika mwezi Aprili, 1997. Tangu wakati huo jumla ya magari ya abiria 6,074 yamefungwa vidhibiti mwendo. Kati ya hayo 83.5% vidhibiti mwendo vyake vinaendelea kufanya kazi na 16.5% vidhibiti mwendo vyake havifanyi kazi kutokana na sababu mbalimbali.

(b) Mheshimiwa Spika, tathmini ya Serikali inaonyesha kwamba iwapo madreva watazingatia sheria hii kwa ukamilifu na polisi wa trafiki wakiisimamia sheria hii kwa ukamilifu ajali za barabarani zitapungua. Kwa mfano, tarehe 1 Aprili, 1996 hadi 1 Aprili, 1997, yaani kipindi kabla ya sheria hii kuanza kutumika zilitokea ajali 1,457 zilizosababishwa na mabasi, mwaka uliofuata yaani baada sasa ya kuweka sheria hii, mwaka 1998 ajali za mabasi zilipungua hadi 1,256, ukiwa ni upungufu wa ajali 210 sawa na 16%.

Mheshimiwa Spika, tathmini inazidi kuonyesha kwamba jinsi miaka ilivyokwenda madreva walianza kubuni mbinu chafu za kunyofoa/kulegeza vidhibiti mwendo hivyo na ajali za barabarani zikaanza kuongezeka mwaka hadi mwaka.

Napenda kutumia nafasi hii kutoa wito kwamba madreva wa mabasi sharti wazingatie sheria ya vidhibiti mwendo, ili kunusuru maisha ya Watanzania yanayopotea kutokana na mwendo wa kasi.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuwakumbusha askari trafiki wasimamie sheria hii kwa dhati, kwa uadilifu na kwa uzalendo wa hali ya juu, hii ni pamoja na kuwaadhibu bila huruma madereva wanaokiuka sheria hii.

(c) Kwa sasa magari yatokayo nchi jirani na kuingia nchini kwetu hayalazimiki kufuata sheria ya vidhibiti mwendo, lakini wanalazimika kufuata sheria zote za usalama barabarani, pamoja na kuzingatia sheria ya ukomo wa *speed* wa kilometa 80 kwa saa na kuzingatia alama zote za barabarani. *(Makofi)*

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kuuliza maswali mawili kama ifuatavyo;-

(a) Kwa kuwa Serikali ilikuwa na nia njema kabisa ya kufunga vidhibiti mwendo ili kupunguza ajali na kwa kuwa katika jibu lake la msingi amekubali kwamba kuna

madreva ambao wanakuwa na tabia chafu za kuharibu hivyo vidhibiti mwendo. Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kubuni mbinu endelevu za kuweza kudhibiti hiyo tabia mbaya ya hao madreva? *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa ajali zinaendelea kuwepo barabarani na kwa kuwa mara nyingi tukiwa tunasafiri tunakuta kuna askari trafiki wamesimama katika vituo mbalimbali, wengine wakiwa kwenye sehemu ambazo zinaonekana na wengine wamejificha.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, anaweza akatueleza kwamba hawa trafiki wanafanya nini barabarani ikiwa mara nyingi wanasimamisha tu malori na mabasi na wanazungumza tu pembeni wanaondoka na watu wanaendelea kufa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba nia ya Serikali katika kuweka hii sheria ya vidhibiti mwendo, ilikuwa ni kupunguza kasi ya mabasi ambayo ndivyo moja ya vyanzo vya ajali. Ni kweli kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba baadhi ya madereva wamegundua mbinu chafu ya kulegeza hivyo vifaa ili waende kasi.

Kwa hiyo, mbinu ni kwanza sheria hii, sisi Serikali tunaomba kwamba inatufaa ya kuzuia mwendo wa kasi, tutaendelea kusimamia. Kwa hiyo, natoa wito kwamba katika hili tushirikiane wote, madreva, askari polisi hasa trafiki na hata abiria. Nasikitika baadhi ya abiria huwa wanashangilia na kumhimiza dreva kwamba aende kasi wafike haraka. Sasa nasema kwamba mbinu endelevu tushirikiane kwa pamoja kusimamia hii sheria.

Kuhusu askari wa trafiki ambao wanajificha, wengine wako hadharani wanaongea na madereva wa mabasi na malori pembeni, nafikiri katika jibu langu la msingi nimesema kwamba tunawatarajia wafanye kazi kwa uadilifu wa hali ya juu na kwa dhati kabisa. Baadhi ya askari trafiki kwa kweli wanafanya kazi yao vizuri na napenda kuchukua nafasi kwa kuwapongeza wamekuwa wanawakamata madreva. Kwa mfano mwaka 2001 walikamatwa madreva 865 wanaokwenda kasi, mwaka 2002 madreva 877 waliokuwa wanakwenda kasi, mwaka jana madreva 1,025 walikamatwa kwa kuendesha magari kwa kasi na kufikishwa mahakamani. Hawa askari wa namna hii tunawapongeza. Lakini wapo wale ambao Mheshimiwa Mbunge, anaosema hawa tutaendelea kupambana nao na Waheshimiwa Wabunge, mkikutana na askari kama hao tuelezeni ili hatua za nidhamu zichukuliwe dhidi yao. *(Makofi)*

Na. 115

**Kuondokana na Vazi la Kiulaya**

**MHE. OMAR S. CHUBI** aliuliza:-

Kwa kuwa ni muda mrefu Taifa letu limekuwa halina vazi rasmi la Kitanzania na kwa kuzingatia wakati Taifa letu linapata Uhuru lilikuwepo vazi la aina ya Lubega na kofia zilizojuliakana kama Sekouture na kwa kuwa baadaye lilivaliwa vazi aina ya *Chuoun Lai* vazi la aliyekuwa Waziri Mkuu wa China:-

(a) Je, Tanzania itapata lini vazi la Kitaifa ili kuondokana na mtindo wa kuwa na kasumba ya vazi la nchi za Ulaya?

(b) Je, uundaji wa kamati hiyo unahitaji fedha za kigeni?

(c) Je, mbona nchi ndogo za Kusini mwa Afrika kama Lesotho na Swaziland wana vazi lao la kitaifa?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omar Chubi, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza wakati nikijibu swali Na. 9 la Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mbunge wa Manyoni Magharibi, katika Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge hili, nchi yetu haijawahi kuwa na vazi rasmi la Taifa kwa wanaume na wanawake. Mavazi ya wanaume ambayo kwa wakati fulani yalielekea kuchukua nafasi ya vazi la Taifa kwa wanaume yalitokana na wananchi kupenda kumuiga Baba wa Taifa mavazi aliyopenda kuyavaa na ndio sababu mavazi hayo yalipoteza umaarufu wake mara Baba wa Taifa alipoacha kuyavaa na alipostaafu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na vazi la Taifa na hivi sasa inaendesha mchakato wa kupata vazi hilo. Mchakato huo unasimamiwa na Wizara yangu na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa ushirikiano na Sekretariati za Mikoa na wadau wengine. Hivi sasa mashindano yamekwisha kufanyika katika mikoa yote ili kupata washindi watakaoshiriki katika mashindano ngazi ya Taifa. Mashindano ya ngazi ya Taifa yatafanyika hapa Dodoma tarehe 26 Juni, 2004. Waheshimiwa Wabunge, pamoja na wewe Mheshimiwa Spika, mmealikwa kushiriki kwa namna moja au nyingine katika mchakato huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwaomba tuifanye jioni hiyo ya Kitanzania halisi na mavazi yetu ya jioni hiyo yafanane hivyo. Nawaomba wanaopenda, tushirikiane na mimi na Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, katika onyesho tangulizi, tupite pale mbele kama walivyofanya akinamama siku ile. Kwa hiyo, nawaomba waliotayari tushirikiane katika *parade* hiyo na nitakuwa tayari kupokea majina ili tuwaweke katika ratiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ni kubwa yenye makabila mengi yapatayo karibu 120, lakini sisi ni wamoja kama aliavyosema Baba wa Taifa katika mojawapo ya maandishi yake na ninanukuu: “Wasegeju wa Tanga na Wafipa wa Sumbawanga wakiwabagua Waunguja wao watakuwa wamoja?” Sasa inawezekana wengine

hawawajui Wasegeju tunaye msegeju maalum hapa Bungeni Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lakini nchi yetu inaendeshwa na mfumo tofauti na nchi alizozitaja Mheshimiwa Mbunge. Hii ndiyo sababu Serikali imeamua kuwashirikisha wananchi katika Mikoa yote ili hatimaye vazi la Taifa litokane na vionjo, utashi na ubunifu wa maeneo yote ya Taifa letu wakiwemo wa makabila yote pamoja na wale ambao wanaitwa Wakutu kama Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, ambao wengine mlikuwa hamjui kabila lake yeye ni Mkude. *(Makofi)*

**MHE. OMAR S. CHUBI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kwa kunipa niulize swali kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini sambamba na hali iliyopo, ili kupata maendeleo sisi watu wa Kusini tumeletewa mifugo, tunashukuru sana. Lakini baadhi ya wafugaji uvaaji wao unaleta mfadhaiko hasa katika maeneo yetu kwa sababu hatujazoea kuona vitu kama hivyo. Je, Waziri atatusaidiaje katika suala hilo, kwa sababu maeneo mengine watu hawajazoea kuona vile vitu vya siri vinakuwa hewani? *(Makofi/Kicheko)*

(b) Mheshimiwa Waziri, anaweza akarejea maombi yetu yale ya mwanzo ya kufanya ziara yake ambayo aliahirisha ili aje kuona sehemu hizo za historia ya Magofu ya Kilwa Kisiwani, Mapango ya Milima ya Umatumbi kama Nang'oma na Kitana Ng'omba? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Omar Chubi, maswali yake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kutokana na mila na desturi tofauti basi ziko na tabia tofauti. Lakini tunapozidi kuwa Taifa moja ndivyo tunavyozidi kuona ya kila kona kwa sababu tunachanganyika na mionjo tofauti na tabia tofauti ni sehemu ya utajiri wa utamaduni wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakubali mwaliko wake kwamba niende tena Kusini hata sisi Mawaziri tukisafiri tunayakuta mambo mengine ambayo kwetu hatujawahi kujayakuta. Kwa mfano, nilivyofanya ziara yangu wakati nikihutubia mkutano pale Newala, halafu mama mmoja, mimi naeleza habari za MMEM zinavyofanikiwa kule kwa wanaonisikiliza anasema ahaa, huyu ndiyo mwanaume wa kuolewa naye huyu! *(Makofi/Kicheko)*

Sasa mimi Mhehe, nilishangaa sana kuambiwa hivyo. Lakini mwenzake akamjibu hapo hapo ahaa, utampatia wapi, huyu analindwa na maaskari. Kwa hiyo, hii ndiyo Tanzania ilivyo kila mahali tunakuta mambo tofauti. Kwa hiyo, nina hakika nikienda Kilwa nitaona mengi zaidi. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 116

**Ujenzi wa Sekondari**

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA** aliuliza:-

Kwa kuwa Kata za Zombo, Ulaya na Kidodi zimejenga madarasa kwa ajili ya Sekondari.

Je, Serikali iko tayari kutoa vifaa vya kuezekea kama vile bati, mbao na kuzisajili?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Christopher Wegga, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuwapongeza sana wananchi wa Kata za Zombo, Ulaya na Kidodi kwa kujenga madarasa ya shule za Sekondari. Juhudi hizo zitasaidia kuongeza idadi ya watoto waliohitimu na kufaulu mtihani wa darasa la VII kupata nafasi ya sekondari katika shule hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na mafanikio ya MMEM, idadi ya watoto wanaomaliza na kufaulu mtihani wa darasa VII imeongezeka, mpaka sasa karibu maradufu kutoka asilimia 22 mwaka 2000 mpaka asilimia 40. Mwaka 2003 jumla ya watoto 196,273 walifaulu mtihani wa darasa la VII ambao ni sawa na 40.5% ya wanafunzi wote waliofanya mtihani. Lakini ni wanafunzi 95,392 tu sawa na asilimia 48.6 ya watoto wote waliofaulu mtihani huo ndiyo walichaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule za sekondari za Serikali.

Kwa hiyo, ipo haja kubwa kwa wananchi wakishirikiana na Serikali kuongeza shule za sekondari. Serikali kwa kutambua mahitaji hayo imeandaa mpango wa maendeleo ya elimu ya sekondari mwaka 2004 - 2009 wa miaka 5 ambao utekelezaji wake, utaanza katika mwaka huu wa fedha 2004/2005. Mpango huu wa kuboresha na kuongeza nafasi za Elimu ya Sekondari utahusu kuongeza mikondo katika shule zilizopo kwa kuongeza madarasa na kujenga shule za sekondari mpya 1500 kule ambako hakuna sekondari za kutosha.

Mheshimiwa Spika, nina hakika Sekondari za Zombo, Ulaya na Kidodi alizozitaja Mheshimiwa Mbunge, zitakuwemo katika mpango huo kama nitakavyo ufafanua katika hotuba yangu ya Bajeti. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali kama ifuatavyo:-

(a) Kutokana na majibu yake mazuri Mheshimiwa Waziri na kwa sasa kwa sababu ni mchapakazi mzuri, Sekondari ya Kidodi tayari imeshafunguliwa bali haina walimu sasa ni mwezi wa pili na kwa sababu yuko mchapa kazi mwenzake Mkuu wa Mkoa, Mheshimiwa Stephen Mashishanga, yupo hapo juu ananisikiliza baada ya maswali haya tutakaa hapo nje ili tupate walimu na vifaa vya kufundishia pale kwenye shule? *(Makofi/Kicheko)*

(b) Kwa kuwa Sekondari ya Zombo ilikuwa *middle school* ilikuwa na mabweni, majengo yale yanakaa bila kutumika. Je, mwezi Januari atakuwa tayari yeye mwenyewe na Mkuu wa Mkoa kuitembelea ile shule na kufungua ili kupata sekondari ya bweni tena pale? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Christopher Wegga, maswali yake mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza kwa kuwa anasema na Mkuu wa Mkoa Mheshimiwa Stephen Mashishanga yupo hapa, nafurahi sana kusikia hakutakuwa na tatizo lolote pamoja na kwamba Mheshimiwa Stephen Mashishanga mnamwona mrefu namna ile ni mwanangu.

Kwa hiyo, mazungumzo yatakwenda vizuri tu. Pia kuhusu kutembelea shule anayoizungumzia Mheshimiwa Cheristopher Wegga pale ni njiani kabisa, ni rahisi kufika ninapokwenda Iringa. Kwa hiyo, naomba tuwasiliane tu tutapanga katika ratiba niweze kufika na kuona. *(MakofiKicheko)*

Na. 117

**Fedha Zilizotengwa kwa Ununuzi wa Trekta**

**MHE. GRACE S. KIWELU (k.n.y. MHE. DR. WILLBROD P. SLAA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilitoa taarifa Bungeni kuwa imetenga fedha katika Bajeti yake ya mwaka 2002/2003 kwa ajili ya mikopo ya kufufua matrekta na kuwawezesha wakulima kununua matrekta mapya.

(a) Je, Serikali ilitenga kiasi gani cha fedha katika mwaka 2002/2003, 2003/2004 na hadi kufikia tarehe 3 Machi, 2004 zimetumika fedha kiasi gani kutoka katika fungu hilo?

(b) Je, ni vigezo gani vimetumika katika kutoa mikopo hiyo kwa kuzingatia mikopo kwa trekta mpya na ya kufufuliwa na ni nani anayewajibika katika Wilaya kusimamia/kukabidhi au kuthibitisha kuwa waombaji wa mikopo hiyo wanastahili?

(c) Je, katika fungu hilo, Wilaya ya Karatu imepata fedha kiasi gani kwa ajili ya matrekta mapya na ni kiasi gani kwa ajili ya kufufua matrekta yaliyo mabovu ikionyesha namba ya matrekta mapya na wamiliki wao na matrekta ya zamani ya kufufuliwa na ni kiasi gani cha mkopo kwa kila mmoja wao?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mbunge wa Karatu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Utaratibu wa kutoa mikopo ya ukarabati wa matrekta na kununulia matrekta mapya ulianzishwa na Serikali katika Bajeti ya mwaka 2003/2004 ambapo shilingi milioni 560 zilitengwa kwa kazi hiyo.

Katika mwaka 2003/2004, jumla ya maombi 2,325 ya mikopo ya kukarabati matrekta na maombi 174 ya mikopo ya kununulia matrekta mapya yalipokelewa. Kati ya maombi hayo, Bodi ya Wadhamini wa Mfuko wa Pembejeo ilipisha maombi 340 yenye thamani ya shilingi 1,127,882,547/= kwa ajili ya kukarabati na kufufua matrekta na maombi 69, yenye thamani ya shilingi 2,182,656,050/= kwa ajili ya kununulia matrekta mapya. Mikopo hiyo ilianza kutolewa mwezi wa Novemba, 2003.

Hadi mwezi wa Machi, 2004 jumla ya shilingi 518,969,146/= zilikuwa zimekwishatolewa kwa wakopaji. Kati ya hizo shilingi 310,481,968/= ni kwa ajili ya kufufua matrekta 94 na shilingi 208,481,178/= ni kwa ajili ya kununuzi wa matrekta mapya tisa.

(b) Vigezo vinavyotumika katika kutoa mikopo ya ukarabati na ununuzi wa matrekta mapya ni kama ifuatavyo:-

(i) Mikopo ya ukarabati wa matrekta, kiwango cha juu cha mikopo ya ukarabati wa matrekta ni shilingi milioni 3.5. Trekta husika sharti likaguliwe na Afisa Zana za Kilimo wa Wilaya kabla maombi hayajapitishwa na Halmashauri ya Wilaya husika, ili kujua ubovu wake na kukadiria gharama za matengenezo. Dhamana ya mkopo ni kadi ya trekta linaloombewa mkopo. Hati miliki ya mali isiyohamishika yaani nyumba, shamba au hati ya kiapo cha mahakama kama mkopaji hana hati miliki.

(ii) Mikopo ya ununuzi wa matrekta mapya. Maombi sharti yapitishwe na Halmashauri ya Wilaya husika. Mwombaji mkopo ni sharti awe na shamba lisilopungua ekari hamsini na dhamana ya mali isiyohamishika yenye hati miliki. Katika utaratibu wa mikopo hiyo anayewajibika kusimamia au kuthibitisha maombi ya mikopo ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri husika.

(c) Hadi mwezi wa Mei, 2004 jumla ya mikopo 18 yenye thamani ya shilingi 77,555,000/= imetolewa Wilayani Karatu. Kati ya hiyo, mikopo 17 ni kwa ajili ya kufufua au kukarabati matrekta ya zamani na mkopo mmoja kwa ajili ya kununulia trekta jipya.

Mheshimiwa Spika, tunayo orodha kamili ya watu waliokopa katika katika Wilaya ya Karatu ambayo atapatiwa Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa. *(Makofi)*

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa upo utaratibu unaowataka wanaochukua mikopo kurejesha na wengine ili waweze kukopa, je, ni kwa kiasi gani Serikali imefanikiwa kukusanya marejesho hayo?

(b) Waliochukua mikopo hiyo na ambao hawajaweza kurudisha je, Serikali imechukua hatua gani juu yao? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Grace Kiwelu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awamu ya kwanza tulikusanya kama shilingi bilioni 3 na kuendelea. Lakini baadhi ya wakopaji wengi kama shilingi bilioni tulipata matatizo ya kupata fedha hiyo, kesi zilipelekwa mahakamani.

Mheshimiwa Spika, huko katika Mahakama, wengine waliokosa kurejesha mikopo hiyo ilibidi dhamana yao ikamatwe na baadhi ya wengine wamesharejesha na orodha hiyo tunayo. Utaratibu wa sasa ni kwamba tunahakikisha kama nilivyosema taratibu zilizopo zile za kuweka hati miliki na kadha wa kadha unafuatiliwa kwa makini. Hapo nyuma haikuwa makini sana na wengine hawakutumia mikopo hiyo kwa kazi iliyokusudiwa wengi walinunua magari na kadha wa kadha. Lakini masuala haya yote yanafuatiliwa kimahakama.

Na. 118

**Kilimo cha Kisasa**

**MHE. BERNARD K. MEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa kilimo cha kutumia matrekta na kile cha umwagiliaji ndio msingi wa Mapinduzi ya ukweli ya kilimo cha kisasa na endelevu na kwa kuwa baadhi ya wakulima/wafanyabiashara wamekuwa wakiingiza matrekta ya kila aina nchini yakiwemo yale madogo yenye sukari kama za mikokoteni.

(a) Je, Serikali inaweza sasa kuwaambia wananchi ni matrekta ya aina gani na yenye nguvu gani *(HP)* yanafaa kwa kilimo kwa mazingira ya ardhi ya nchi yetu?

(b) Je, Serikai inaweza kutambua na kuwapatia zawadi ya matrekta wakulima bora binafsi au wa vikundi bora vya Wilaya wakati wa sherehe za nane nane zinazofanyika kila mwaka Mikoani ili kuleta chachu ya maendeleo ya kilimo nchini?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bernard Membe, Mbunge wa Mtama, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Matrekta ambayo yamekuwa yakiingizwa nchini yamegawanyika katika makundi matatu yafuatayo:-

Kwanza, Matrekta madogo ambayo hujumuisha matrekta ya mkono, pili, matrekta ya kati na matrekta makubwa. Matrekta yanayoingizwa nchini kabla ya kuruhusiwa kutumika hufanyiwa majaribio ya kuhakiki ubora katika kituo cha kujaribia zana za kilimo kinachofahamika kama *CARMATEC* kilicho Arusha. Aina ya matrekta ambayo yamefanyiwa majaribio na kuruhusiwa kutumika nchini ni *Massey Ferfuson, Ford, Fiat, John Deere, Deutz, International Harvester Case, Swaraj, Farmtrac, Escort Shangai, Valmet* na *Kubota.*

(b) Vigezo vinavyotumika kuchagua nguvu ya trekta itakayofaa hutegemea aina ya udongo, ukubwa wa shamba, mwinuko, kiwango cha unyevunyevu katika ardhi na upya wa shamba. Matrekta madogo ya mkono ya *HP 7-14* hutumika kulima mashamba madogo, majaruba ya mpunga na bustani. Matrekta hayo yana uwezo wa kulima ekari kati ya 25 hadi 50 kwa mwaka.

Matrekta madogo ya *HP 15-50* yana uwezo wa kutifua udongo mwepesi *(sandy loam soil)* Matrekta yenye *HP 50 - 75* yana uwezo wa kutifua ardhi ya udongo mwepesi hadi mzito. Matrekta makubwa ya *HP* zaidi ya 75 hutumika kwenye mashamba makubwa na ardhi yenye udongo mzito. Ufanisi wa aina zote za matrekta makubwa na madogo unategemea matumizi mazuri, matunzo na ukaguzi wa kila siku kama inavyoelekezwa katika miongozo inayotolewa na watengenezaji wa matrekta hayo. Wakulima wanashauriwa kupata ushauri wa mara kwa mara kutoka kwa maafisa zana za kilimo walioko Wilayani katika kuchagua na kuoanisha nguvu ya trekta na zana ya kulimia.

(c) Serikali kila mwaka husimamia sherehe za Nane Nane ambazo zinajumuisha maonyesho ya kilimo na kuwashindanisha wakulima ili kupata wakulima na vikundi bora. Washindi hupewa zawadi mbalimbali zikiwemo pembejeo, zana bora za kilimo fedha taslimu na vyeti. Lengo la Serikali ni kutoa zawadi zitakazotoa motisha kwa wakulima. Serikali itaangalia uwezekano wa kutoa matrekta kama zawadi za washindi wa maonyesho ya nane nane.

**MHE. BERNARD K. MEMBE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri na hasa hili la mwisho analosema Serikali itaangalia. Ningependa kusisitiza hilo kwamba kivutio kikubwa cha wakulima napenda kutoa ushauri kwamba kivutio kikubwa cha wakulima kiwe ni utoaji wa matrekta na siyo zawadi zingine ambazo hazina *input* kubwa.

Lakini swali langu la nyongeza, je, katika kipindi cha mwaka uliopita Serikali ilipoagiza matrekta 172 kwa nini yote yaliagizwa madogo madogo yenye *HP* ndogo bila kuzingatia mazingira na hali halisi ya kilimo katika nchi hii?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia masuala haya ya kilimo mara nyingi kuhusiana na Jimbo lake na zaidi ya hayo napenda kujibu kuwa ni kweli kivutio ni matrekta. Lakini kama nilivyosema uwezo wetu kwa sasa ni mdogo kidogo ingawa fedha nyingi zimetengwa kuliko huko nyuma kwa kununua matrekta. Kwa hiyo, uwe na tumaini.

Kuhusu matrekta madogo, napenda kuishauri kwamba mwaka uliopita yameagizwa matrekta ya aina yote, madogo na makubwa na baadhi ya walionunua matrekta haya makubwa yamefika mpaka *HP 85.* Mfano nakumbuka Jimbo na Mkoa mmoja umeagiza *higher trecter service* matrekta matano ya *HP 85* na nafikiri tena Mkoa mwingine. Lakini napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba aina zote za matrekta zinapatikana mradi tu anayeomba afuate masharti ya kuurudisha mkopo kusudi tusipate matatizo tuliyokumbana nayo kwa kipindi cha nyuma.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali yote yamejibiwa. Sasa tangazo la vikao vya leo, ni kikao kimoja tu. Kamati moja tu ina kikao nayo ni Kamati ya Kilimo na Ardhi. Mheshimiwa Mwenyekiti Eliachim Simpasa, anawaomba wajumbe wa Kamati ya Kilimo na Ardhi wakutane leo kuanzia saa 5.00 asubuhi katika chumba Na. 227 ghorofa ya pili.

Baada ya tangazo hilo nielezee kwamba Waheshimiwa Wabunge kabla hamjaenda kwenye chai wale ambao wanaokusudia kuchangia hoja itakayowasilishwa leo, naomba wawasilishe maombi yao ili tuweze kupanga sasa watakaochangia leo na wale watakaochangia kesho.

Kuna baadhi ya Wabunge wanafikiri anayewahi kuleta maombi ndiyo anapangiwa kwanza. Siyo hivyo. Tunapanga kwa vigezo tofauti kujaribu kuwachanganya makundi mbalimbali yaliyomo kwenye Bunge kwa sababu Bunge letu ni la Muungano basi lazima kuchanganya pande zote mbili za Muungano, Chama Tawala, Upinzani, Wanawake, Wanaume yote haya tunayafikiria ili kusudi wasikilizaji wetu wasikie maoni ya kila kundi. Kwa hiyo, siyo kwamba anayewahi ndiyo anapangwa kwanza hapana. Mwisho wa matangazo.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2004/2005 - Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala iliyochambua

Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu likubali kujadili na hatimaye kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudi zake kubwa za kufufua uchumi wa nchi hii, kujenga demokrasia na kudumisha Umoja wa Kitaifa. Aidha, nampongeza kwa kazi nzuri aliyoifanya akiwa Mwenyekiti Mwenza wa Tume ya Dunia ya Utandawazi na pia kuteuliwa kuwa Kamishna wa Kamisheni ya Afrika yenye jukumu la kuangalia vikwazo ambavyo vinarudisha nyuma maendeleo ya bara la Afrika. Vile vile, namtakia Mheshimiwa Rais afya njema.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuimarisha Muungano na juhudi za kuhimiza utekelezaji wa mkakati wa kuondoa umaskini. Pia, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mbunge wa Ukerewe, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Kwanza wa Bunge la Afrika na Wabunge wote waliochaguliwa kutuwakilisha katika Bunge hilo ambao ni Mheshimiwa Dr. William Shija, Mbunge wa Sengerema, Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, Mbunge wa Kigoma Mjini, Mheshimiwa Dr. Remidius Kissassi, Mbunge wa Dimani na Mheshimiwa Athumani Janguo, Mbunge wa Kisarawe.

Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, Mbunge wa Muhambwe, kwa kuteuliwa kwake kuwa Rais wa Baraza la Kimataifa la Mazingira, Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu, Mbunge wa Maswa, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Tume ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia na Mheshimiwa Sophia Simba, Mbunge wa Viti Maalum na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, kwa kuteuliwa kuiwakilisha Tanzania katika Baraza la Wabunge wa *SADC* yaani *SADC Parliamentary Forum.*

Vile vile, nampongeza Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge katika Bunge lako Tukufu na Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Bariadi Mashariki.

Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Sumaye, Mbunge wa Hanang, kwa hotuba yake iliyoeleza mwelekeo na majukumu ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2004/2005. Napenda kuliahidi Bunge lako Tukufu kwamba, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, itatekeleza maagizo yaliyomo katika hotuba yake inayozingatia malengo na mikakati tuliyojiwekea katika Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025. Aidha, naomba niwashukuru na kuwapongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mbunge wa Handeni na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba, Mbunge wa Rombo, kwa hotuba zao ambazo zimefafanua hali ya uchumi wa nchi na kufanya tathmini ya Bajeti ya Serikali katika kipindi cha mwaka wa fedha 2003/2004 na matarajio kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuipongeza Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Athumani Janguo, Mbunge wa Kisarawe, kwa kuchambua kwa kina Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2004/2005. Maoni na ushauri wa Kamati utazingatiwa wakati wa kutekeleza majukumu na malengo yaliyowekwa katika maeneo yote kwa mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kutoa tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2003/2004 pamoja na maelezo ya malengo ya Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mikoa na Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kupitisha Sera ya Maendeleo Vijijini, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Mkakati wa Maendeleo Vijijini sasa umekamilika na kupitishwa na Serikali mwezi Machi, 2004. Kwa kuwa tayari sekta nyingine zinazo sera na mikakati ambayo inatekelezwa, mathalan Maji, Misitu, Maendeleo ya Jamii, Ushirika, Kilimo na Mifugo, utekelezaji wa Sera na Mkakati wa Maendeleo Vijijini utakuwa na mrengo wa uratibu wa sera na mikakati ya sekta hizo katika ngazi ya kijiji.

Mheshimiwa Spika, Ofisi yangu itajenga uwezo wa Watendaji watakaohusika katika ngazi ya Kijiji na Kata. Sekta nyingine zitahusishwa kwa ukamilifu katika suala hili na ikibidi sera na mikakati ya utekelezaji wa sheria mbalimbali katika sekta hizo zitapitiwa kwa lengo la kuzirekebisha ipasavyo ili kufanikisha shabaha ya Sera na Mkakati wa Maendeleo Vijijini.

Aidha, Ofisi yangu imeanza kutafsiri Sera na Mkakati wa Maendeleo Vijijini katika lugha ya Kiswahili na itatilia mkazo elimu kwa umma ili kuhakikisha kwamba wananchi wanaelewa, wanasimamia, wanamiliki na wananufaika na mkakati wa maendeleo yao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, moja ya mikakati ya utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Vijijini ni kutoa madaraka zaidi kwa wananchi ili waweze kushiriki, kuamua, kupanga, kutekeleza, kufuatilia na kutathmini shughuli za maendeleo katika maeneo yao na pia waweze kumiliki matokeo ya maamuzi yao wenyewe. Mfumo wa upangaji Mipango Shirikishi Jamii wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo ulibuniwa kukidhi haja hii. Mafunzo ya matumizi ya mfumo huu yametolewa katika Halmashauri mbalimbali nchini kutokana na ruzuku ya Serikali na msaada wa *UNICEF, DANIDA* na *SIDA.* Jumla ya Halmashauri 28 zimeeneza mfumo huu katika vijiji na mitaa yake. Kwa sasa mfumo huu unaendelea kuenezwa katika Halmashauri nyingine 13. Lengo ni kueneza mfumo huu katika Halmashauri zote nchini ifikapo mwaka wa fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, tangu Mfuko wa Mikopo kwa Wanawake na Vijana ulipoanzishwa mwaka 1995, maendeleo yake yamekuwa si ya kuridhisha kutokana na sababu mbalimbali. Sababu hizo ni pamoja na kutokuwepo kwa utaratibu mzuri na

endelevu wa uendeshaji wa Mfuko, utaratibu usiofaa wa utoaji mikopo kwa walengwa, wakopaji kutorejesha mikopo na kutokuwa na ushauri wa kitaalam unaokidhi mahitaji ya walengwa wa Mfuko.

Aidha, kutokana na mapato madogo ya Halmashauri na majukumu mengine ya kuleta maendeleo kwa jamii yamechangia kwa kiasi kikubwa kutofikiwa kwa malengo ya Mfuko. Kutokana na sababu hizi, Halmashauri karibu zote hazijaweza kufikia lengo la kuchangia asilimia 10 ya mapato yake kwa ajili ya Mfuko huu tangu ulipoanzishwa. Hivyo ni kiasi kidogo tu cha mikopo kimetolewa na kurejeshwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge kuwa na picha kamili juu ya suala hili, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa itawagawia taarifa kamili kuhusu utekelezaji wa Mfuko huu.

Aidha, Serikali inaendelea kusisitiza umuhimu wa kuwepo Mfuko huu wa mikopo kusaidia maendeleo ya wanawake na vijana. Ofisi yangu kwa kushirikiana na wadau wengine, inachukua hatua mbalimbali kutekeleza maelekezo ya Serikali ya kuufanya Mfuko huu uwe endelevu na hivyo kujiendesha wenyewe. Aidha, Halmashauri zitaendelea kuchangia asilimia 10 ya mapato yao ikiwa ni pamoja na kutumia sehemu itolewayo na Serikali kama fidia ya mapato kwa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu Waheshimiwa Wabunge wamekuwa na tatizo la kutokuwa na ofisi zenye stahili ya Ubunge. Serikali imelifanyia kazi suala hili. Kwa sasa Wabunge wengi wanazo ofisi katika majengo ya Serikali kote nchini. Hadi sasa ofisi hizi zimekuwa zikihudumiwa na ofisi za Wakuu wa Mikoa kwa kutumia fedha za matumizi ya kawaida. Hata hivyo fedha hizo ni kidogo sana kutokana na viwango vidogo vya fedha vinavyotolewa kwa Mikoa. Mawasiliano yanafanyika na Ofisi ya Waziri Mkuu ili kupata njia bora zaidi ya kuhudumia ofisi za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuboresha Sekretarieti za Mikoa ili zitekeleze majukumu yake ipasavyo, suala la ofisi na nyumba za Wakuu wa Wilaya linahitaji kuangaliwa. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2002/2003, Ofisi yangu ilifanya tathmini ya hali ya ofisi na nyumba za Wakuu wa Wilaya nchini. Tathmini hiyo imeonyesha kwamba baadhi ya ofisi na nyumba hizo ziko katika hali mbaya na hivyo kuhitaji ukarabati. Bado tathmini ya kubaini gharama za ujenzi au ukarabati wa majengo haya inaendelea. Hata hivyo fedha zinaendelea kutengwa katika Bajeti za Mikoa kila mwaka kwa ajili ya ukarabati wa majengo hayo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004, Ofisi yangu imeendelea kutoa mafunzo kwa Viongozi na Watendaji mbalimbali. Mafunzo maalum ya *Information Technology and Public Sector Management* katika Chuo cha Uongozi cha Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika (ESAMI). Baadhi ya Viongozi kutoka Ofisi yangu na Sekretarieti za Mikoa wamepatiwa mafunzo hayo. Mafunzo mengine yaliyotolewa ni pamoja na ya Cheti na *Diploma* katika fani ya Uhazili na mafunzo ya muda mfupi kuhusu utunzaji wa kumbukumbu *(records management).* Pia, Makatibu Tarafa 49 wa Mikoa ya Lindi na Mtwara wamepatiwa mafunzo ya Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, Makatibu Tawala wa Mikoa ya Dodoma, Mbeya, Morogoro, Tanga, Arusha, Lindi, Pwani, Kagera na Iringa na Wakurugenzi wa Halmashauri 18 kutoka Mikoa hiyo wamepatiwa mafunzo ya uendeshaji wa mfumo wa Serikali za Mitaa *(Country Focused Training Programme on Local Government Reform in Tanzania)* nchini Japan. Watumishi waliopata mafunzo wamepewa jukumu la kuwafundisha wenzao ambao hawakwenda nchini Japan kwa mafunzo hayo.

Aidha, Maafisa wa Serikali za Mitaa 19 wa Sekretarieti za Mikoa na wanne wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wamepatiwa mafunzo ya mbinu na stadi za kutoa ushauri wa masuala ya uendeshaji na menejimenti ya Serikali za Mitaa. Mafunzo ya mbinu na stadi za kazi yalitolewa kwa Maafisa Watendaji wa Kata 845 kati ya 976. Kwa sasa Serikali imetoa mafunzo ya awali kazini kwa Maafisa Watendaji wa Vijiji 3,940 walioajiriwa na Halmashauri. Mafunzo yametolewa pia kwa Waheshimiwa Madiwani wote 3,447 katika nyanja mbalimbali ikiwa ni pamoja na sheria, uhamasishaji wa maendeleo, usimamizi na udhibiti wa fedha. Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2004/2005, Ofisi yangu itaendelea kutoa mafunzo kama haya kwa kada mbalimbali kuanzia ngazi ya Makao Makuu ya Ofisi yangu hadi kijiji.

Mheshimiwa Spika, programu ya mfumo wa kuweka na kutoa taarifa kwa ajili ya kupima kiwango cha utoaji huduma kwa wananchi *(Local Government Monitoring Database)* iliyoanza kutengenezwa mwaka 2002 kwa msaada wa Serikali ya Japan, imekamilika na kukabidhiwa rasmi. Programu hiyo itakayotumiwa na Ofisi za Sekretarieti za Mikoa itakusanya taarifa na takwimu zitakazotumiwa na wadau wote.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa muundo mpya wa Sekretarieti za Mikoa umekuwa hauridhishi kutokana na upungufu wa watumishi katika Sekretarieti hizo tangu zianzishwe. Matatizo mengine ni pamoja na ikama ya watumishi kutozingatia mazingira na hali ya kipekee ya Mikoa kijiografia, kimaendeleo, kiuchumi na kiutumishi, maslahi ya wataalam wa Sekretarieti kutofahamika, taratibu za mawasiliano kutofuatwa na kuwepo kwa migongano ya kisheria katika utekelezaji wa majukumu ya Sekretarieti za Mikoa.

Mheshimiwa Spika, kutokuwepo kwa vikao vya ushauri katika ngazi ya Wilaya kuliwanyima nafasi Wakuu wa Wilaya, wataalam na wadau wengine walio Wilayani kuchangia na kushauri kuhusu maendeleo ya Wilaya zao. Baada ya kubaini upungufu huo, Ofisi yangu iliandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri ambao ulipendekeza marekebisho katika Sheria ya Tawala za Mikoa Na. 19 ya mwaka 1997 ili kuyaweka wazi majukumu na madaraka ya Sekretarieti za Mikoa ziweze kuzisaidia, kuziwezesha na kuzishauri Mamlaka za Serikali za Mitaa. Waraka huu ulipitishwa na Baraza la Mawaziri na sasa muswada wa marekebisho ya sheria hiyo unaandaliwa na utawasilishwa Bungeni mara utakapokamilika.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi kirefu Serikali imekuwa ikiwatumia Makatibu Tarafa kufanya kazi za Serikali za Mitaa bila kuwa na mwongozo wowote wa kuonyesha namna watumishi hawa wanavyoweza kutekeleza majukumu yao na kuwajibika ipasavyo

kwa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa bila ya kuathiri taratibu zinazotawala utumishi wao.

Aidha, haikuwa imebainishwa kisheria kama Makatibu Tarafa ni watumishi wa umma au ni viongozi wa kisiasa. Uzoefu uliopatikana baada ya kuwatumia Makatibu Tarafa kusimamia shughuli za ulinzi na usalama, uzalishaji mali na huduma za kiuchumi na jamii katika Serikali za Mitaa umeonyesha kuboreka kwa huduma na kuongezeka kwa tija. Hivyo wakati huu ambapo Serikali inaendelea na hatua za kuboresha utendaji kazi na utoaji huduma kwa umma katika sekta mbalimbali kupitia mipango ya uboreshaji, Ofisi yangu iliona kuna umuhimu wa kuandaa mwongozo wa utaratibu wa kazi unaowawezesha Makatibu Tarafa kufanya kazi za Serikali za Mitaa bila kuathiri majukumu na masharti ya kazi walizopangiwa na Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, Ofisi yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma iliandaa mwongozo wa kuwawezesha Makatibu Tarafa kuwajibika kwa Serikali Kuu na pia Serikali za Mitaa. Mwongozo huu umesambazwa na umeanza kutekelezwa. Aidha, Ofisi yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itafanya marekebisho katika Sheria mbalimbali za Serikali za Mitaa pamoja na Sheria ya Tawala za Mikoa Na. 19 ya mwaka 1997 ili miundo na majukumu ya Makatibu Tarafa yawekwe bayana kisheria.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2003/2004, Ofisi yangu imepokea maombi mengi ya kuanzisha maeneo mapya ya utawala. Uchambuzi uliofanywa umebaini kuwepo kwa gharama kubwa ya kuanzisha maeneo mapya ya utawala. Kwa mfano, kuanzisha Wilaya mpya inaigharimu Serikali wastani wa shilingi 1,000,000,000/= zikiwa ni gharama za ujenzi, mishahara na matumizi mengineyo ya uendeshaji. Uanzishwaji wa Tarafa mpya unaigharimu Serikali wastani wa shilingi 50,000,000/= ikiwa ni gharama ya ujenzi na uendeshaji wa Ofisi.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 1996 hadi sasa Serikali imeanzisha Wilaya mpya 17 na Mkoa mpya mmoja. Uzoefu uliopatikana baada ya kutathmini Wilaya zilizoanzishwa kwa kipindi hicho unaonyesha kwamba baadhi hazina majengo yenye hadhi ya Wilaya. Wilaya nyingine hazina ofisi za Makamanda wa Polisi wa Wilaya, Mahakama, nyumba za Wakuu wa Wilaya, vitendea kazi na watumishi wa kutosha. Hata baadhi ya Wilaya za zamani hazina majengo ya ofisi wala nyumba za Wakuu wa Wilaya zenye hadhi. Serikali imeazimia kuimarisha Wilaya zilizopo kwa fedha kidogo zinazopatikana. Hivyo, katika mwaka huu wa fedha Serikali haikusudii kuanzisha maeneo mapya ya utawala. Hali ya uchumi itakapoimarika, Serikali itaendelea kugawa maeneo mapya ya utawala hasa yale ambayo kwa kugawanywa yataleta manufaa kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004, niliahidi kutangaza maeneo mengi zaidi ambayo ni Makao Makuu ya Wilaya, kuwa na hadhi ya Miji Midogo na kuyaondolea hadhi ya Vijiji. Mamlaka za Miji Midogo 88 imehusika katika zoezi hili. Hadi kufikia Januari 2004 Miji Midogo ilikuwa haijaanzishwa kwa sababu utaratibu wa

kisheria wa jinsi ya kuanzisha Miji Midogo bado unaandaliwa. Uanzishwaji wa Miji hiyo utaanza mara tu taratibu zitakapokamilika.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa muundo wa Serikali za Mitaa, ngazi ya Kijiji ndiyo kitovu cha ujenzi wa utawala bora na demokrasia shirikishi. Moja ya changamoto muhimu katika uboreshaji wa Serikali za Mitaa ni uimarishaji wa suala zima la demokrasia na utawala bora kijijini. Ngazi hii ya Serikali za Mitaa ina umuhimu mkubwa kwa Serikali katika kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa shughuli zinazofanywa kijijini ambazo zinalenga kusaidia juhudi za kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu huo, Ofisi yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwakilishi wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP),* imeandaa taarifa inayoitwa *Village Democracy Initiatives.* Taarifa hii inaelezea mapitio ya historia ya Mfumo wa Serikali za Mitaa na mapendekezo ya masuala mbalimbali yanayoweza kutekelezwa katika mchakato mzima wa uboreshaji wa mfumo wa Serikali za Mitaa nchini hususan ngazi ya Kijiji. Serikali itahakikisha kuwa taarifa hii inawafikia Waheshimiwa Wabunge wote na wananchi na kuchukua hatua madhubuti kwa mapendekezo yaliyotolewa katika taarifa hiyo.

Mheshimiwa Spika, suala la utawala bora linahusu pia uchaguzi mzuri wa Viongozi wa ngazi za Vijiji, Mitaa na Vitongoji watakaoweza kuongoza na kusimamia shughuli za maendeleo katika Serikali za Mitaa.

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa uchaguzi wa Viongozi katika ngazi hizi unatarajia kufanyika mwezi Novemba, 2004. Ofisi yangu inaendelea kuratibu shughuli za uchaguzi huo kwa kufanya maandalizi ya kimsingi ili kuwezesha uchaguzi kuwa huru, wa haki na kidemokrasia.

Aidha, napenda kusisitiza kuwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa haisimamii Uchaguzi huu kama wengi wanavyodhani. Kwa mujibu wa Kifungu cha 56 (3) cha Sheria Namba 7 ya mwaka 1982 na Vifungu vya 4 na 70 (c) vya Sheria Namba 8 ya mwaka 1982, jukumu la msingi la Ofisi yangu ni kuandaa Kanuni tu. Uchaguzi huu kwa kweli unaendeshwa na Serikali za Mitaa zenyewe.

Mheshimiwa Spika, maandalizi yaliyofanyika ni pamoja na kuandaa Kanuni za Uchaguzi ambazo Viongozi wa Vyama vya Siasa wameshiriki katika kuzijadili na kutoa maoni katika kikao kilichofanyika Dodoma tarehe 17 - 18 Aprili, 2004. Katika kupanua demokrasia, Ofisi yangu ilitangaza katika magazeti mapendekezo ya Kanuni za Uchaguzi ili kila mwananchi aweze kuzisoma na kutoa maoni yake. Rai yangu ni kuwataka Viongozi wa Halmashauri kusimamia vizuri uchaguzi huo pamoja na Wananchi kushiriki kikamilifu katika kupiga kura ili kuendeleza azma ya Serikali ya kuwa na utawala bora wenye kufuata haki na demokrasia katika ngazi hizi muhimu.

Mheshimiwa Spika, masuala ya ulinzi na usalama ngazi ya vijiji ni muhimu kwa kuleta utulivu, amani na maendeleo ya Taifa kiuchumi, kijamii na kisiasa. Serikali za Vijiji zina jukumu la kwanza la kuhakikisha ulinzi na usalama wa wananchi katika

maeneo yao. Ofisi yangu itahakikisha kwamba Serikali za Vijiji zinahusishwa kikamilifu katika matukio yote yanayotokea katika ngazi hizo yakiwemo masuala ya ulinzi na kusaka wahalifu. Napenda kusisitiza kuwa kusitendeke tukio lolote katika ngazi hiyo bila kushirikisha Viongozi wa Vijiji husika.

Mheshimiwa Spika, watumishi wanaohitajika katika Sekretarieti zote za Mikoa ni 1,743 ikilinganishwa na 1,111 waliopo. Aidha, jumla ya watumishi 204,421 wa kada mbalimbali wanahitajika katika Halmashauri zote. Watumishi waliopo ni 178,720 na upungufu halisi ni watumishi 25,701. Ofisi yangu inaendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Wizara za kisekta kuangalia uwezekano wa kujaza nafasi wazi katika Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu kumekuwa na tatizo la uanzishwaji wa vijiji bila kufuata taratibu. Hali hii imesababisha kuwepo ongezeko la makazi holela, tatizo la upatikanaji wa huduma muhimu za kijamii, kiuchumi na uendeshaji. Ofisi yangu inakamilisha zoezi la kuhakiki na kusajili vijiji vyote na kuvipatia hati kwa mujibu wa sheria za Serikali za Mitaa. Zoezi hili litakamilika kabla ya mwezi Agosti, 2004.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka wa fedha 2003/2004, nilieleza utaratibu mpya wa utoaji leseni mbalimbali unaoondoa mlolongo mrefu unaoleta usumbufu kwa wafanyabiashara. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba kila Halmashauri imeanzisha kituo kimoja cha kutolea leseni *(one stop licensing center).* Kutokana na utaratibu huu mpya, mfanyabiashara wa zamani huchukua muda wa siku moja kupata leseni yake na mfanyabiashara mpya huchukua chini ya siku saba kupata leseni, kinyume na utaratibu wa zamani ambapo walikuwa wanachukua zaidi ya mwezi mmoja. Ni imani yangu kuwa utaratibu huu mpya umeondoa kero na kuongeza tija kwa wafanyabiashara na pia utawavutia wananchi wengi kufanya biashara kwa kupata leseni bila vikwazo.

Aidha, kufuatia uamuzi wa Serikali wa kufuta ada ya leseni inayotozwa chini ya Sheria ya Leseni za Biashara ya mwaka 1972 kwa biashara zenye mauzo yasiyozidi shilingi 20,000,000/= kwa mwaka, Halmashauri zinaagizwa kuzingatia uamuzi huu na kwamba zinakuwa na takwimu sahihi za leseni za biashara ili kuwafahamu walipa kodi walio katika maeneo yao. Halmashauri pia zinatakiwa kuhakikisha kwamba wafanyabiashara wanaendelea kulipa kodi, ada na ushuru mbalimbali kwa mujibu wa Sheria za mapato na kuendesha biashara katika maeneo yanayoruhusiwa.

Kwa msingi huu, Halmashauri hazitakiwi tena kuhusisha utoaji wa leseni na masharti, kama vile uthibitisho wa ukaguzi wa afya au wa kulipa kodi ya majengo wakati wa kutoa leseni. Aidha, wafanyabiashara wanatakiwa kuzingatia masharti ya Sheria nyingine zote pasipo kusubiri hadi wakati wa kuomba leseni.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya mwaka wa fedha 2003/2004, nililifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, Ofisi yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha ilikuwa inaendelea kutafiti njia za kuboresha mapato ya Halmashauri. Ili kuondoa kero zinazotokana na kodi mbalimbali zinazotozwa na Halmashauri ikiwemo

kodi ya maendeleo, Serikali ilifuta kodi zote zenye kero na kuziagiza Halmashauri kubakiza vyanzo vyenye tija na ukusanyaji usio na kero kwa wananchi.

Katika mwaka wa fedha 2003/2004, Halmashauri zilikadiria kukusanya shilingi bilioni 74. Hadi kufikia mwezi Mei, 2004, shilingi bilioni 47 zilikuwa zimekusanywa. Ili kufidia pengo lililotokana na kufutwa kwa baadhi ya kodi, jumla ya shilingi bilioni 22.9 zimetolewa na Serikali kwa Halmashauri kama ilivyokusudiwa. Kwa mwaka wa fedha 2004/2005, Serikali imetenga shilingi bilioni 25 kama ruzuku isiyo na masharti *(unconditional grant)* ili kufidia upungufu wa mapato kutokana na kufutwa kwa kodi zenye kero.

Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, kwa ujumla Halmashauri zimeendelea kufunga vitabu na kuwasilisha hesabu hizo kukaguliwa kwa wakati. Kwa mujibu wa taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hesabu za Halmashauri zinazoishia Desemba 2002, kati ya Halmashauri 117, Halmashauri 20 zilipata Hati Safi ya ukaguzi ikilinganishwa na Halmashauri 11 zilizopata Hati Safi mwaka 2001 na zilizopata hati zenye masharti ni 70 ikilinganishwa na Halmashauri 60 mwaka 2001.

Vile vile, Halmashauri zilizopata Hati Chafu zilipungua kutoka 43 mwaka 2001 na kufikia 27 mwaka 2002. Nachukua nafasi hii kuzipongeza Halmashauri zote zilizopata Hati Safi na kuhimiza Halmashauri zilizopata Hati Chafu kuchukua hatua za dhati kutunza hesabu zao kwa mujibu wa Kanuni za Fedha zilizopo.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza juhudi za kupambana na rushwa, katika mwaka wa fedha 2003/2004, Ofisi yangu imeendesha warsha mbili katika Mikoa ya Lindi na Pwani. Washiriki mbalimbali wakiwemo Viongozi wa Mikoa na Wilaya, Mashirika ya Dini na yasiyo ya kiserikali walishiriki. Mada zilizotolewa na kujadiliwa ni Utawala Bora na Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Rushwa, Sheria ya Kuzuia Rushwa na Maadili katika Utumishi wa Umma. Warsha hizi zimesaidia kujenga ushirikiano wa pamoja na ari katika kupambana na rushwa. Lengo katika mwaka wa fedha 2004/2005 ni kuendelea na warsha kama hizi katika Mikoa mingine. Masuala yatakayozingatiwa ni pamoja na kuendeleza juhudi za kuziba mianya ya rushwa katika ununuzi wa vifaa na ajira kwa kuzingatia Sheria ya Ununuzi ya Umma Namba 3 ya mwaka 2001 na Sheria ya Utumishi wa Umma Namba 8 ya mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, kwa lengo la kufanikisha juhudi za kupambana na vita dhidi ya UKIMWI, Ofisi yangu imeandaa na kusambaza Waraka wa kuunda kamati za kusimamia na kuratibu mapambano dhidi ya UKIMWI. Halmashauri zote zimeunda kamati hizo hadi ngazi ya kijiji. Katika kuziimarisha kamati hizo kwa kushirikiana na Tume ya Kudhibiti Ukimwi *(TACAIDS)* mafunzo yametolewa kwa Sekretarieti za Mikoa ili kuzijengea uwezo wa kuratibu utekelezaji wa mipango ya Halmashauri. Aidha, Kamati za kudhibiti Ukimwi ngazi ya Halmashauri zimepata mafunzo. Katika mwaka wa fedha 2004/2005, Halmashauri zote zitaendelea na utekelezaji wa mipango yake.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya mwaka 2003/2004 nililifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba Serikali itaanza kuajiri Maafisa Watendaji wa Vijiji na Mitaa kuanzia Januari, 2004. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imetoa kibali cha kuajiri Maafisa Watendaji wa Vijiji 9,803. Hadi Mei, 2004 jumla ya Maafisa Watendaji wa Vijiji 3,940 walikuwa wameajiriwa na Halmashauri na mishahara yao kulipwa na Serikali Kuu. Mafunzo ya muda mfupi yanaendelea kutolewa kwa Maafisa Watendaji hawa kabla ya kuanza kazi. Maafisa Watendaji wa Vijiji wasio na sifa wamepewa muda wa miaka mitatu ili wajiendeleze na kufikia viwango vinavyohitajika. Maafisa Watendaji wa Vijiji ambao hawatatimiza sharti hili wataachishwa kazi na nafasi zao kutangazwa.

Aidha, taratibu zinaendelea za kujaza nafasi wazi 5,863 za Maafisa Watendaji wa Vijiji ambao hawana barua. Ajira ya Maafisa Watendaji wa Mitaa 2,666 katika Mamlaka za Miji itafanyika katika mwaka wa fedha 2004/2005. Serikali imetenga jumla ya shilingi 5,949,165,600/= kwa ajili ya kulipia mishahara ya Maafisa Watendaji wa Vijiji na Mitaa katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004, Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa uliendelea kutekeleza majukumu yake makuu yaliyoainishwa chini ya Sheria Na. 6 ya mwaka 2000. Majukumu hayo ni pamoja na kukusanya michango na mapato mengine, kulipa mafao kwa wanachama waliopo na wale watakaojiunga na Mfuko baadaye, kuwekeza katika vitegauchumi mbalimbali na kubuni na kutekeleza mikakati endelevu ya kuboresha mafao na maslahi mengine ya uzeeni kwa wanachama wake.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu hayo, katika mwaka wa fedha 2003/2004, Mfuko uliandikisha wanachama 43,618 hadi mwezi Aprili, 2004. Katika mwaka wa fedha 2004/2005, wanachama wote watakaokuwa wameandikishwa watapewa vitambulisho watakavyovitumia wakati wote wa kupewa huduma na Mfuko.

Aidha, Mfuko ulikusanya shilingi bilioni 23.5 kama michango na marejesho ya fedha zilizowekezwa katika Dhamana za Serikali na Amana za mabenki. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 12.3 zilikusanywa kama makato ya wanachama ikilinganishwa na makisio ya kukusanya shilingi bilioni 12.2. Mafanikio hayo yametokana na Wizara ya Fedha kuanza kupeleka fedha zote za makato moja kwa moja katika Mfuko bila kupitia katika Halmashauri kama ilivyokuwa hapo awali. Ili kuongeza mapato nje ya michango ya kawaida ya wanachama, Mfuko huwekeza fedha zake katika vitegauchumi mbalimbali kama Dhamana za Serikali, Amana za Mabenki, Hisa za Makampuni yaliyoorodheshwa katika Soko la Mitaji na kwenye rasilimali za majengo. Katika mwaka 2003 shilingi bilioni 27.6 sawa na asilimia 93.6 ya lengo la mwaka la shilingi bilioni 29.5 ziliwekezwa katika vitegauchumi na kufanya jumla ya fedha katika vitegauchumi mbalimbali kuwa shilingi bilioni 52.6.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003, Mfuko ulilipa shilingi 712,994,820/= ikilinganishwa na makisio ya shilingi 580,000,000/= kwa wanachama 1,638. Aidha, hesabu za wanachama za mwaka 2001/2002 ziliandaliwa na kutumwa kwao. Vile vile,

Mfuko umefanyiwa uchambuzi kwa lengo la kuubadilisha kuwa wa malipo ya pensheni. Katika mwaka wa fedha 2004/2005, Mfuko utaendelea kuandikisha wanachama wake wapya ili kuwa na kumbukumbu zao muhimu, kuorodhesha na kukusanya madeni yote ambayo Mfuko unawadai wateja wake wote na kufanya tathmini ya mali inayohamishika na isiyohamishika ili kubaini thamani ya rasilimali zote za Mfuko.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa iliundwa chini ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Na. 9 ya mwaka 1982. Madhumuni ya kuundwa kwa Bodi hii ni kuzipatia Halmashauri fedha kwa njia ya mikopo kwa ajili ya kuanzisha na kuendesha miradi ya kiuchumi na huduma nyingine ambazo zinalenga katika kuziongezea mapato Halmashauri. Fedha za mtaji wa kuendeshea huduma ya mikopo zinatokana na Michango ya Akiba ya Halmashauri ijulikanayo kama *Minimum Compulsory Reserve (MCR),* ruzuku ya Serikali, mikopo ya Benki na riba. Kulingana na Sheria, kila Halmashauri inatakiwa iweke akiba katika Bodi ambayo wakati wote itakuwa sawa na asilimia 10 ya mapato halisi ya Halmashauri ya mwaka uliotangulia yanayotokana na vyanzo vyake vya mapato.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2003/2004, Bodi imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kukusanya michango, kutoa mikopo na kufuatilia marejesho ya mikopo kutoka katika Halmashauri zilizokopa. Hadi kufikia Mei, 2004 shilingi 27,804,919/= zilikuwa zimechangwa na kufanya michango yote kufikia shilingi 1,310,149,020.25 ikilinganishwa na kiasi cha shilingi 1,917,689,488.73 zilizopaswa kuchangwa sawa na asilimia 68.31.

Aidha, ruzuku ya shilingi milioni 200 ilipatikana kutoka Serikalini na mkopo wa shilingi milioni 400 kutoka Benki ya *CRDB.* Katika kutekeleza jukumu lake la msingi la utoaji mikopo kwenye Halmashauri, Bodi imeweza kutoa mikopo ya shilingi 542,535,920/= na kufanya mikopo yote iliyotolewa kufikia shilingi 1,245,910,350/=. Kwa upande wa marejesho, jumla ya shilingi 558,916,409.65 kati ya shilingi 737,909,097.30 zimerejeshwa. Riba iliyolipwa kutokana na mikopo ni shilingi 183,168,776.90 kati ya shilingi 268,654,222.85 zinazodaiwa.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa linaloifanya Bodi ishindwe kutoa mikopo kwa wingi na kwa viwango vikubwa linatokana na mtaji mdogo wa Bodi. Kulingana na uchambuzi wa awali uliofanywa na Wataalam Washauri, kiasi kisichopungua shilingi bilioni 4.5 kinahitajika ili kuiwezesha Bodi kutoa mikopo katika viwango vitakavyoleta matokeo kwenye Halmashauri nyingi zaidi. Hivyo, katika mwaka wa fedha 2004/2005, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa itaendelea kukusanya michango na kufuatilia marejesho ya mikopo na riba kutoka katika Halmashauri zinazodaiwa kama hatua mojawapo ya kuongeza mtaji wa Bodi.

Napenda kutoa wito kwa Halmashauri kuhakikisha zinakamilisha michango yake na kwa zile zilizokopa kuhakikisha zinarejesha mikopo ili ziweze kuendelea kukopa zaidi kwa ajili ya shughuli mbalimbali za maendeleo katika Halmashauri zao.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nililiarifu Bunge lako Tukufu kuhusu hatua ya kuifanyia Bodi uchambuzi *(study)* kulingana na miundo iliyopendekezwa ili kuweza kuamua aina ya muundo mmoja utakaofaa kutumika kwa madhumuni ya kuleta ufanisi. Kazi ya uchambuzi wa mapendekezo hayo inatarajiwa kuanza wakati wowote baada ya taratibu za zabuni kukamilika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004, Shirika limeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi. Shirika limeendelea kutoa elimu kwa watoto wadogo *(nursery school),* msingi na sekondari. Vilevile, Maafisa Tabibu *(Clinical Officers)* 75 wamepatiwa mafunzo. Huduma ya elimu ya afya na matibabu kwa wagonjwa pamoja na majeruhi wa ajali za barabarani zimeendelea kutolewa. Pia, Shirika limeendelea kuboresha na kutoa mafunzo ya kilimo, mifugo, ufundi stadi na sayansi kimu kwa wananchi kama njia ya kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana Ofisi yangu ilipanga kuanza ujenzi wa sekondari ya bweni ya wasichana. Kutokana na uhaba wa fedha, ujenzi wa sekondari ya bweni ya wasichana bado haujaanza. Hata hivyo, juhudi za kutafuta fedha kwa ajili ya sekondari hiyo muhimu zinaendelea. Shirika litaendelea na jitihada za kupambana na ujinga, maradhi na umaskini katika mwaka wa fedha 2004/2005 kwa kuendelea kutoa huduma mbalimbali kwa jamii na kuendelea na ukarabati wa miundombinu ya Shirika.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya kuanzishwa kwa Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo ni pamoja na:-

(i) Kutoa mafunzo ya uendeshaji wa Serikali za Mitaa kwa Viongozi na Watumishi walio katika ngazi mbalimbali za Serikali za Mitaa nchini;

(ii) Kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu ya taaluma ya Serikali za Mitaa;

(iii) Kutoa mafunzo juu ya mabadiliko yanayohusu Serikali za Mitaa kulingana na programu ya uboreshaji wa mfumo wa Serikali za Mitaa; na

(iv) Kutoa ushauri kwa Serikali; Mamlaka za Serikali za Mitaa; Mashirika na watu binafsi juu ya masuala yote yanayohusu Serikali za Mitaa.

Katika mwaka wa fedha 2003/2004, Chuo kimekamilisha uandaaji wa makisio ya gharama *(Bill of Quantities)* kwa ajili ya ujenzi wa uzio, uimarishaji wa chanzo cha uhakika cha maji safi na salama na gharama za uendeshaji wa Ofisi. Kazi ya ukarabati wa ukumbi wa mikutano, uandaaji wa mitaala na kuajiri Mkuu wa Chuo hazijafanyika kutokana na uhaba wa fedha. Kazi hizi zimepangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2004/2005 ikiwa ni pamoja na ununuzi wa vyombo vya usafiri.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Masoko ya Kariakoo lilianzishwa kwa madhumuni ya kusimamia na kuendesha Soko Kuu la Kariakoo na Masoko mengine yatakayosimamiwa na Shirika pamoja na kujenga masoko mengine mapya Jijini Dar es Salaam na kuyasimamia. Katika mwaka wa fedha 2003/2004, Shirika limefanikiwa

kuimarisha mfumo wa ukusanyaji mapato uliowezesha kiwango cha makusanyo kuongezeka kutoka shilingi milioni 63 mwaka wa fedha 2002/2003 hadi shilingi milioni 78.5 mwaka wa fedha 2003/2004, kujenga maumbo 110 ya kufanyia biashara ndogo ndogo kwa ushirikiano na Umoja wa Wafanyabiashara ndogo ndogo Kariakoo, kujenga maturubai eneo la mita za mraba 618.87 kwa ajili ya soko la wazi pamoja na ujenzi wa uzio wa soko la Tabata na kuendelea na ukarabati wa majengo ya soko.

Mheshimiwa Spika, ili kuinua ari ya utendaji kazi, Shirika limegharamia mafunzo ya watumishi wake katika fani za biashara, sheria na elimu ya UKIMWI, kulipa gharama za matibabu kwa watumishi na kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi 88,362,000/= kwa watumishi. Aidha, Shirika limeendelea kulipa madeni ambapo shilingi 96,387,568.68/= kati ya shilingi 188,380,345/= zimelipwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2004/2005, Shirika limepanga kuendelea na ukarabati wa paa la jengo kuu na soko la jumla, kujenga paa la maturubai mita za mraba 700, kutengeneza maumbo 200 ya biashara na kununua vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nililijulisha Bunge lako Tukufu kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa chini ya Programu ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa kwa mwaka wa fedha 2003/2004, kazi zifuatazo zimetekelezwa:-

(i) Kuwapatia wananchi uelewa zaidi na nafasi yao katika kufanikisha Mpango wa Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa kupitia vipindi vya Redio na Televisheni, makala kwenye magazeti, warsha na mikutano ya wananchi ili kufanikisha mpango huu;

(ii) Kutekeleza mkakati wa kupeleka madaraka, majukumu na rasilimali kwa wananchi kupitia Serikali za Mitaa;

(iii) Kuandaa mwongozo utakaoiwezesha kila Halmashauri kutayarisha mpango wake wa kuzuia mianya ya rushwa katika eneo lake kwa kuwashirikisha wananchi;

(iv) Kukamilisha mchakato wa uboreshaji wa miundo ya Halmashauri 38 za Awamu ya Kwanza ya programu ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa ikiwa ni pamoja na utayarishaji wa Mipango Mikakati (Strategic Plans), miundo na mifumo ya utumishi. Zoezi hili limesababisha idadi ya Idara za Halmashauri kupungua kutoka 406 hadi 301 hali itakayosababisha watumishi 826 kupunguzwa kazi;

(v) Ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu katika Halmashauri nyingine 52 ili kujua hali halisi ya utoaji wa huduma katika maeneo yao;

(vi) Kuendelea na juhudi za kupeleka madaraka ya usimamizi wa fedha kwenye Serikali za Mitaa kwa kuandaa vigezo maalum *(formula- based criteria)* vitakavyotumika katika kugawa ruzuku ya matumizi ya kawaida ya sekta za elimu na afya katika mwaka wa fedha 2004/2005.

Katika sekta ya elimu kigezo kilichotumiwa kugawa ruzuku ya matumizi ya kawaida ni idadi ya watoto wenye umri wa kwenda shule, yaani umri wa miaka 7 hadi 13 katika eneo la Halmashauri. Kwa upande wa sekta ya afya, vigezo vilivyotumika kugawa ruzuku ya matumizi ya kawaida ni pamoja na:-

(a) Idadi ya watu - asilimia 70;
(b) Kiwango cha umaskini - asilimia 10;
(c) Umbali kutoka makao makuu ya Halmashauri hadi vituo vya kutolea huduma - asimilia 10;
(d) Kiwango cha vifo vya watoto wa umri chini ya miaka mitano - asilimia 10.

Mheshimiwa Spika, vigezo vya kugawa ruzuku ya sekta zilizobakia za Maji, Barabara, Kilimo na Utawala vitaandaliwa na kukamilishwa ili vitumike katika kugawa ruzuku ya matumiz kawaida kwa mwaka wa fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Ofisi yangu kwa kushirikiana na sekta husika iliendelea kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kuzifanyia mapitio na kuzirekebisha Sheria za kisekta ili ziende sambamba na azma ya kupeleka madaraka kwa wananchi. Sheria zilizofanyiwa mapitio na kutolewa mapendekezo ya marekebisho ni Sheria za Elimu, Afya, Utumishi wa Umma *(The Public Service Act, No. 8 of 2002)* na Sheria ya Majadiliano ya pamoja katika Utumishi wa Umma *(The Public Service Negotiating Machinery Act, No. 19 of 2003).* Inatarajiwa kuwa Miswada ya Sheria hizo itawasilishwa Bungeni na Wizara husika.

(ii) Kurekebisha Kanuni na Taratibu za Uchaguzi wa Viongozi katika ngazi ya Vijiji, Mitaa na Vitongoji ili kuweka mazingira ya kisheria yatakayowezesha kufanyika kwa uchaguzi ulio huru, wa haki na kidemokrasia.

(iii) Kujenga uwezo wa Sekretarieti za Mikoa katika kusimamia na kuratibu maboresho kwa kugharamia shughuli mbalimbali zilizopo katika mpango Mkakati wa Programu ya Uboreshaji wa Serikali za Mitaa.

(iv) Kuendelea kuratibu mipango mbalimbali ya uboreshaji inayotekelezwa katika Halmashauri.

(v) Kuendesha mafunzo juu ya mfumo mpya wa ufuatiliaji na tathmini ya utoaji huduma muhimu katika ngazi ya Serikali za Mitaa yalitolewa katika Mikoa 16. Mafunzo haya yalihusisha Wakurugenzi na Maafisa Mipango wa Halmashauri pamoja na Wakuu wa Idara zinazohusika na upunguzaji wa umaskini.

(vi) Kuhamasisha wadau wanaohusika na ukusanyaji na utunzaji wa takwimu kuhusu Mfumo wa Kupima Umaskini na kueleweshwa kuhusu umuhimu wa kukusanya na kutunza takwimu za kiutawala ili ziwe sahihi wakati wote.

(vii) Kusambaza *register* za wakazi wa Vijiji na Mitaa kwa ajili ya kukusanya na kutunza kumbukumbu za wakazi ikiwa ni hatua muhimu katika kuandaa Daftari la Wapiga Kura.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/2005, shughuli zifuatazo zitatekelezwa:-

(i) Kuziwezesha Halmashauri 38 za Awamu ya Kwanza kutekeleza mipango, mikakati na miundo yao mipya;

(ii) Kuziwezesha Halmashauri 52 kutayarisha mipango, mikakati na miundo mipya;

(iii) Kukamilisha uchambuzi wa takwimu ili kujua hali halisi ya utoaji wa huduma katika Halmashauri 24 zilizobakia;

(iv) Kukamilisha maandalizi ya vigezo maalum vya kugawa ruzuku ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo;

(v) Kuzijengea Halmashauri za Vijiji na Mitaa uwezo wa kusimamia fedha;

(vi) Kuanzisha mfumo wa kusimamia fedha kwa kutumia kompyuta katika Halmashauri nyingine 29;

(vii) Kuendelea kuboresha usimamizi, udhibiti wa fedha na ukaguzi wa ndani katika Halmashauri;

(viii) Kuendelea kuzipitia na kuzirekebisha sheria za kisekta ili ziende sambamba na sera ya kupeleka madaraka kwa umma;

(ix) Kuanzisha mfumo wa ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa *(Management Information System)* na kuendesha mafunzo;

(x) Kuendesha mafunzo ya mbinu za uchambuzi wa hali ya umaskini kwa Sekretarieti za Mikoa na Wataalam wa Ofisi yangu;

(xi) Kutekeleza programu ya kujenga uwezo wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Sekretarieti za Mikoa katika kusimamia na kuratibu kazi za Halmashauri;

(xii) Kuendesha vikao vya wadau wakuu wa mpango wa Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa;

(xiii) Kuwapatia watumishi wa sekta zinazohusika mafunzo ya namna ya kushughulikia uratibu wa kupeleka madaraka kwa wananchi;

(xiv) Kutafsiri Sera ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa kwa Kiswahili na kusambaza vijitabu vyake;

(xv) Kuendelea kutoa mafunzo ya ufuatiliaji na tathmini katika Mikoa iliyobakia ya Kigoma, Mtwara, Mwanza, Pwani na Ruvuma; na

(xvi) Kuendesha Semina kwa Waheshimiwa Wabunge na Viongozi wa Vyama vya Siasa kuhusu Programu ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi ulianza kutekelezwa mwezi Julai 2001, ukiwa na lengo la kuboresha elimu ya msingi nchini kwa kuongeza uandikishaji wa watoto, kuinua ubora wa elimu na kujenga uwezo na mifumo ya Taasisi. Katika mwaka wa fedha 2003/2004, mpango ulilenga kujenga vyumba vya madarasa 14,203 na nyumba za walimu 8,000, kutoa fedha za uendeshaji wa shule *(capitation grant),* kutoa mafunzo kwa Kamati za Shule, Halmashauri na Mikoa, kuajiri walimu 10,563, kufanya ukaguzi wa matumizi ya fedha za mpango na kufanya mapitio ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004, shilingi 75,981,523,100/= zilipelekwa kwenye Halmashauri kutekeleza mpango huu. Hadi kufikia mwezi Mei, 2004 shilingi 49,640,576,703.90 zilikuwa zimetumika. Hii ni sawa na asilimia 65 ya fedha zilizotolewa. Shughuli zilizofanyika ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuandikisha watoto 1,253,711 darasa la kwanza kati ya lengo la kuandikisha watoto 1,640,969;

(ii) Nyumba za walimu 559 zimekamilika na ujenzi wa nyumba 368 unaendelea;

(iii) Vyumba vya madarasa 5,646 vimejengwa na kukamilika na ujenzi wa vyumba vya madarasa 4,968 unaendelea;

(iv) Walimu 15,583 wameajiriwa kufundisha shule za msingi;

(v) Kamati za shule zimepatiwa mafunzo ya uendeshaji shule na usimamizi wa fedha;

(vi) Maafisa wanne katika kila Halmashauri na wawili kutoka kila Mkoa wamepatiwa mafunzo juu ya usimamizi wa mpango;

(vii) Fedha zote za uendeshaji shule na ununuzi wa vitabu zimepelekwa shuleni kupitia Halmashauri;

(viii) Maafisa watano kutoka kila Halmashauri wamepatiwa mafunzo ili kuwafundisha walimu juu ya ununuzi wa vitabu ngazi ya shule.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya jumla ya mpango huu ni kama ifuatavyo:-

(i) Uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi umeimarika kutoka kitabu kimoja kwa wanafunzi wanane hadi wastani wa kitabu kimoja kwa wanafunzi watatu kwa madarasa ya kwanza hadi la nne na wastani wa kitabu kimoja kwa wanafunzi watano kwa madarasa ya tano hadi sita;

(ii) Kutokana na fedha za uendeshaji shule *(capitation grant)* baadhi ya majengo, vifaa na mazingira ya shule yameimarishwa. Majengo yamefanyiwa ukarabati, meza na viti vimenunuliwa na vifaa vya kufundishia na kujifunzia vimeongezeka;

(iii) Walimu wengi wamehudhuria mafunzo mbali mbali ya kuongeza taaluma yao;

(iv) Ajira ya walimu wapya imepunguza upungufu mkubwa uliokuwepo;

(v) Kwa kutumia kiwango cha fedha kilichotolewa na Serikali, wananchi wameweza kujenga vyumba vingi vya madarasa, kuweka madawati au kujenga vyoo kwa kuzingatia ubora unaotakiwa;

(vi) Kamati za Shule kwa kushirikiana na Serikali za Vijiji/Kamati za Mtaa zimeweza kusimamia matumizi ya fedha kikamilifu; na

(vii) Watoto wengi hasa wa kike wameandikishwa darasa la kwanza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa na mafanikio niliyoyaelezea, mpango huu umekuwa na matatizo yafuatayo:-

(i) Watoto wengi waliandikishwa hivyo kuongeza msongamano darasani;

(ii) Baadhi ya walimu kutotaka kwenda kufundisha katika sehemu nyingine za nchi;

(iii) Watoto wenye umri wa miaka 11-13 chini ya Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa (MEMKWA) bado kuanza masomo kutokana na mpango huo kutokamilika;

(iv) Baadhi ya maeneo wananchi kukataa kushiriki kazi za ujenzi kwa kisingizio kuwa Serikali imetoa fedha za kutosha na kuwa michango imefutwa;

(v) Ukosefu wa nyumba za walimu hasa maeneo ya vijijini kutokana na kutofikiwa kwa malengo ya ujenzi;

(vi) Upungufu wa wataalam wa kusimamia shughuli za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2004/2005, mpango umelenga kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kujenga nyumba za walimu 6,000;

(ii) Kujenga vyumba vya madarasa 7,794;

(iii) Kuendelea kutoa fedha za uendeshaji *(capitation grant)* ikiwa ni dola kumi kwa kila mwanafunzi;

(iv) Kujenga matanki 2,000 ya kuvuna maji ya mvua;

(v) Kuajiri walimu 7,286;

(vi) Kuandikisha watoto 1,041,880 wenye umri wa kwenda shule;

(vii) Kuendelea kutoa mafunzo juu ya mpango huu kwa wataalam wa Halmashauri na Kamati za Shule.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Pamoja wa Afya ulianza mwaka wa fedha 2000/2001, mpaka sasa jumla ya Halmashauri 113 zinatekeleza shughuli zinazogharamiwa na Mfuko huu. Madhumuni yake ni kuboresha huduma za afya zinazotolewa na sekta ya afya katika Halmashauri ili kuimarisha afya za wananchi, kusaidia mkakati wa kupunguza umaskini kwa wananchi, kuwezesha upatikanaji wa dawa, vifaa na huduma nyingine muhimu kwenye vituo vya kutolea huduma za afya na kuwapa wananchi madaraka zaidi ya kumiliki huduma za afya. Maeneo makuu ya mpango huu ni kama yafuatayo:-

(i) Uboreshaji wa huduma ya uzazi na afya ya mtoto;

(ii) Uboreshaji wa huduma za kudhibiti na kutibu magonjwa ya kuambukiza;

(iii) Uboreshaji wa huduma za kinga ya afya ya jamii na kinga dhidi ya magonjwa;

(iv) Uboreshaji wa huduma za kinga na tiba ya magonjwa yasiyoambukiza; na
(v) Uboreshaji wa huduma za utawala.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mpango huu kwa mwaka wa fedha 2003/2004 ni kama ifuatavyo:-

(i) Halmashauri zimeendelea na ukarabati mdogo mdogo wa vituo vya kutolea huduma za afya zikiwemo Hospitali za Mikoa, Wilaya, vituo vya Afya na Zahanati;

(ii) Halmashauri zimenunua vifaa muhimu vya kutolea huduma za afya na madawa na kuvisambaza kwenye vituo vyake;

(iii) Mafunzo mbalimbali yametolewa kwa Wataalam wa Afya jamii na vikundi rika ili kuongeza stadi na uwezo wa kutoa huduma za afya, elimu dhidi ya UKIMWI, magonjwa ya kuambukiza na milipuko na uendeshaji na usimamizi wa vyombo vya usafiri pamoja na uchangiaji wa huduma za Afya;

(iv) Kutoa huduma za chanjo ya surua na magonjwa mengine ya kuambukiza kwa watoto na akina mama wajawazito na kufikia kiwango cha asilimia 90; na

(v) Uimarishaji wa miundombinu ya mawasiliano umefanyika ambapo Halmashauri nyingi zimenunua na kusimika mawasiliano ya njia za redio za upepo kati ya Hospitali za Wilaya na Vituo vya Afya na Zahanati.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Mei, 2004 shilingi 12,768,834,236.50 zilitolewa na kutumika katika Halmashauri 113 kutekeleza majukumu mbalimbali kwa mujibu wa mipango yao ya mwaka wa fedha 2003/2004. Sambamba na utekelezaji huu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imetumia kiasi cha shilingi 500,000,000.00 kutoka Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Denmark *(DANIDA)* kuendesha mafunzo kwa Maafisa Usafiri kutoka Halmashauri 69 na Maafisa Usafiri 13 kutoka Sekretarieti za Mikoa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeamua kuanzisha utaratibu wa usimamizi endelevu wa vyombo vya usafiri kwenye Serikali za Mitaa zote kufuatia mafanikio mazuri yaliyopatikana katika Mpango wa Mfuko wa Afya. Lengo kuu la utaratibu huu ni kuzijengea uwezo Halmashauri zetu kusimamia matumizi ya vyombo vya usafiri na hivyo kuweka mazingira na utaratibu mzuri wa upatikanaji wa vyombo hivyo vinapohitajika, kuwawezesha wananchi wetu kutumia kwa malipo huduma ya vyombo vya usafiri inayotolewa na Halmashauri na kuweka utaratibu kwa Halmashauri wa kuweza kununua vyombo vipya vya usafiri na hivyo kuondokana na matumizi ya vyombo chakavu ambavyo ni mzigo na hasara kwao kuvitumia. Katika kutekeleza utaratibu huu Sekretarieti za Mikoa zimepewa jukumu la kuratibu matumizi ya magari katika Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2004/2005, shilingi 18,697,480,100.00 zimetengwa kwa ajili ya Mfuko wa pamoja wa Afya ili kuimarisha huduma za mama na mtoto, kuimarisha udhibiti wa magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukiza na kuimarisha mafunzo kwa watumishi wa sekta ya afya.

Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusu uandaaji wa michoro ya majengo ya kutolea huduma za afya, ukarabati wa majengo na upelekaji wa vifaa vya kitaalam na samani kwenye Hospitali za Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati. Katika mwaka wa fedha 2003/2004, mradi umekuwa katika hatua za maandalizi. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na:-

(i) Kuendesha mafunzo kuhusu taaluma ya kutathmini mahitaji ya ukarabati, taratibu za manunuzi na mipango endelevu ya ukarabati wa majengo na vifaa vya huduma za afya;

(ii) Kuandaa hadidu za rejea za kumpata mtaalam mshauri wa kuandaa michoro *(standard drawings)* ya majengo itakayozingatiwa na Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati zinazojengwa;

(iii) Kusambaza mwongozo wa taratibu za ununuzi *(Procurement Manual)* kwa Halmashauri zote ili kuwawezesha kuwa na rejea ya kuzingatia wakati wote wanapofanya ununuzi; na

(iv) Kuandaa taratibu za kuwapata wataalam watakaofanya tathmini ya mahitaji ya ukarabati wa majengo ya hospitali za Wilaya na vifaa vya kitaalam.

Mheshimiwa Spika, malengo ya mwaka wa fedha 2004/2005 ni pamoja na:-

(i) Kuendeleza mafunzo kuhusu taaluma ya kutathmini na kupanga mahitaji ya ukarabati wa huduma za afya;

(ii) Kuzipatia Halmashauri fedha kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya kutolea huduma za Afya;

(iii) Kukamilisha michoro *(standard drawings)* ya majengo ya kutolea huduma za afya kwa ajili ya matumizi ya Halmashauri; na

(iv) Kufanya tathmini ya mahitaji ya ukarabati wa hospitali za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, mradi ulianza rasmi mwezi Mei, 1997 na unatarajia kumalizika mwezi Desemba, 2004. Madhumuni ya mradi ni kukarabati na kufanya upanuzi wa huduma muhimu katika Manispaa za Arusha, Iringa, Mbeya, Morogoro, Moshi, Tabora, Tanga, Dodoma na Majiji ya Dar es Salaam na Mwanza ili kuzijengea Manispaa na Majiji hayo uwezo wa utoaji huduma kwa wananchi. Lengo ni kuleta maendeleo na kupunguza umaskini katika maeneo husika. Shughuli zinazotekelezwa ni pamoja na upanuzi na ukarabati wa barabara zilizopo chini ya Halmashauri za Manispaa na Jiji, ukarabati na upanuzi wa mifumo ya maji safi na maji taka iliyopo chini ya Mamlaka za Maji Safi na Maji Taka, ukusanyaji wa taka ngumu, ujenzi wa karakana na uimarishaji na ujenzi wa miundombinu katika Manispaa zilizo chini ya mradi. Katika Manispaa ya Dodoma, mradi umehusika na usambazaji maji katika eneo la Nkuhungu.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizokamilika katika mwaka wa fedha 2003/2004 ni ujenzi wa barabara za nyongeza (awamu ya kwanza) na mifereji ya maji ya mvua iliyohusisha barabara za Manispaa za Arusha, Moshi, Morogoro, Iringa na Mbeya pamoja na stendi za mabasi katika Manispaa za Tabora, Mwanza na Tanga.

Kuhusu uboreshaji miundombinu thabiti, mafunzo kwa watumishi mbalimbali na viongozi wa Halmashauri na Mamlaka za Maji Safi na Maji Taka yalikamilika. Mradi uliweza pia kutoa nyenzo na vifaa vya kufanyia kazi katika Manispaa hizo hususan kompyuta 3 kwa kila Manispaa, mashine ya kusaidia uthamini wa majengo na tingatinga la kusambaza, kupakia na kushindilia taka ngumu.

Aidha, awamu ya mwisho ya vifaa vimekwishaagizwa na vitasambazwa kwenye Manispaa husika. Vifaa hivi ni vya matengenezo ya mifumo ya maji safi na maji taka. Awamu ya pili ya kazi za nyongeza kwa kutumia fedha zilizobakia katika mpango huu, zilihusisha barabara za Manispaa za Arusha, Moshi, Tanga, Iringa, Mbeya, Tabora na Jiji la Mwanza zenye jumla ya kilometa 11.61 na stendi ya mabasi ya Msamvu katika Manispaa ya Morogoro yenye eneo la mita za mraba 11,170. Katika Jiji la Dar es Salaam kazi za nyongeza awamu ya pili zitahusu kuondoa tatizo la barabara kujaa maji kwa barabara za Kijitonyama katika Manispaa ya Kinondoni na Barabara za Tabata katika Manispaa ya Ilala. Kazi hizi zilianza kati ya Novemba na Desemba 2003 na zinatarajiwa kumalizika mwezi Juni 2004.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2004/2005, mradi utakamilisha kazi za nyongeza awamu ya pili, uchimbaji wa dampo katika Manispaa ya Moshi na maandalizi ya mradi unaofuata ujulikanao kama Mpango wa Kuzisaidia Serikali za Mitaa. Mradi unatarajia kutumia kiasi cha shilingi 1,146,610,000.00 fedha za nje kukamilisha kazi zilizobakia.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaandaa mpango utakaoziwezesha Serikali za Mitaa kupata fedha zaidi kwa matumizi ya shughuli za maendeleo utakaogharamiwa kwa pamoja na fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia, Serikali za Ireland na Uholanzi na mchango wa Serikali Kuu pamoja na Halmashauri husika. Hatua za awali za maandalizi ya Mpango zimekamilika.

Aidha, tathmini ya kina itafanyika Septemba, 2004 ikifuatiwa na majadiliano kati ya Serikali na Benki ya Dunia kuhusu vipengele vya mkataba wa mkopo na masharti yake. Inatarajiwa fedha zitapatikana kuanzia mwezi Januari, 2005. Utekelezaji wa mpango mzima unatarajiwa kuwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka wa fedha 2004/2005 - 2008/2009 na utagharimu dola za Marekani milioni 121.7.

Mheshimiwa Spika, mpango huu utahusu maeneo yafuatayo:-

(i) Utoaji wa ruzuku kwa Halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam kwa ajili ya kutekeleza miradi ya miundombinu itakayobuniwa kwa kuwashirikisha wananchi katika kupanga kuanzia chini kwenda juu pamoja na kuzijengea Halmashauri uwezo wa kutekeleza mpango kwa ufanisi;

(ii) Ruzuku itatolewa kwa Halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kuboresha miundombinu katika maeneo ya makazi duni, kuboresha ukusanyaji wa mapato ili miundombinu itakayojengwa iweze kuwa endelevu kwa kufanyiwa matengenezo ya mara kwa mara na utekelezaji wa Programu ya Afya na Usafi

ngazi ya Kaya itakayohusisha Mitaa 31 yenye wakazi wapatao 330,000. Ili kuonyesha uhitaji, kaya zitatakiwa kuchangia asilimia 5 ya gharama ya mradi unaokusudiwa; na

(iii) Kujenga uwezo wa Wizara yenye dhamana ya Serikali za Mitaa pamoja na Sekretarieti za Mikoa ili ziweze kusimamia utekelezaji wa Mpango na kuziwezesha Halmashauri kutimiza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, masuala muhimu yatakayozingatiwa katika utekelezaji ni pamoja na:-

(i) Kuzishirikisha Halmashauri 47 zilizopatikana kwa kupima hali ya kifedha, uwezo wa kusimamia fedha, hali ya utumishi na uwezo wa kutekeleza miradi. Halmashauri 42 zitaendelea kupata msaada chini ya programu za kieneo *(Area Based Programmes)* zinazoendeshwa sasa na Wahisani mbalimbali na Halmashauri 25 zilizobaki zitatengewa ruzuku ili ziweze kujijengea uwezo na kufanikiwa kupata ruzuku ya kujenga miundombinu;

(ii) Kutimiza masharti yanayohusu utunzaji mzuri wa kumbukumbu za kihasibu na usimamizi wa fedha ikiwa ni pamoja na utumiaji wa kompyuta katika kutunza hesabu za Halmashauri zinazotumia mfumo huu, kupata hati safi za ukaguzi wa hesabu, kuwa na wafanyakazi wenye sifa na uwezo unaotakiwa kwenye ngazi mbalimbali, kuonyesha uwazi wa kutosha kuhusu maamuzi na utendaji wa Halmashauri, kuwa na uwezo wa kifedha wa kuchangia asilimia 5 ya gharama za shughuli za maendeleo, kudhihirisha kuwepo kwa taratibu zinazokubalika kuhusu zabuni, uwezo wa kupanga na kutekeleza mipango shirikishi kuhusu maendeleo ya Halmashauri na uwezo wa kupanga na kutekeleza taratibu endelevu kuhusu utunzaji wa mali za Halmashauri na ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, mpango huu utaijengea uwezo Ofisi yangu pamoja na Sekretarieti za Mikoa ili ziweze kusimamia utekelezaji wa Mpango na kuziwezesha Halmashauri kutimiza majukumu yake. Aidha, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2004/2005, mpango utatumia Shilingi 12,451,598,100.00. Fedha hizi zitatolewa kwa kutumia vigezo maalum. Kwa upande wa ruzuku ya miradi ya miundombinu vigezo hivyo ni idadi ya watu (asilimia 70), hali ya umaskini (asilimia 20) na eneo la Halmashauri (asilimia 10). Ili kujenga uwezo wa Halmashauri ziweze kuendelea kuwa na sifa ya kupata ruzuku ya maendeleo dola za Marekani 35,000 zitatengwa kwa kila Halmashauri ambapo Halmashauri itapata ruzuku ya mfuto *(fixed sum)* ya dola 20,000 na kiasi kilichobakia kitagawiwa kufuatana na idadi ya watu asilimia 70, hali ya umaskini asilimia 20 na ukubwa wa eneo la Halmashauri asilimia 10.

Mheshimiwa Spika, fedha hizi zitatolewa bila masharti maalum kuhusu shughuli zitakazotekelezwa hivyo kuzipa Halmashauri wigo mpana wa kuamua. Kwa mara ya kwanza Halmashauri zitakuwa na uhuru wa kutumia fedha hizi kwa kulenga maeneo yatakayoboresha utoaji wa huduma muhimu kwa wananchi kama yatakavyoamuliwa na wananchi wenyewe. Natoa wito kwa Halmashauri zitakazopata fedha hizo kuzitumia

vizuri kwa manufaa ya wananchi na zile zitakazotumia fedha hizi vibaya zitachukuliwa hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Usafiri na Uchukuzi Vijijini unatekelezwa katika Halmashauri za Wilaya za Iramba, Muheza, Mbozi, Iringa, Rufiji, Masasi na Morogoro. Mpango huu umejihusisha na:-

(i) Kutengeneza njia za waendao kwa miguu vikiwemo vivuko na madaraja ya kuunganisha vijiji na huduma mbalimbali;

(ii) Kueneza wanyamakazi hasa matumizi ya punda na mikokoteni katika uchukuzi wa mizigo hivyo kupunguza adha ya kubeba mizigo mizito kichwani; na

(iii) Kusogeza huduma za jamii karibu na vijiji zikiwemo huduma za afya, masoko na vinu vya kusaga.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizofanyika katika mwaka wa fedha 2003/2004 ni pamoja na:-

(i) Uratibu wa shughuli za utengenezaji njia za waendao kwa miguu na kueneza wanyamakazi katika Wilaya za programu;

(ii) Kuandaa na kusambaza vipeperushi vya UKIMWI na usalama wa chakula kwa jamii *(food security);* na

(iv) Kufanya tathmini kwa ajili ya kueneza Mpango huu katika maeneo mengine.

(v) Kuendesha semina kwa Waheshimiwa Wabunge kuhusu mpango huu.

Kutokana na ukosefu wa fedha, lengo la kueneza mpango huu katika Halmashauri zingine 35 halikuwezekana. Katika mwaka wa fedha 2004/2005, Ofisi yangu itaendeleza juhudi za kuandaa mkakati wa kueneza mpango katika maeneo mengine ya Wilaya za majaribio na Mikoa kwa kushirikiana na Wahisani wanaosaidia mpango huu ambao ni Shirika la Kimataifa la Misaada la Norway *(NORAD),* Shirika la Kimataifa la Misaada la Denmark *(DANIDA),* Shirika la Kazi la Umoja wa Mataifa *(ILO),* Benki ya Dunia na Shirika la Maendeleo la Uswisi *(SDC).*

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa matengenezo ya barabara umeendelea kupokea fedha kutoka kwenye Bodi ya Mfuko huo na kuzigawa kwa ajili ya matengenezo ya Barabara za Jiji, Manispaa, Miji na Halmashauri zote za Wilaya za Tanzania Bara kulingana na programu za matengenezo ya barabara zilizoandaliwa na Halmashauri husika na kupitishwa na Mabaraza ya Madiwani. Matengenezo hayo ni matengenezo ya muda maalum *(periodic maintenance),* matengenezo ya dharura ya sehemu korofi *(spot improvement and emergency repair)* na matengenezo ya madaraja na makalvati. Kiasi kidogo cha fedha kilichotolewa kimetumika katika ufuatiliaji na usimamizi wa shughuli

za barabara ngazi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mikoa na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwishoni mwa robo ya tatu, jumla ya kilometa 4,328 zilikuwa zimefanyiwa matengenezo mbalimbali kati ya kilometa 12,784 zilizopangwa katika mwaka wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2003/2004, kazi ya ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za Mfuko wa Barabara imeendelea kufanywa na Bodi ya Mfuko kwa kusaidiana kwa karibu sana na Ofisi yangu pamoja na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Aidha, Ofisi yangu imeweza kufanya ukaguzi na ufuatiliaji wa fedha hizo katika Halmashauri zote. Kutokana na ukaguzi huo inaonyesha kwamba Halmashauri nyingi kwa sasa zina nidhamu ya matumizi ya fedha hizo kuliko miaka miwili iliyopita. Hali hii imejidhihirisha wazi katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2002/2003. Ofisi yangu itahakikisha kwamba taarifa ya mgao wa fedha za barabara zinazotolewa kwa Halmashauri zinaendelea kutangazwa magazetini na katika mbao za matangazo.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kwamba Halmashauri zote zinakuwa na uwezo wa kutengeneza bajeti zao za matengenezo ya barabara, kusimamia matengenezo hayo na kutoa ripoti za utekelezaji kwa ubora unaohitajika, Ofisi yangu kwa kushirikiana na wafadhili mbalimbali imeanzisha mfumo wa kompyuta wa kuendeleza shughuli hizo ujulikanao kama *District Road Maintenance System (DROMAS).*

Kwa sasa hivi mfumo huo unafanyiwa majaribio katika Halmashauri 12 na umeanza kuonyesha mafanikio yanayoridhisha. Halmashauri hizo ni Sengerema, Geita, Missungwi, Kwimba, Ukerewe, Magu, Bukombe, Kahama, Maswa, Ulanga, Ruangwa na Nachingwea. Kutokana na matokeo ya tathmini ya utekelezaji wa mfumo huu katika Wilaya za majaribio, Serikali itaangalia uwezekano wa kuueneza katika Halmashauri nyingine 12 katika mwaka wa fedha wa 2004/2005.

Lengo kubwa la Mfuko wa Barabara ni kuendelea kufufua barabara nyingi za vijijini ili ziweze kupitika wakati wote. Ofisi yangu ikishirikiana na Benki ya Dunia inatarajia kufanya tathmini *(Road Inventory and Condition Survey)* ili kuweza kujua urefu wa mtandao wote wa barabara za Miji na Wilaya tulizonazo. Kwa kufanya hivi utengenezaji wa barabara kwa kuzingatia umuhimu wake utatekelezwa vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2003/2004, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa iliendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa sera, mikakati na programu mbalimbali za sekta za Kilimo, Maliasili na Mazingira, Elimu, Afya, Maji, Ardhi, Makazi na Ushirika.

Mheshimiwa Spika, Ofisi yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula, Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, Wizara ya Ushirika na Masoko na wadau wengine, imejihusisha kikamilifu kutekeleza programu ya maendeleo ya sekta ya

kilimo katika Mikoa mitano ambayo utekelezaji wake ulianza mwaka wa fedha 2003/2004.

Jukumu la Ofisi yangu ni kuratibu programu hiyo katika sehemu ya uwekezaji ngazi ya Wilaya na Kijiji. Semina za kuwaelimisha watendaji ngazi za Mikoa na Wilaya zilifanyika kwa ajili ya kuwashirikisha viongozi na watendaji wa ngazi hizo kufanikisha programu hii ya maendeleo ya kilimo. Katika kuimarisha utendaji kazi, Halmashauri zilisisitizwa kuandaa programu zake za sekta ya kilimo kwa kushirikisha jamii kwa lengo la kuwawezesha wananchi kuongeza uzalishaji na kupunguza umaskini.

Katika mwaka wa fedha 2004/2005, Ofisi yangu itaendelea kuratibu utekelezaji wa Programu ya maendeleo ya kilimo katika Mikoa na Wilaya zilizo chini ya Mpango.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inalo jukumu la kuhakikisha kuwa suala la kutunza na kuendeleza mazingira *(conservation and management of environment)* linapewa msukumo unaostahili. Kazi hii inatekelezwa kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Kilimo na Chakula, Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, Wizara ya Ujenzi, Wizara nyingine za kisekta na Asasi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004 yafuatayo yametekelezwa:-

(i) Maandalizi ya utekelezaji wa awamu ya tatu ya mradi wa *Management of Natural Resources* unaofadhiliwa na Serikali ya Denmark yamekamilika kwa kuendesha semina kwa Wakurugenzi wa Halmashauri pamoja na watendaji, katika Wilaya 12 za Mikoa ya awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi huo. Mikoa hiyo ni Morogoro, Lindi, Mbeya na Iringa;

(ii) Maandalizi ya mradi huo katika Wilaya 25 za Mikoa 14 ambayo utekelezaji wake utaanza mwezi Julai, 2004 yamekamilika. Miradi katika Mikoa hii inafadhiliwa na Benki ya Dunia. Miradi yote katika Mikoa hiyo 18 inatumia mbinu shirikishi jamii *(Participatory Forest Management);*

(iii) Waraka wa Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wa mwezi Oktoba, 2003 kuhusu Uharibifu wa Mazingira na hususan vyanzo vya maji uliandaliwa na kupelekwa Mikoani;

(iv) Sheria ndogo 67 zilitungwa na kuanza kutumika katika Halmashauri husika; na

(v) Usimamizi wa matumizi endelevu ya maliasili ulifanyika kwa kuanzisha miradi mbalimbali kama vile ufugaji wa nyuki.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/2005, malengo yanayotarajiwa kutekelezwa ni:-

(i) Kuendelea kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Waraka wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa uliotolewa mwezi Oktoba, 2003 kuhusu Uharibifu wa Mazingira na hususan vyanzo vya maji;

(ii) Kusimamia na kuratibu shughuli za miradi shirikishi jamii *(Participatory Forest Management)* katika hifadhi ya mazingira;

(iii) Kuhimiza utungaji zaidi wa sheria ndogo na kuhakikisha kuwa zinatekelezwa;

(iv) Kuendelea kuwaelimisha viongozi mbalimbali kuhusu hifadhi ya mazingira; na

(v) Kuendelea kufuatilia utunzaji wa mazingira katika Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004, Serikali iliendeleza vita dhidi ya maadui watatu ambao ni ujinga, umaskini na maradhi kama ifuatavyo:-

(i) Katika kupambana na adui ujinga, Serikali iliendelea kuweka kipaumbele katika elimu kwa kusisitiza watoto wote walio na umri wa kuanza shule wawe wameandikishwa kuanza darasa la kwanza;

(ii) Kupitia mkakati wa Taifa wa kupambana na umaskini *(Poverty Reduction Strategy),* vita dhidi ya umaskini viliendelezwa kwa kushirikisha zaidi Mikoa na Halmashauri na wananchi katika kuboresha upatikanaji wa huduma muhimu;

(iii) Elimu katika vita dhidi ya janga la ugonjwa wa UKIMWI iliendelezwa katika Mikoa na Halmashauri ikiwa ni pamoja na kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa uchangiaji katika huduma ya afya; na

(iv) Kwa kushirikiana na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo na Halmashauri, Ofisi yangu iliendelea kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama. Mkazo uliwekwa katika kuwashirikisha wananchi kutunza vyanzo vya maji, uchimbaji wa visima na uanzishaji wa Kamati za Maji.

Katika mwaka wa fedha 2004/2005, Ofisi yangu itaendeleza vita dhidi ya umaskini, ujinga na maradhi kwa kuwashirikisha zaidi wananchi katika kutambua matatizo yao, kupanga mipango ya maendeleo, kufuatilia utekelezaji na kufanya tathmini katika lengo la kuboresha huduma za jamii.

Mheshimiwa Spika, suala la nyumba bora ni hitaji la msingi la binadamu na ni kielelezo cha ubora wa maisha. Katika mwaka wa fedha 2003/2004, Ofisi yangu iliendelea kusimamia uanzishaji na usajili wa vijiji pamoja na kuhimiza kuongeza kasi ya upimaji viwanja na kusimamia uendelezaji kwa kufuata kanuni za ujenzi.

Katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, Halmashauri zitaendelea kuhimizwa kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa kanuni za ujenzi ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa ujenzi unafanyika katika viwanja vilivyopimwa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi yangu iliendelea kushirikiana na Wizara ya Ushirika na Masoko katika kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa ushirika katika kujiletea maendeleo yao. Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, Ofisi yangu itaendelea kushirikisha zaidi Halmashauri kuimarisha vyama vya ushirika hasa vyama vya kuweka na kukopa, kufanya ukaguzi wa hesabu za Serikali za Vijiji, kutoa mafunzo na uanzishaji wa vikundi vya uzalishaji mali kama vile vya wakulima, wafugaji, wavuvi na wachimbaji wadogo wadogo wa madini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa iliidhinishiwa jumla ya shilingi 32,292,811,800.00 kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo, Mfuko wa Barabara na ruzuku kwa ajili ya Shirika la Elimu Kibaha.

Hadi kufikia mwezi Mei, 2004 jumla ya shilingi 21,483,524,985.60 zimepokelewa na zimetumika. Kati ya fedha hizo, shilingi 2,599,455,361.85 ziligharamia mishahara na matumizi mengineyo ya Ofisi Kuu. Shirika la Elimu Kibaha lilitumia shilingi 1,267,871,900.00 kugharamia mishahara na shilingi 797,471,775.00 kugharamia matumizi mengineyo. Aidha, shilingi 16,818,725,948.75 zilitumika katika Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Spika, Ofisi za Wakuu wa Mikoa ziliidhinishiwa jumla ya shilingi 28,999,826,500.00 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizi, shilingi 14,255,244,600.00 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 14,744,581,900.00 ni kwa ajili ya kugharamia matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi Mei, 2004 Mikoa imepokea jumla ya shilingi 22,937,806,925.00 kwa ajili ya kugharamia mishahara na matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ziliidhinishiwa jumla ya shilingi 290,973,801,000.00 na kati ya fedha hizi shilingi 230,024,524,600.00 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 60,949,276,400.00 ni kwa ajili ya kugharamia matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi Mei, 2004 Halmashauri zimepokea jumla ya shilingi 237,399,061,133.00 kugharamia matumizi ya kawaida zikiwemo shilingi 191,687,103,833.00 za mishahara na shilingi 45,711,957,300.00 za matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004, Bunge lako Tukufu liliidhinisha jumla ya shilingi 134,116,701,400.00 kugharamia utekelezaji wa miradi na programu chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kati ya fedha hizi shilingi 270,000,000.00 ni fedha za ndani na shilingi 133,846,701,400.00 ni fedha za nje. Hadi kufikia mwezi Mei, 2004 jumla ya shilingi 217,500,000.00 fedha za ndani na shilingi 91,141,748,170.00 fedha za nje zimetolewa na kutumika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004, Mikoa pamoja na Halmashauri zilitengewa jumla ya shilingi 35,490,957,200.00 kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizi shilingi 9,857,745,100.00 ni fedha za ndani na shilingi 25,633,211,100.00 ni fedha za nje. Hadi kufikia mwezi Mei, 2004 jumla ya shilingi 7,393,308,825.00 fedha za ndani zimetolewa na kutumika.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu napenda kuyashukuru Mashirika yasiyo ya Kiserikali, makundi mbalimbali na watu binafsi kwa michango yao ya hali na mali waliyotoa kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Aidha, natoa shukrani kwa Mashirika ya Umoja wa Mataifa, Mabenki na Wahisani mbalimbali waliochangia jitihada za Watanzania za kujiletea maendeleo. Mashirika ya Umoja wa Mataifa ni pamoja na *UNCDF, UNDP, UNICEF* na *IFAD,* Wahisani wengine ni pamoja na Umoja wa Nchi za Ulaya *(EU),* Serikali za Austria, Canada, Denmark, Finland, Ireland, Japan, Marekani, Norway, Sweden, Ubelgiji, Uholanzi, Uingereza, Ufaransa, Ujerumani, Uswisi, Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika.

Mheshimiwa Spika, Bajeti inayowasilishwa leo imeandaliwa kwa ushirikiano wa watumishi wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri. Napenda niwashukuru Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Mpanda Mashariki, Katibu Mkuu Bwana Deotrephes Mmari, Naibu Katibu Mkuu Bwana Damian Foka, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi na Wakurugenzi Wasaidizi katika Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wakurugenzi wa Halmashauri, Wakuu wa Asasi na Miradi iliyo chini ya Ofisi Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na wafanyakazi wote wa Ofisi yangu. Napenda pia kumshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kazi nzuri ya kuchapa hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niwasilishe Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2004/2005 ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2004/2005, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Asasi zake inaombewa jumla ya shilingi 36,604,007,500.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 6,559,839,200.00 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 30,044,168,300.00 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Kadhalika, jumla ya shilingi 141,324,747,200.00 zinaombwa kwa ajili kugharamia miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi 270,000,000.00 ni fedha za ndani na shilingi 141,054,747,200.00 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2004/2005, Ofisi za Wakuu wa Mikoa zinaombewa jumla ya shilingi 33,472,943,500.00 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 18,297,669,600.00 ni kwa ajili ya kulipia mishahara na shilingi

15,175,273,900.00 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Vile vile, Mikoa inaombewa jumla ya shilingi 39,177,314,000.00 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo zikiwemo shilingi 5,317,932,100.00 fedha za ndani na shilingi 33,859,381,900.00 fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2004/2005, Halmashauri za Miji zinaombewa ruzuku ya jumla ya shilingi 73,132,487,700.00 zikiwemo shilingi 52,405,241,800.00 kwa ajili ya mishahara na shilingi 20,727,245,900.00 kwa ajili ya matumizi mengineyo. Halmashauri za Miji zinaombewa jumla ya shilingi 905,213,300.00 fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2004/2005, Halmashauri za Wilaya zinaombewa ruzuku ya jumla ya shilingi 313,635,315,600.00 zikiwemo shilingi 229,145,858,000.00 kwa ajili ya mishahara na shilingi 84,489,457,600.00 kwa ajili ya matumizi mengineyo. Halmashauri za Wilaya zinaombewa jumla ya shilingi 4,548,100,600.00 fedha za ndani kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa muhtasari, nawasilisha makadirio ya matumizi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2004/2005 kama ifuatavyo:-

| | |
|---|---|
| OR-TAMISEMI | shilingi 177,928,754,700.00 |
| Ofisi za Wakuu wa Mikoa | shilingi 72,650,257,500.00 |
| Halmashauri za Miji | shilingi 74,037,701,000.00 |
| Halmashauri za Wilaya | shilingi 318,183,416,200.00 |
| Jumla | shilingi 642,800,129,400.00 |

Mheshimiwa Spika, majedwali mbalimbali yamegaiwa pamoja na hotuba hii ili kutoa ufafanuzi zaidi wa masuala yaliyoelezwa na kutoa mchanganuo wa Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio haya ya matumizi ya fedha kwa ajili ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. ATHUMANI S.M. JANGUO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 70(2) ya Kanuni za Bunge za mwaka 2004, naomba kutoa Maoni na Mapendekezo ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya 2003/2004 na

makadirio ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, kabla sijafanya hivyo, napenda kusema kwamba wale wote waliopatwa na mikasa tulikwishawapa pole na wanaostahili kupongezwa tumeshawapongeza. Moja kwa moja naenda kwenye majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Kamati hii yametajwa katika Kanuni za Bunge Na 92 (2) ya mwaka 2004 na yametajwa kama ifuatavyo:-

(a) Kushughulikia Bajeti za Wizara inazozisimamia.

(b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge ambayo chanzo chake ni Wizara inazozisimamia.

(c) Kushughulikia taarifa za kila mwaka za utendaji na hesabu zilizokaguliwa za Mashirika ya Umma yaliyochini ya Wizara hizo.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati hii ni kama walivyoainishwa katika Kanuni za Bunge Na 87 (1-2) na 93 (1) 2004 na ni hawa wafuatano Mheshimiwa Athumani Janguo, Mwenyekiti, Mheshimiwa George Lubeleje,Makamu Mwenyekiti na wajumbe ni Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Mheshimiwa Chifu Abdallah Fundikira, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Rosemary Nyerere, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga,Mheshimiwa Khamis Salum Ali, Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambate, Mheshimiwa Ramadhan Hashim Khalfan, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Pascal Degera, Mheshimiwa Nimrod Mkono na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa.

Mheshimiwa Spika, maagizo ya Kamati ambayo yalitolewa wakati tunapitisha Bajeti ya mwaka 2003/2004 ni haya yafuatayo:-

(a) Mfuko wa Pembejeo, Halmashauri za Wilaya zipewe uwezo wa kusimamia Mfuko wa Pembejeo.

(b) Ukosefu wa Ajira, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ishirikiane na Wizara nyingine katika kutafuta nama ya kukabiliana na tatizo la ukosefu wa ajira.

(c) Upungufu wa Watumishi wenye sifa hasa katika Idara ya Uhasibu, iandaliwe orodha ya Mikoa inayokabiliwa na upungufu huu, ielezwe jinsi upungufu wa Wahasibu unavyoathiri Hesabu za Mikoa/Halmashauri husika na hatua zinazochukuliwa ili kuirekebisha hali hiyo.

(d) Nafasi ya Makatibu Tarafa, Sheria Na.6 ya mwaka 1999 ifanyiwe marekebisho ili nafasi na majukumu ya Makatibu Tarafa yawekwe wazi.

(e) Ajira kwa Watendaji wa Vijiji, Kata na Mitaa; uandaliwe utaratibu maalum wa kusimamia ajira ya Watendaji wa Vijiji, Kata na Mitaa. Pia Watendaji hao wapewe elimu juu ya majukumu yao katika Chuo cha Hombolo au katika Vyuo vingine.

(f) Ofisi za Wabunge, juhudi zifanyike kutekeleza agizo la Kamati hii la mwaka 2002/2003 la kuwapatia Ofisi Wabunge wote wa Majimbo, wa Kuteuliwa na wa Viti Maalum, hususan katika Mikoa ambayo bado haijatekeleza agizo hilo.

(g) Kukabiliana na Majanga ya Moto, ianzishwe programu maalum ya kuwapatia Watumishi wa ngazi mbalimbali elimu kuhusu jinsi ya kukabiliana na janga la moto.

(h) Utungaji na uandishi wa sheria ndogo, Serikali za Mitaa zipatiwe mwongozo wa kutunga Sheria hizo na uwe unafanyiwa rejea mara kwa mara.

(i) Sheria ndogo zichapishwe kwa wingi na kusambazwa Wilayani na Vijijini.

(j) Mpango wa Maboresho ya Serikali za Mitaa; Mpango huu uzifikie Halmashauri zote na uhusishe pia kuboresha huduma zinazotolewa kama vile huduma za afya na upatikanaji wa maji safi na salama.

(k) Tatizo la Umaskini, Halmashauri za Wilaya zitenge fedha za kutosha kwa ajili ya mipango ya maendeleo inayolenga kupunguza hali ya umaskini inayowakabili Watanzania wengi.

(l) Mfumo wa uandishi wa taarifa, kuanzia mwaka wa fedha 2004/2005 Mikoa yote iwe na mfumo mmoja wa uandishi wa taarifa zinazowasilishwa mbele ya Kamati kulingana na maelekezo ya Hazina.Taarifa hizo zionyeshe ufananisho wa mwaka uliopita, mwaka uliopo na mwaka ujao.

(m) Maagizo yanayotolewa na Kamati yazingatiwe katika bajeti za Mikoa husika kwa mwaka unaofuata.

Mhehimiwa Spika, katika kuzipitia Bajeti, Kamati iliridhishwa na utekelezaji wa maagizo hayo katika ngazi ya Wizara na kwa Mikoa mingi. Baadhi ya Mikoa haikufuata mtiririko na mfumo uliowekwa na Hazina hata ikalazimika Mikoa ya Kilimanjaro na Mbeya iagizwe kwenda kuzifanyia marekebisho Bajeti zao. Mikoa hiyo ilileta tena bajeti zao zenye marekebisho hapa Dodoma tarehe 22 Juni, 2004.

Nafurahi kusema kuwa katika kikao hicho Bajeti ya Mkoa wa Kilimanjaro ilipitishwa. Lakini Kamati haikuridhishwa na Bajeti ya Mkoa wa Mbeya. Hivyo wakarudishwa tena na baada ya marekebisho ya ziada, bajeti hiyo ilipitishwa jana tarehe 23 Juni, 2004. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati hii ilikutana na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wakuu wa Mikoa yote 21 ya Tanzania Bara tarehe 25 Mei, 2004 na 26 Mei, 2004, ili kupitia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hiyo na Mikoa kwa Bajeti ya mwaka 2003/2004 na Mapendekezo ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2004/2005. Kutokana na baadhi ya Mikoa kutokutekeleza kikamilifu maagizo ya Kamati yaliyotolewa wakati wa bajeti ya mwaka 2003/2004, kama nilivyokwishasema hapo awali, kwamba Mikoa miwili ikaelekezwa kwenda kufanya marekebisho na kulazimika kurudi tena mbele ya Kamati tarehe 22 Juni, 2004 na 23 Juni, 2004.

Mheshimiwa Spika, katika kupitia utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2003/2004, Kamati iliona kuwa bado kuna matatizo ya utekelezaji kwenye mfuko wa pembejeo ambao kwa sasa unasimamiwa na Wizara ya Kilimo na Chakula, wakati walengwa wa mfuko huo wako kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine lenye matatizo ni ruzuku inayotolewa na Serikali kwa Halmashauri zote nchini ili kuziba pengo lililotokana na kufuta kodi zenye kero. Kamati inadhani kuwa fedha hizo hazitoshi na hazipelekwi kwa wakati na hivyo Halmashauri kushindwa kutekeleza majukumu yake ya asili kwa wananchi wake. Kamati inaona kuwa pamoja na Serikali kuwa na nia njema ya kuondoa kero ya utitiri wa ushuru wa Halmashauri, ipo haja ya kuweka utaratibu thabiti wa kuzisimamia vizuri Halmashauri zetu ili zisibweteke na ruzuku kutoka Serikali Kuu.

Kamati inahofia tusirudi nyuma kule kwenye nyakati za Mashirika ya Umma ambayo yalikuwa yakiweka mstari mbele ya Hazina.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia imeona kuwa bado kuna upungufu mkubwa wa Wataalam kwenye Halmashauri zetu na hasa Wahasibu. Upungufu huu utakuwa na athari sana kwa sasa kuliko wakati wowote mwingine kwa sababu Serikali sasa hivi inapeleka fedha nyingi kwenye Halmashauri zetu.

Kamati imeridhika na uamuzi wa Serikali wa kusomesha Wahasibu wa Halmashauri na Wahasibu kwa jumla. Hata hivyo huenda uwingi huo wa wataalam usizisaidie sana Halmashauri kama maslahi yao hayataboreshwa. Pia upungufu wa Wataalam hao umeathiri hata utayarishaji wa taarifa mbalimbali hali ambayo inasababisha baadhi ya Halmashauri kukosa kupewa ruzuku kwa sababu ya taarifa ambazo hazijadiliwi vizuri.

Aidha, Halmashauri nyingi hazipati hati safi kutokana na sababu mbalimbali ukiwemo ukosefu wa wataalam katika Halmashauri. Hali hii imesababisha Halmashauri hizo kunyimwa fedha za maboresho.

Kwa mujibu wa taarifa ya Waziri na kama alivyosema mwenyewe hivi karibu, katika mwaka 2004/2005 ni Halmashauri 47 tu nchini ambazo zitapata fedha za maboresho. Jana tulielezwa hapa na Waziri wa nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu na kutajiwa orodha ya Wilaya ambazo hazikupata ruzuku. Sisi tunaamini si sawa kwa hatua hii ya

Serikali ya kuwaadhibu wananchi kwa Halmashauri ambazo hazikutoa taarifa za marejesho kwa kosa ambalo siyo lao. Tunafikiri utaratibu ubadilishwe ili adhabu wapewe wanaokosa badala ya Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati imepitia kwa makini mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo kwa mwaka 2004/2005 na kuwa na maoni yafuatayo:-

Kamati imefurahishwa na uamuzi wa Serikali wa kutoa ajira kwa Maafisa Watendaji wa Vijiji, kuanzia mwezi Mei, 2004 ingawa zoezi hili lilitakiwa lianze tangu Julai, 2003. Hata hivyo, Kamati inashauri Serikali iharakishe utaratibu wa kuwaajiri Watendaji waliobaki. Kamati ilielezwa kuwa Serikali itaajiri Watendaji 4,240 tu kati ya Watendaji 10,000 wanaohitajika nchi nzima. Hawa wataajiriwa kwa mkataba wa majaribio wa miaka mitatu. Kamati ina maoni kuwa Kada hii ni muhimu sana katika kuhamasisha maendeleo, kwa hiyo ni muhimu pia wakapatiwa vitendea kazi hususan usafiri.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inakubaliana na uamuzi wa Serikali wa kumuweka Katibu Tarafa chini ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri. Hii itaondoa utata wa uwajibikaji wake katika kusimamia maendeleo ya Tarafa. Miaka ya nyuma, Katibu Tarafa aliwajibika moja kwa moja kwa Mkuu wa Wilaya wakati alikuwa anafanya kazi nyingi sana za Halmashauri. *(Makofi)*

Kamati pia imeridhika na uamuzi wa Serikali wa kuwapatia pikipiki Makatibu Tarafa wote nchini na ni matumaini yetu kuwa pikipiki hizi zitaongeza ufanisi katika utendaji kazi wao. Hata hivyo, Kamati inashauri ili Makatibu waweze kuzimudu kazi zao vizuri, hapana budi wapatiwe wasaidizi na vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, wote tunajua hali ya ubovu wa barabara zetu huko Vijijini. Matengenezo hayafanyiki kila wakati na hivyo kutopitika kirahisi. Hali hii inatokana na ufinyu wa fedha zinazotengwa kwa ajili hiyo. Tunaishauri Serikali kuwa katika kuimarisha barabara nchini, mkazo mkubwa uwekwe kwenye barabara za vijijini.

Mheshimiwa Spika, katika matumizi ya miradi ya maendeleo, Kamati imegundua kuwa kuna matumizi mabaya na kutojali matatizo ya Maofisa kwenye ofisi na makazi yao. Kwa ajili hiyo, baada ya kudokezwa matatizo ya Mkoa wa Pwani, Kamati iliamua kukagua miradi michache ya Mkoa huo ikiwemo jengo la Utawala la Mkoa, ukarabati wa nyumba ya Mkuu wa Mkoa na ofisi na nyumba ya kuishi ya Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo.

Hali ya majengo hayo yote hairidhishi. Jengo la Utawala la Mkoa ambalo limekuwa likikarabatiwa kwa fedha nyingi mwaka hadi mwaka tangu 1999, linaathiriwa na ardhi mbaya ya udongo wa mfinyanzi na utaalamu mbovu wa kiuhandisi wakati michoro ilipofanywa. Ofisi ya Mkuu wa Wilaya inasababishwa na uzee wa jengo la zamani ambalo lilijengwa tangu enzi za Wajerumani. Lakini nyumba ya Mkuu wa Wilaya inaathiriwa na usimamizi mbovu katika ngazi ya Wilaya na Mkoani.

Kamati pia inayo taarifa kuwa kumekuwa na matumizi mabaya ya fedha kwenye utekelezaji wa ukarabati na ujenzi wa baadhi ya majengo katika Wilaya nyingine ndani ya Mkoa wa Pwani. Kamati imeamua kukutana na viongozi wa Mkoa na Wilaya husika hapa Dodoma tarehe 28 Juni, 2004. Kama Kamati haitaridhika na maelezo tutakayopewa hapa Dodoma, Kamati inaamua kupeleka Tume katika maeneo husika ili kujiridhisha na hali ilivyokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2004/2005 inaonyeshwa kuwa kila Ofisi ya Mkuu wa Wilaya imetengewa shilingi milioni 2 tu kwa mwaka. Fedha hizo hazitoshi hata kidogo tukichukulia majukumu waliyonayo viongozi hao. Fedha hizo hazitoshi kuwawezesha Wakuu hao kuyafikia maeneo yao ili kusimamia maendeleo na maagizo mbalimbali ya Serikali. Matokeo yake ni Wakuu hawa kuwa ombaomba wa mafuta, matengenezo ya magari yao na hata posho za safari kutoka kwa Halmashauri na wafadhili wengine. Hali hii siyo nzuri hata kidogo kwani itawaondolea Wakuu hao uwezo wa kutoa maamuzi huru katika kusimamia shughuli za Wilaya zao. *(Makofi)*

Aidha, imeonekana kuwa katika Wilaya nyingi nchini ama Wakuu wa Wilaya hawana Ofisi zenye hadhi ya nyadhifa zao au hawana nyumba nzuri za kuishi, hali ambayo inaweza kuathiri utendaji wa kazi zao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na Wizara katika kurahisisha mchakato wa kutunga sheria ndogo za Halmashauri, bado kuna ucheleweshaji mkubwa katika kusainiwa sheria hizo . Mara nyingi sheria hizo hukamilika wakati lengo la mwaka huo limeshapita au msimu umemalizika. Mheshimiwa Waziri aliieleza Kamati kuwa lilikuwepo tatizo ambalo sasa hivi limeshatatuliwa kwa sababu kulikuwa na upungufu wa Wanasheria katika Wizara yake ambao sasa Wanasheria wachache wamepelekwa Wizarani. Kamati inashauri kuwa Serikali itafute kila njia ili kutatua tatizo hili haraka.

Mheshimiwa Spika, baada ya maoni hayo, Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

Kwanza, Kamati inashauri kuwa Mfuko wa Pembejeo usimamiwe na TAMISEMI badala ya Wizara ya Kilimo kama ilivyo sasa ili mfuko huo uweze kuwafikia walengwa haraka. Ili kutekeleza hili Serikali inashauriwa kuleta sheria ya marekebisho kwenye sheria iliyounda mfuko huu.

Pili, Kamati inashauri kuwa fedha za ruzuku kwa Halmashauri ziongezwe na zipelekwe kwenye Halmashauri moja kwa moja badala ya kupitia Ofisi ndogo za malipo Mikoani *(Sub-Treasury)*.

Tatu, Serikali iweke utaratibu utakaozivutia na kuziwezesha Halmashauri hatimae ziweze kujitegemee kifedha, nne, Serikali ipeleke katika Halmashauri zetu wataalam wa fani zote wakiwemo Wahasibu, Wahandisi, Maafisa Mipango na kadhalika ili kusimamia majukumu mbalimbali ya kitaaluma katika Halmashauri hizo. Uamuzi huo uende sambamba na kuboresha mazingira ya wafanyakazi na tano, Serikali iangalie upya Sheria

ya Mfuko wa Barabara ambayo inazigawia Halmashauri asilimia 30 tu ya mapato yote ya mfuko huo, ili kiwango hicho kiongezwe kwa lengo la kukidhi hali halisi ya barabara zetu vijijini.

Mheshimiwa Spika, sita, Serikali iangalie kwa makini kiwango kinachotolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya Mkuu wa Wilaya ili kiwango hicho kiwiane na majukumu yake, saba, Serikali iangalie uwezekano wa kuwajengea mazingira mazuri ya kazi Wakuu wa Wilaya kwa kuwajengea Ofisi na nyumba za kuishi ikiwa ni pamoja na kuwahamasisha wananchi kushiriki katika ujenzi huo na nane, Serikali iweke utaratibu wa kudumu wa kukagua utekelezaji wa miradi Mikoani ili kuhakikisha kuwa fedha itolewayo inatumika vizuri. Panapotokea matumizi mabaya basi wahusika wawajibishwe.

Mheshimiwa Spika, tisa, Wizara ichukue hatua za makusudi kuhakikisha kuwa sheria ndogo za Halmashauri hazicheleweshwi kiasi cha kukosa maana zinapokuwa zimesainiwa na kumi, Kamati inapendekeza fedha za maboresho zitolewe kwa Halmashauri zote na wananchi wasiadhibiwe kwa kosa ambalo siyo lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inayakubali mapendekezo ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Mapato na Matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo kwa Mikoa na Halmashauri zenye jumla ya shilingi 642,800,129,400 kwa mgawanyo ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, Fungu 56, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Matumizi ya kawaida shilingi 36,604,007,500/= na Miradi ya Maendeleo shilingi 141,224,747,200/=.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mikoa na Halmashauri, Matumizi ya kawaida shilingi 420,240,746,800/=, Miradi ya Maendeleo shilingi 44,630,627,900/= na jumla shilingi 642,800,129,400/=.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi kuwa mchangiaji wa kwanza baada ya hotuba ya Waziri wa TAMISEMI. Napenda pia nimshukuru Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Brigedia Jenerali (Mstaafu) Hassan Ngwilizi, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, Katibu Mkuu, Ndugu Mmari, Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa wote Tanzania Bara na Watumishi wote wa Wizara pamoja na Mikoa kwa ushirikiano wao wakati tunajadili bajeti yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi maalum ya kuwashukuru Wabunge, Wajumbe wenzangu kwenye Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa uchambuzi na michango kwa masuala mbalimbali wakati wa kujadili utekelezaji na mapendekezo ya bajeti ya Wizara.

Pia nataka kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Kipenka Mussa na Makatibu wa Kamati hii Ndugu Ernest Zulu na Ndugu Aggrey Nzowa, kwa kuihudumia Kamati hii vizuri wakati wote.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii na nawaomba Waheshimiwa Wabunge waijadili hoja ya Mheshimiwa Waziri pamoja na maoni ya Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante, baada ya kumsikiliza Msemaji wa Kambi ya Upinzani, wachangiaji wanne wa mwanzo ni Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa James Musalika na Mheshimiwa Profesa Daimon Mwaga.

Sasa namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou.

**MHE. DR. AMANI W. A. KABOUROU - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa fursa hii kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2004/2005 kwa mujibu wa Kifungu cha 43 (5) (c) cha Kanuni za Bunge, Toleo la 2003.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Mhe. Brigedia Mstaafu Hassan Ngwilizi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, Naibu Waziri, Wakuu wa Mikoa wote, Bwana D. Mmari, Katibu Mkuu TAMISEMI na timu yake ya wataalam waliosaidiana kuandaa Hotuba hii ya Bajeti inayolenga kuboresha maisha ya Watanzania. Pamoja na pongezi hizo Kambi ya Upinzani inaamini kwamba bado yapo maeneo katika bajeti hii ambayo yanahitaji maboresho ili kuleta ufanisi kiutekelezaji.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuwapa pole Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda kwa kufiwa na baba yao mzazi Mzee Omari Kigoda. Mola ailaze pema peponi roho ya marehemu. *Amin.*

Vile vile niwape pole Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan kwa msiba wa binti yake, Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere kwa kupata ajali ya gari, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela kwa mkasa wa majambazi, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya kwa kupigwa na kujeruhiwa katika harakati za siasa. Kwa Waheshimiwa hawa wote nawaombea tu wawe na mioyo ya subira kwani kama wasemavyo Waswahili hujafa hujaumbika.

Mheshimiwa Spika, tunapenda kusema kwamba tunataka tu kutoa tathmini ya yale ambayo yaliwasilishwa hapa na Wizara ya TAMISEMI mwaka 2003/2004 na ambayo tunaamini yalisemwa vizuri katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Lakini

tunatoa tathmini hiyo ili tuondokane na tabia au utamaduni wa kupongezana bila kujua kwa kweli matokeo ya haya yaliyosemwa.

Mheshimiwa Spika, tungependa tusilazimike kurudia rudia malalamiko kuhusu kukosekana ufanisi katika Wizara hii lakini tunajikuta hatuna budi kufanya hivyo kwani Wizara aidha imeshindwa au inakataa makusudi kutimiza wajibu wake kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya TAMISEMI kwa Kamati ya Bunge ya Katiba Sheria na Utawala ya mwezi Mei 2004 iliyotolewa Jijini Dar es Salaam, dira ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ni kuziwezesha Halmashauri kujiendesha kwa misingi ya Utawala Bora na kutoa huduma bora kwa wananchi kwa misingi endelevu. Ili kufanikisha dira hiyo majukumu ya TAMISEMI yamefafanuliwa.

Majukumu hayo yamegawanywa katika mafungu mawili yaani ya kisera na kiutendaji. Majukumu ya kisera yanalenga katika kuendeleza umoja na mshikamano wa Kitaifa, hali ya amani na utulivu nchini, kuchochea na kuhimiza ukuaji wa uchumi kwa maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla, kusimamia maendeleo ya kijamii hususan elimu, afya, maji na barabara Vijijini na mwisho kujenga na kuimarisha demokrasia na utawala bora.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya kiutendaji yanayolenga kufanikisha sera ni kama yafuatayo:-

(a) Kujenga uwezo wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika kusimamia Tawala za Mikoa.

(b) Kuratibu na kusimamia Tawala za Mikoa ili ziweze kuzisaidia Halmashauri katika kutekeleza wajibu wake.

(c) Kuratibu utekelezaji wa sera ya maendeleo vijijini na mkakati wake.

(d) Kuendeleza programu ya uboreshaji wa mfumo wa Serikali za Mitaa nchini ili kuziwezesha Halmashauri kutoa huduma bora.

(e) Kuzijengea Serikali za Mitaa uwezo wa kusimamia ukusanyaji wa mapato na matumizi.

(f) Kuboresha miundo, taaluma, maslahi ya watumishi na mifumo ya kazi katika Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mikoa na Halmashauri.

(g) Kusimamia Taasisi, Mashirika ya Umma na miradi inayotekelezwa chini ya TAMISEMI.

(h) Kuratibu shughuli za hifadhi ya mazingira.

(i) Kuratibu vita dhidi ya Ukimwi na Rushwa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais pia imekasimu baadhi ya majukumu yake ya kiutendaji kwa Mikoa. Majukumu hayo ni:-

(a) Kuzijengea Halmashauri uwezo wa kutekeleza shughuli zake za kila siku.

(b) Kutoa ushauri wa kitaalam kwa Halmashauri ili ziweze kutoa huduma bora kwa wananchi.

(c) Kuhakikisha kwamba kunakuwepo amani na utulivu katika Mikoa.

(d) Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya serkali na sera za kisekta katika Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, tukizingatia wingi na unyeti wa majukumu yote haya yaliyoorodheshwa hapo juu, tunalazimika kuona kuwa matatizo mengi na mzigo mkubwa unaoielemea Wizara hii ni ya kujitakia. Hapana shaka kuwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ni mfano dhahiri wa dhana ya ukiritimba katika utawala wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba yetu Sura ya Nane, vifungu vya 145 na 146 Serikali za Mitaa ndiyo Mamlaka halali inayostahili kushughulikia asilimia themanini ya majukumu yote yanayoshughulikiwa na Wizara hii. Kambi ya Upinzani ingependa kujua ni kwa nini mpaka sasa hakuna Wizara mahsusi inayoshughulikia Serikali za Mitaa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano mdogo hapa unaweza ukatuonyesha ni kwa vipi TAMISEMI imejitwika mzigo isiouweza na usiokuwa wake Kikatiba. Akijibu hoja ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu upungufu wa watumishi wenye sifa ndani ya idara za Uhasibu, Waziri katika Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mheshimiwa Brigedia Mstaafu Hassan Ngwilizi, aliitaja Mikoa yenye upungufu mkubwa wa wahasibu wenye sifa kuwa ni Mtwara, Lindi, Iringa, Kigoma, Kilimanjaro na Manyara. Alisisitiza kuwa ili Halmashauri ziweze kufanya kazi vizuri zinatakiwa kuwa na wahasibu wenye sifa. Aliongeza kwamba: "Na kwa kuwa Halmashauri nyingi zina watumishi wachache wenye sifa, baadhi ya Halmashauri zimeshindwa kufunga kwa wakati hesabu zao na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali."

Aliendelea kudai kuwa: "Hesabu hizo vile vile zimekuwa na mapungufu mengi kama vile mahesabu kuandikwa chini ya kiwango, Halmashauri nyingi kupata hati chafu au zenye masharti, ushauri mbaya wa matumizi ya ruzuku, utunzaji mbovu wa hesabu na upotevu wa nyaraka."

Mheshimiwa Spika, akielezea hatua zinazochukuliwa na Wizara yake kupambana na hali hiyo Mheshimiwa Hassan Ngwilizi, aliifahamisha Kamati hiyo ya Bunge kuwa Serikali imepeleka jumla ya Wahasibu 285 katika Vyuo mbalimbali vya Uhasibu hapa

nchini kuchukua mafunzo ya *Postgraduate Diploma in Accountancy* na *Advanced Diploma in Accountancy.* Pia kwamba Serikali imetoa vibali 15 vya ajira za Wahasibu 7 na Wakaguzi wa Ndani 8 na kuahidi kwamba vibali hivyo vitaendelea kutolewa kadri uwezo wa Serikali utakapopatikana na papo hapo akakiarifu kikao kuwa baadhi ya Halmashauri zimetumia Wahasibu wa kuazima ili kuweza kufunga hesabu zao kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Mheshimiwa Hassan Ngwilizi kwa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu mapungufu ya shughuli za uhasibu katika Halmashauri zetu inafaa itafakariwe kwa kina.

Kwanza, ni dhahiri kuwa hata pale Serikali inapokuwa tayari kulishughulikia tatizo hili bado inakuwa haina uwezo wa kulikabili kikamilifu. Hivi ni kwa kiwango gani wanafunzi hao waliopelekwa masomoni wataweza kupunguza tatizo la Uhasibu nchini. Kwa maana nyingine Wahasibu hao, watakapokuwa wamehitimu mafunzo yao, watapunguza tatizo hili kwa kiasi gani, asilimia mia moja, arobaini, tano au ngapi?

Wakati tukiwasubiri wahitimu mafunzo yao ni nani atakayedhibiti ufisadi na ubadhirifu ambao umekuwa adha katika Halmashauri zetu mwaka hadi mwaka? Hivi kweli vibali 15 vilivyotolewa na Serikali vitakidhi haja ya Halmashauri zenye upungufu mkubwa kama alivyosema Mheshimiwa Waziri katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Iringa, Kigoma, Kilimanjaro na Manyara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata katika kuonyesha kwake kukata tamaa kuhusu hali mbaya kihasibu Mheshimiwa Waziri bado alikiri mbele ya kikao kuwa baadhi ya Halmashauri zimetumia Wahasibu wa kuazima ili kuweza kufunga hesabu kwa wakati. Hivyo cha kuzingatia hapa ni ukweli kwamba kwa kutumia uwezo wa soko huria la taaluma, Halmashauri kadhaa zimefanikiwa kukamilisha mahesabu yake katika muda muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kukumbusha tu ile methali ya Kiswahili isemayo samaki huoza kuanzia kichwani. Kama ni kweli kuwa utunzaji sahihi wa mahesabu ndiyo msingi wa maendeleo na kwa kuwa Wizara imekiri kuwa wengi wa Wahasibu walioko kwenye Halmashauri wana uwezo usiokidhi haja ya majukumu yao, hivi inakuwaje tuendelee kuwa na imani kuwa Wizara inao uwezo wa kurekebisha hali hiyo? Sasa ni kwa nini Halmashauri zenyewe zisifanye utaratibu wa kuajiri watu wenye sifa nzuri ambao kwa bahati mbaya au nzuri tuseme hawakuwemo Serikalini na hivyo hawapewi ajira katika Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni vema ikakumbukwa kuwa karibu watendaji wote wa Halmashauri wamerithiwa kutoka Serikali Kuu. Hivyo basi, kama ni kweli kuwa baadhi au wengi wa watendaji hao katika fani ya Uhasibu wameonyesha kutokidhi viwango vya ubora, hivi haiwezekani hali ikawa hivyo hivyo hata kwenye fani nyingine kama Utumishi, Uhandisi na kadhalika?

Je, Waziri anasema nini kuhusu rai kwamba kukosekana kwa ufanisi kwa kiwango kinachoridhisha katika Wizara yake kunatokana na kuwepo watendaji wengine wengi tu katika fani mbalimbali ambao wamepewa ajira wasizostahili?

Mheshimiwa Spika, wakati akitoa hotuba ya Mwaka wa Fedha 2003/2004 kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kuhusu TAMISEMI Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa alikuwa na haya ya kusema kuhusu TUMITAA: "Sasa napenda kwa kifupi nigusie suala la TUMITAA. Siku za hivi karibuni kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa Madiwani wa Halmashauri mbalimbali kuhusu Watendaji na jinsi malalamiko yao yanavyoshughulikiwa. Malalamiko yametokea kwenye Halmashauri tofauti zikiwemo Manispaa kama ya Morogoro, Korogwe, Arumeru, Karatu, Songea na kadha wa kadha. Mgogoro mara nyingi unatokana na Madiwani kulalamikia utendaji kazi mbovu, matumizi mabaya ya fedha za Halmashauri, ubadhirifu na kadhalika. Kambi ya Upinzani inadhani malalamiko hayo yatazidi kuongezeka jinsi Madiwani wenye kujua wajibu wao watakavyoongezeka." Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa aliiomba Serikali kuchukua hatua za haraka kutafuta msingi wa matatizo hayo na kuiasa isitoe majibu ya haraka haraka kama vile kusema Madiwani wasiingie jikoni, Madiwani wawaachie watendaji kufanya kazi zao na kadhalika.

Napenda kusisitiza wosia huo wa Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa na napenda pia kumwuliza Mheshimiwa Waziri kama amejaribu kufanya tathmini kuhusu malalamiko hayo ya wanasiasa dhidi ya watendaji na kujiridhisha kuwa kilio chao hakitokani na udhaifu katika utendaji?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ingependa ipate jibu. *(Makofi)*

Pamoja na kwamba kuna uwezekano kuwa Wizara hii inajihusisha na majukumu yanayoizidi uwezo kwa sababu Halmashauri hazijawa na uwezo wa kuyakabili majukumu hayo kikamilifu, cha kushangaza ni kwamba Wizara haina malengo yoyote ya muda mfupi au mrefu ya kuziachia Halmashauri madaraka yake ya Kikatiba katika maeneo zinakotawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba Katiba yetu imezipa mamlaka hizi uwezo wote katika maeneo husika, tangu ulinzi wa amani, ukusanyaji na utumiaji wa mapato, hadi ukuzaji wa demokrasia. Sasa hivi haki hii imehodhiwa na TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, wakati akijibu swali namba 90 la Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, aliyetaka kujua kwa nini Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa amenyang'anywa uwezo wa kuteua Madiwani watano katika Halmashauri baada ya uchaguzi wa Madiwani wakati Rais amepewa uwezo wa kuteua Wabunge kumi, Mheshimiwa Pinda, Naibu Waziri TAMISEMI alisema, naomba kunukuu: "Aidha, kwa mujibu wa vifungu 145 na 146 vya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 2000, Serikali za Mitaa ni Serikali kamili zenye majukumu ya kisheria ya kuhakikisha utekelezaji wa Sheria ya Ulinzi wa wananchi, na

kuimarisha demokrasia na kutumia demokrasia kuharakisha maendeleo ya wananchi katika eneo lake."

Mheshimiwa Mizengo Pinda aliendelea kufafanua kuwa: "Sababu ya msingi ya kufutwa kwa uwezo wa kisheria wa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa kufanya uteuzi wa Madiwani zinatokana na mahitaji ya Kikatiba ya kupeleka madaraka zaidi kwa wananchi ili kuwawezesha wananchi kuchagua viongozi wao wanaowapenda ikiwa ni pamoja na Madiwani. Marekebisho hayo yalifanyika ili kuimarisha ushirikishaji wa wananchi na viongozi wao katika kubuni, kupanga, kutekeleza na kusimamia shughuli zao za maendeleo katika maeneo yao pasipo kuingiliwa na Serikali Kuu. Mheshimiwa Mizengo Pinda alimalizia kwa kubainisha sababu pekee zinazoweza kuipa uhalali Serikali Kuu kuingilia masuala ya Serikali za Mitaa kwa kusema kuwa: "Endapo itabainika kuwepo ushahidi wa kutosha kuwa Halmashauri ama ya Wilaya au ya Mji itashindwa kutekeleza wajibu na kazi zake zilizowekwa kisheria, basi Serikali Kuu italazimika kutumia sheria, taratibu na kanuni zilizopo kuchukua hatua zinazostahili."

Mheshimiwa Spika, kauli hii ya Serikali iliyotolewa na Mheshimiwa Mizengo Pinda ni kielelezo tosha kuwa watendaji wengi katika Wizara hii waliopelekwa kwenye ngazi za Halmashauri za Wilaya na Miji ama hawaelewi dhana hii ya mgawanyo wa madaraka kikatiba au wanafanya mambo makusudi yaani *mind set* zao bado zipo kule walikotoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya Mheshimiwa Pinda hakuweka wazi ni mamlaka ipi yenye uwezo wa kuamua kwamba Halmashauri fulani imeshindwa kutekeleza wajibu wa kazi zake zilizowekwa kisheria. Hatujui sasa kama uchunguzi na kisha uamuzi wa kuichukulia hatua Halmashauri iliyoshindwa kuwajibika hufanywa na watendaji wa TAMISEMI au Mahakama!

Mheshimiwa Spika, hapa Kambi ya Upinzani ingependa kutoa wito kuwa nafasi mbili za kiutendaji, ile ya Mkuu wa Wilaya na Katibu Tarafa ziangaliwe upya kwani tunaamini kuwa matatizo mengi yanayojitokeza kati ya Wakuu wa Wilaya na Viongozi wa kuchaguliwa ni moja ya vikwazo vikubwa katika uimarishaji wa moja ya majukumu muhimu ya kisera ya TAMISEMI. Jukumu hilo ni kujenga na kuimarisha Demokrasia na Utawala Bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Wakuu wa Wilaya tayari wamekwishajitwalia madaraka ya kuzituhumu na kuzihukumu Halmashauri kwa madai kuwa zimeshindwa kutekeleza wajibu wake. Moja ya mbinu wanazotumia ni kuihusisha Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya kufikia maamuzi yanayokinzana na yale ya Madiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuwepo kwa Kamati ya Ulinzi na Usalama katika ngazi ya Wilaya ambayo haiwashirikishi viongozi wa kuchaguliwa katika Wilaya husika ni ukiukwaji wa Katiba yetu inayotamka wazi kuwa ulinzi na usalama ni jukumu la Serikali za Mitaa katika maeneo husika. Kwa mantiki hiyo Kamati hizi katika mfumo wake wa sasa ni kikwazo katika kufanikisha dhana ya Demokrasia na Utawala Bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati hizi za Ulinzi na Usalama zimetumika katika baadhi ya Wilaya kumpa nguvu Mkuu wa Wilaya kutoa amri zinazolenga kuwadhalilisha viongozi wa kuchaguliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali haijasema lolote kuhusu malalamiko mengi tu dhidi ya Wakuu wa Wilaya, Kambi ya Upinzani inasisitiza kuwa ni vema TAMISEMI iliangalie suala hili kwa undani kwani Kamati hizi zinatumika kutoa maamuzi yanayokiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hasa pale zinapoingilia na kusitisha maamuzi halali ya Madiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa TAMISEMI imetoa taarifa kwenye Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu marekebisho yaliyofanywa katika Sheria Na. 6 ya Mwaka 1999 kulingana na maelekezo ya kikao cha Baraza la Mawaziri, mabadiliko hayo bado hayajafikishwa kwa wadau kikamilifu. Ni Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri tu ndio waliokuwa na taarifa hiyo hadi sasa. Kambi ya Upinzani inashauri kuwa watendaji hao wafanye haraka kufikisha mabadiliko hayo kwa Madiwani ili kuepusha migongano ya kimajukumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na hayo niliyoyasema hapo juu, tunaamini kuwa malalamiko mengi yanayoikumba Wizara hii kama hotuba ya Kambi ya Upinzani ya Mwaka wa Fedha 2003/04, livyoyaorodhesha ni matokeo ya Wizara kukosa mwelekeo. Tunafahamu kwa mfano kuwa hata Dira yetu ya Taifa imejiwekea kikomo cha lini matarajio yake yatafikiwa *(Vision 2025)*. Kwa bahati mbaya dira ya TAMISEMI haisemi Wizara hii itajihusisha na majukumu iliyopangiwa hadi lini, ili angalau wananchi wawe na matumaini kuwa ipo siku watakuwa huru kujiamulia na kisha kutekeleza kile walichojiamulia wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha pale wananchi wanapofanya chaguzi kikatiba kuwachagua viongozi wao katika ngazi za Wilaya, Vijiji, Mitaa na Vitongoji na halafu wakashuhudia kuwa viongozi hao waliowachagua wenyewe hawana maamuzi ya mwisho katika kuwatatulia kero zao.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, vyovyote vile utakavyotaka kuuangalia uamuzi wa kuwaondoa Madiwani kwenye Bodi za *Tender* za Halmashauri, kwa wananchi walio wengi, kitendo hicho kinamaanisha kuwa Madiwani hawaaminiki na kwamba Serikali Kuu inawaamini watendaji wake zaidi ya viongozi waliochaguliwa na wananchi kidemokrasia. *(Makofi)*

Katika hili, Kambi ya Upinzani ingependa kupata tathmini ya TAMISEMI inayoonyesha kumekuwa na mafanikio gani dhidi ya rushwa na ufisadi katika Halmashauri zetu tangu Madiwani waondolewe toka kiungo hiki muhimu katika shughuli za usimamizi wa mali ya Umma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dhana kwamba Serikali Kuu inaziyumbisha Halmashauri inazidi kujengeka kwa wananchi wa kawaida kwa sababu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imekuwa ikiingilia sana utendaji wa Halmashauri. TAMISEMI

imekuwa ya kwanza kuhalalisha maamuzi yeyote ya Serikali Kuu hata kama uamuzi husika hauendani na hali halisi. Kwa mfano, kitendo cha Serikali kufuta kodi mbalimbali kwa madai kuwa zote hizo zilikuwa ni kero kwa wananchi bila kujali mazingira ya Halmashauri husika ni ushuhuda wa kutozingatia Katiba ya nchi.

Mheshimiwa Spika, cha kushangaza zaidi ni pale Wizara ilipochukua dhamana ya kuahidi kuwa pato lililokuwa likikusanywa na mamlaka hizo lingefidiwa na Hazina. Lakini sote ni mashahidi kuwa Hazina haikuzifidia Halmashauri kwa kiwango zilizopoteza na hivyo kupelekea miradi mingi iliyokuwa ikitegemea mapato yaliyokusanywa na Halmashauri zenyewe kusimama. Hali hii imejenga ufa kati ya wananchi na Madiwani wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine kutofidiwa kikamilifu kumeleta manung'uniko makubwa kwa upande wa Madiwani ambao kama sote tunavyofahamu hawalipwi mishahara na kwamba posho zao zinaweza kuongezeka pale tu wanapozikusanyia Halmashauri zao mapato ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kweli wengi katika Halmashauri zetu walitegemea kuwa Wizara hii ndiyo ingekuwa mtetezi mkubwa dhidi ya ufutaji kodi huo kwani ni dhahiri kuwa kwa sababu mwaka wa fedha wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ni tofauti, kwa vyovyote vile mabadiliko yeyote yaliyofanywa au yanayofanywa bila mashauriano kati ya ngazi hizi mbili za Serikali yaani Serikali za Mitaa na Serikali Kuu yana athiri ufanisi wa Halmashauri zetu ambazo mara nyingi hukutwa hazijajitayarisha kwa maamuzi hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kadhalika kumekuwa na malalamiko mengi katika Halmashauri kadhaa kuhusu majukumu ya TAMISEMI hususan katika zile zinazoongozwa na Vyama vya Upinzani. Halmashauri za Wilaya ya Karatu na ile ya Mji wa Kigoma Ujiji zinazoongozwa na Chadema, mathalan, zimeingizwa kwenye migogoro ya kisiasa na kiutendaji kwa utashi wa Wakuu wa Wilaya, kinyume cha sheria, ambao wamediriki hata kuwashawishi watendaji wa Halmashauri kutowatii Madiwani. Kwa bahati mbaya sana wameweza kufanya hivyo bila wasiwasi wowote *(with impunity),* kitu ambacho ni kinyume na matarajio ya dira ya TAMISEMI inayolenga katika kujenga na kuimarisha Demokrasia na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, kuanzia tarehe 4 Machi, 2004 hadi tarehe 20 Juni, 2004 Halmashauri ya Mji wa Kigoma Ujiji imefanya matumizi ya mamilioni ya fedha, imeajiri wafanyakazi zaidi ya mia mbili, imeuza mali za umma, na mengine mengi tu bila idhini ya kikao chochote cha Madiwani. Vitendo vyote hivyo vimefanywa na watendaji kwa idhini ya Mkuu wa Wilaya ya Kigoma. Ni dhahiri kuwa uendeshaji wa Halmashauri kwa mtindo huu ni ukiukaji wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa ningependa kutahadharisha kuhusu dhana ya vurugu inayoonekana kuzungumziwa sana katika kipindi hiki cha uchaguzi. Kumekuwa na kauli kutoka kwa viongozi kwamba kuna watu hasa Wapinzani wanaoandaa vurugu.

Wapinzani tumewahi kusema humu na napenda kurudia kauli ya Mheshimiwa Teddy Kassella-Bantu kwamba makubaliano ambayo sasa tunaambiwa ilikuwa ni ushauri na tunaona ajabu ni vipi ushauri uletwe mpaka huku Bungeni na waletwe viongozi wa Vyama vya Siasa, makubaliano yaliyofikiwa kuhusu wagombea binafsi kwenye ngazi za chini kabisa, utayarishaji wa daftari la wapiga kura, yote yamesahauliwa na tumeambiwa kwamba tulikuwa tunashauriwa tu.

Sasa tunasema, hayo nayo ni maandalizi ya vurugu kwa sababu imekubalika hapa kwamba imefikia mahali na napenda Mheshimiwa Waziri ambaye ni Naibu Katibu Mkuu wa CCM akiri kwamba Mabalozi wameruhusiwa kushiriki katika uandaaji wa daftari la wapiga kura, kitu ambacho tunadhani ni kinyume cha taratibu za Serikali yetu. Kwa hiyo, tunapenda kutahadharisha kwamba haya maneno ya vurugu yasije kuwa yanaangalia upande mmoja tu na tuwe waangalifu kwa sababu fujo ni jambo linaloweza kutokea wakati wowote kama watu wanaamini wameonewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda tena niwakumbushe TAMISEMI kuwa maswali mengi yaliyoulizwa katika hotuba ya mwaka jana ya Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara hii hayajajibiwa na kwa hiyo tungeomba yatiwe katika majumuisho ya mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa na mimi ya kuchangia kwa mara ya kwanza kwenye kipindi hiki cha Bajeti na kuwa mchangiaji wa kwanza wa hotuba ya Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Naomba nami niwape pole wafiwa wote na majeruhi wote hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe pongezi kwa Waziri, Mheshimiwa Hassan Ngwilizi, kwa kusoma hotuba nzuri na kuahidi kusaidia kuboresha miundombinu ya Wilaya changa kama ya Kongwa, Misungwi na Wilaya kama hizo ambazo bado hazina majengo mengi yanayozipa sura ya Wilaya. Nampongeza Naibu Waziri, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda kwa kutembelea Kongwa, lakini naomba nimkumbushe tu ahadi yake ya kurudi huko kuona juhudi zetu za ujenzi wa hospitali ya Wilaya na zahanati zetu. Nawapongeza Katibu Mkuu na watumishi wengine wote nchi nzima kwa kazi nzuri sana ambayo imekuwa ikifanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wapo baadhi ya watu ambao wamekuwa wakibeza katika kipindi hiki cha Bajeti utekelezaji wa Serikali katika mwaka uliopita wa 2003/2004, lakini mimi niseme kwamba Serikali hii kwa kweli imefanya mambo mengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikisema machache tu ya Wilayani kwangu, tumekuwa na mradi wa maji mkubwa kabisa ambao hatujawahi kupata toka uhuru wa shilingi milioni 700 wa Benki ya Dunia ambao unatekelezwa Wilayani Kongwa hivi sasa. Majosho yanajengwa, mabwawa ya maji yanachimbwa, tuna soko la Kimataifa linajengwa pale Kibaigwa, soko la Kimataifa katika Wilaya ya Kongwa.

Katika kipindi hiki cha miaka minne zimejengwa shule mpya 32, tulikuwa na shule 65, sasa hivi tuna shule 97. Tulikuwa na zahanati 12, sasa hivi tumeongeza zahanati 13 kwa miaka minne, jumla zahanati 25. Jengo la Halmashauri ya Wilaya linajengwa sasa hivi lipo kwenye *linter,* Mahakama ya Wilaya ipo inajengwa hivi sasa. Basi yako mengi, mengi kabisa ambayo Serikali hii inafanya na kwa kweli hatuna sababu ya kubeza bali kupongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwezi Februari, 2004, Mheshimiwa Rais alikuja hapa kwa Watanzania wale ambao hawakusikia niurudie kidogo alisema kulikuwa na walevi wawili wanatembea, wanabishana hili ni jua au huu ni mwezi. Wakakutana na mlevi mwenzao wa tatu, wakaona ili kupata ufumbuzi awasaidie, wakasema bwana wewe tusaidie hili ni jua au ni mwezi. Yule bwana akasema kwamba mimi ni mgeni nchi hii. Sasa haya yanayofanyika na Serikali hii kwa kweli wote tunayaona, asiyeyaona ni mgeni katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kupongeza sana kinachoendelea na tunachofanya sisi kama Wabunge sasa hivi ni kuimarisha hapa na pale ili kazi hii iwe bora zaidi na katika *spirit* hiyo ya kuimarisha sasa naanza kuchangia katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na la kwanza ambalo nimpe hongera sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa tamko la jana kuhusiana na matatizo ya walimu. Tunampongeza sana kwa hatua zote ambazo ameahidi ili kumaliza tatizo hili la Walimu. Wilaya ya Kongwa peke yake walimu wanadai zaidi ya shilingi milioni 86 za matatizo yao mbalimbali ila TAMISEMI ambao ndio wanaohusika sana, maana yake ndio wenye kasma ya kuhusu mapato ya walimu, ukiangalia pale kwenye hotuba hii ukurasa wa 39, fungu 53, Mheshimiwa Waziri anasema yafuatayo na naomba kunukuu: “Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa na mafanikio niliyoyaelezea mpango huu umekuwa na matatizo yafuatayo:-

(a) Watoto wengi waliandikishwa, hivyo kuongeza msongamano darasani.

(b) Baadhi ya walimu kutotaka kwenda kufundisha sehemu nyingine za nchi.

(c) Watoto wenye umri wa miaka 11 au 13 chini ya Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa (MEMKWA), bado kuanza masomo kutokana na mpango huu kutokamilika.

(d) Baadhi ya maeneo wananchi kukataa kushiriki kazi za ujenzi kwa kisingizio kuwa Serikali imetoa fedha za kutosha na kuwa michango imefutwa.

(e) Ukosefu wa nyumba za walimu na hasa maeneo ya Vijijini kutokana na kutofikiwa kwa malengo ya ujenzi.

(f) Upungufu wa wataalam wa kusimamia shughuli za ujenzi." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo matatizo yaliyoonekana na Wizara. Kwa hiyo, utaona kwamba hili suala la walimu na malipo yao bado Wizara walikuwa hawajaliona kama ni moja ya matatizo makubwa sana ambayo kwa namna moja au nyingine ni upungufu mkubwa sana katika kufanikisha suala la MMEM.

Kwa hiyo, tunaomba sasa tatizo hili likubaliwe na Wizara kuingizwa kama tatizo namba moja ili litatuliwe na liishe kama alivyoahidi Mheshimiwa Waziri Mkuu na mimi naamini kabisa Mheshimiwa Hassan Ngwilizi suala hili atalivalia njuga ili liweze kupata ufumbuzi. Lakini si hilo tu peke yake katika madai ya watumishi wapo Watendaji wa Vijiji, Kata na watumishi wengine wa Halmashauri ambao wana madai yao mengi sana na wenyewe wana mabilioni wanadai. Hebu yahakikiwe, yaainishwe na yenyewe tuyajue ili kadri tunavyokwenda na bajeti inavyoruhusu tuwe tukipunguza baadhi ya madeni hayo.

Mheshimiwa Spika, vile vile katika *point* hiyo hiyo nikumbushie ahadi ambayo uliitoa ya ajira ya Watendaji wa Vijijini na Kata. Ulitoa tamko katika kikao fulani cha Bunge hapa imeishapita kitambo, sasa tuna watendaji 9,000 wanahitajika 5,000 zaidi lakini mpaka sasa tumeajiri 3,000. Ni *phase* ndogo sana ya utekelezaji wa jambo hili na hao watu ni muhimu sana katika maendeleo ya vijiji tungeliomba masuala hayo yawekwe *fast track.*

Mheshimiwa Spika, kuhusu mpango unaokuja utakaosomwa na Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni wa ujenzi wa shule za sekondari katika nchi nzima, tunajua mtekelezaji mkuu atakuwa Wizara ya TAMISEMI kwa sababu ndiyo yuko na watu kule vijijini. Ushauri tu wa haraka haraka tusije tukaangalia idadi ya Kata tulizonazo hivi sasa peke yake inatudanganya sana. Kwa sababu Wilaya ya Kongwa ina watu 250,000 nina Kata 14 tu nina baadhi ya Kata zina wakazi 35,000, baadhi ya Kata zina wakazi 27,000 ukiunganisha Kata mbili unapata wakazi 50,0000 au 40,000 na kadhalika. Wakati tuna Wilaya fulani fulani kwa mfano Pangani ina wakazi 43, 000 ni Kata zangu mbili, Mafia watu 40,000, Lindi Vijijini 41,000 Bukoba Mjini kwa Mheshimiwa Wilfred Lwakatare watu 40,000 wakati ni Kata mbili za kwangu.

Sasa ukisema utagawa shule za sekondari Kikata kama Kata ndiyo kigezo, kata iwe kigezo sawa, idadi ya watu katika eneo lile kama Kata ina watu 30,000 basi ipewe mgao wa idadi ya shule unaofanana na idadi ya watu wa mahali pale na umbali wa kutoka shule moja hadi nyingine kwa maana ya *catchment area,* hayo yote yakitazamwa vizuri tutapata uwiano mzuri kama ilivyokuwa kwa MMEM. Kwa sababu MMEM umekuwa ni mradi wa mfano wa uwiano wa ugawaji wa huduma katika nchi nzima mtu hawezi kusema kwamba kuna upendeleo hapo kwenye MMEM. Kwa hiyo, ningeomba kwenye mradi huu wa Elimu ya Sekondari nao uende katika *spirit* ile ile ya MMEM.

Mheshimiwa Spika, nije katika suala la ugawaji wa Vijiji na Kata kama nilivyoeleza. Wilaya ya Kongwa ina watu 250,000 ,Wilaya ya Mpwapwa inatuzidi kwa

watu 3,000 almost 250,000 lakini vijiji ukivitazama huku ni vingi sana au Kata huku ni nyingi zaidi na huku ni chache. Sasa kwa sababu tuna uchaguzi mwezi Novemba, mwaka huu wa Serikali za Mitaa ningeomba sana Wizara hii ingeliangalia kwa sababu mnatunyima fursa ya wananchi wetu kupata maendeleo. Mtendaji wa Kata mmoja ana vijiji 8 au vijiji 10 atawahudumia vipi haiwezekani.

Kwa hiyo, tuangalie maeneo yale ambao tumebanwa sana tunapoleta maombi yetu myasikilize na myafanyie kazi ili vijiji hivi na Kata hizi ziweze kutamkwa rasmi hiyo mwezi Agosti ili mwezi Novemba, zifanyiwe uchaguzi kama ambavyo tunatarajia. Kwa hiyo, zoezi hilo la uhakiki liangalie Wilaya kama hii ya Kongwa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu Bajeti za Halmashauri ambazo zimekuwa zikivurugika kwa sababu tunatengeneza Bajeti za Halmashauri kwanza halafu tunakuja kwenye Bajeti ya Serikali Kuu, ikija kwenye Bajeti ya Serikali Kuu inafuta baadhi ya kodi kwenye mambo ambayo tumekwishapita kwenye Halmashauri. Ni jambo ambalo ni nzuri kwa sababu Hazina inasema itafidia lile pengo. Lakini kwa mfano, mwaka 2003 sisi Kongwa tumefidiwa kwa *quarterly* shilingi milioni 15, sasa wanapofidia milioni 15 kwa miezi minne hizi milioni 15 Halmashauri izifanyie nini?

Kwa hiyo, vikao vinakuwa havifanyiki, malipo ya watumishi yanakuwa hakuna na uendeshaji unakuwa ni mgumu sana. Kama nilivyosema tuchukue *population* kama ndiyo *index* yetu badala ya vigezo vingine vingine tulifanya sensa ya nini tuangalie idadi ya watu. Ukipeleka milioni 15 kwa wakati wakazi 250,000 kwa miezi 4 japo wanasema wanajazia tu lakini kwa kweli Halmashauri inakuwa haiwezi kujiendesha.

Mheshimiwa Spika, lakini pia niiombe sana Wizara waangalie sana suala hili la kuwatoa Madiwani katika Kamati za Bodi za *Tender,* mimi sina uhakika ufanisi wake. Kulikuwa na kundi kubwa la watu linalotoa *tender* sasa umepunguza kundi lingine umebakiza wachache ndiyo wanatoa *tender* na unasema hii ina mafanikio watendaji pekee yao.

Mimi nilifikiri utaongeza idadi kama kuna wasiwasi wa rushwa unaongeza wigo. Mimi nilifikiri utaongeza idadi kama kuna wasiwasi wa rushwa unaongeza wigo. Sasa wewe unapunguza wigo kwa kuweka watu wachache. *Actually* upungufu mkubwa wa *Procurement Act* ni kupeleka madaraka makubwa sana ya ku-*procure* kwenye Wizara na kwenye nini kwa kikundi kidogo sana cha watu tusipoangalia tunawapelekea watu wachache sana rushwa nyingi kweli tupanue wigo badala ya kupunguza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwenye eneo la afya. Kwenye eneo la Afya Vijijini ni muhimu sana kama ilivyokuwa kwa elimu. Wananchi wamekuwa wakijenga zahanati kama nilivyosema, tumejenga zahanati nyingi kila ilivyowezekana kwa nia ya kuongeza ubora wa huduma vijijini kulingana na umbali na wingi wa watu. Lakini watumishi wa Idara ya Afya ni wachache kweli. Tunazo zahanati kadhaa zina miaka 2 au 3 hata milango haijawahi kufunguliwa kwa sababu hakuna watumishi kila tukiomba kibali cha kuajiri watumishi 30 au 50, tunapata kibali cha kuajiri watumishi wawili ndiyo wanaruhusiwa kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba sana kama tunavyoangalia kwenye elimu na kwenye maeneo mengine tuangalie kwenye afya pia. Watumishi wa Afya waajiriwe kwa sababu matatizo ni makubwa sana vijijini ili tuweze kufikia malengo yale ya dunia, yale malengo saba *Millennium Development Goals* kati ya saba, tatu ni za Afya, moja ya UKIMWI, Malaria na Kifua Kikuu, nyingine kupunguza vifo vya akinamama wajawazito, nyingine kupunguza vifo vya watoto *under five years, out of seven, three* ni za Afya. Kwa hiyo, tuangalie katika eneo hili maana ziko nane ile ya nane ni ya uendeshaji tu, zile za utekelezaji ni saba. Kati ya saba, tatu ni za Afya kwa hiyo, tuangalie kwa makini katika eneo hili la Afya. Pale zilipojengwa Zahanati *new Kits* zipelekwe kule.

Madaktari na manesi waajiriwe na vifaa vya chanjo kwa mfano, friji ya kuwekea zile dawa kwa ajili ya chanjo zipatikane. Baadhi ya watu kule Wizara ya Afya wanasema ni Zahanati za kisiasa hizi si za kisiasa wananchi wanazihitaji kabisa kwa hiyo ziwekewe huduma zinazohitajika ili tutekeleze Ilani yetu kama ilivyoahidi kupeleke Afya kwa wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeomba suala la uanzishwaji wa Bodi za Huduma za Afya na Bodi nyingine za Huduma, Bodi za Maji, Bodi za Afya katika Wilaya zetu lipewe kipaumbele cha aina yake. Tumekuwa tukifanya katika Wilaya zile taratibu zote zinazohusika, lakini kuna hatua nyingi sana za kufuata. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Gazeti la Serikali na nini upo utaratibu mrefu sana unafanya bodi hizi haziundwi na kama huundi Bodi ya Afya utatekelezaje yale malengo mazuri ya Afya, kama huundi Bodi ya Maji utaboreshaje masuala ya maji, kuunda tu Bodi inatuchukua mwaka moja au miaka miwili hebu tufupishe. Kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye suala la walimu tufupishe hii kamba tufanye fupi zaidi. Wizara ya TAMISEMI wawe na mamlaka makubwa zaidi ya kuweza kufanikisha mambo haya ili yaweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, niwaombe Wizara ya Kilimo na Chakula katika ule Mfuko wa Pembejeo, mikopo imetolewa katika nchi nzima kama nilivyosema siku moja kwenye semina hapa. Wilaya ya Kongwa ni moja yenye matrekta mengi katika nchi hii, hatuna maana ya nyingi kwamba zinatuzidi uwezo hapana, tuna maana ukitulinganisha linganisha trekta zetu sisi ni mbovu mbovu tu. Lakini wakati wa kilimo tunaweza kuziweka kwenye mashamba angalau zikatusaidia.

Mheshimiwa Spika, mimi nina kijiji kimoja kina trekta zetu hizo mbovu mbovu 50. Tuliambiwa hapa mwaka 2002 Mkoa wa Lindi una trekta 26 wakati mimi nina vijiji vina trekta zaidi ya hizo. Lakini katika mkopo ule Wilaya ya Kongwa hata mkulima mmoja hakupata mkopo. Kwa nini hawakupata mikopo kwa sababu ya masharti magumu magumu, hatimiliki za shamba hivi nani katika Wilaya ya Kongwa ana hatimiliki ya shamba, hatimiliki ya nyumba, zile nyumba za Kongwa nani ana hatimiliki kule?

Mheshimiwa Spika, tuna nyumba za tembe na nini, lakini siku hizi tunaziboresha, tunaziezeka kwa mabati. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali kama kweli tuna nia hiyo ya kuwafikishia mikopo, ni kweli matrekta yamepaki nje lakini

ningeomba masharti yale yaangaliwe na Halmashauri za Wilaya ndizo zipewe jukumu nzima la kuamua nani akopeshwe na kwa kiasi gani na zimfikieje, azirejeshe vipi badala ya kuyapa mabenki kama *EXIM* jukumu hilo la kutoa mikopa hiyo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Nianze moja kwa moja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI na Naibu Waziri naye kabisa bila nongwa anafanya kazi vizuri.

Mimi nimeshaingia zaidi ya mara sabini ofisi kwake juu ya vijiji ingawa sijapata, lakini kila nikienda nikirudi ninaridhika na majibu na maelekezo ingawa sijapata. Kwa kweli anafanya kazi vizuri na kama ningekuwa natoa cheo sasa hivi angepanda cheo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya TAMISEMI imetatua tatizo langu mimi la malalamiko yangu kwamba Mtwara mnafanya dampo na sehemu ya adhabu kuwaleta watumishi wenye matatizo mmemaliza matatizo siku hizi mambo yamekaa vizuri. *RC, DC* na *DED* mlionipa kwa kweli wanafanya kazi vizuri na mmewahamisha katika uhamisho wa kawaida siyo dampo la adhabu. Maana ikiwa dampo nitawambieni, wakifanya vizuri nitasema vilevile kama kawaida yangu.

Mimi wanavyonifurahisha ni jinsi wanavyoshirikiana na kusisitiza ujenzi wa shule za sekondari, miradi ya maendeleo wanavyoshirikiana *DC,* Mkurugenzi na *RC* wake ahaa hapo ndiyo wananimaliza kabisa. Lakini wakianza mambo yao nitasema, maana mna kawaida tukisifu mnapiga makofi, lakini tukisema matatizo yao mnasema fitina, basi na mimi nitakuwa fitina wakianza taabu. Lakini kwa sasa hivi wanafanya kazi nzuri sana na endeleeni kutupa watumishi wa aina hiyo sisemi wale waliopita wabaya hapana, labda sikuwepo niliokuwa nao hawa ndiyo ninaosema jinsi wanavyofanya kazi vizuri. *(Makofi/Kicheko)*

*(Hapa umeme ulikatika na kurudi baada ya muda mfupi)*

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Wamezoea kuniona gizani ndiyo maana wamekata umeme. Lakini nataka kuwaelezeni siku hizi Mtwara umeme upo, unapatikana kidogo, kwa hiyo, masuala ya umeme yamepungua.

Mheshimiwa Spika, kama kawaida yangu ninapokaribia kuja kwenye kikao cha Bajeti huwa ninapita kuwaaga wapiga kura wangu. Wananipa utumwa, utumwa walionipa kwenye Wizara ya TAMISEMI ni kwamba maamuzi katika Wizara ya TAMISEMI yanachelewa mno. Tumeleta maombi ya Serikali za vijiji mwaka 2001 tumepata namba ya vijiji vitatu, Kiweguro, Mnivatta na Ninyumba mpaka leo hatujapata hati. Tumeleta maombi 27 ya vijiji mwaka 2003 mpaka leo hatujapata hati masuala haya siyo ya kisiasa ni ya kiuchumi pia.

Kwa mfano, vijiji vilivyoko mpakani ambavyo vina vitongoji kulingana na ugomvi wa kijiji na kitongoji basi kitongoji kinakwenda kuuza korosho Tandahimba, kwa sababu wakiuza kwenye kijiji kuna ugomvi katika ugawaji wa ushuru wa kijiji hatimaye wanachukua korosho kwa hasira wanakwenda kuuza katika Wilaya nyingine. Kwa hiyo, tunapungukiwa na mapato katika Halmashauri kwa ajili ya tatizo hili la ugomvi wa kijiji mama na kitongoji, hasa vitongoji vikubwa.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana tunasema mandhari kime-*qualify* kupata kijiji kitongoji hiki kipewe Serikali ya kijiji, lakini fedha tulizopewa ni kidogo, kwa nini mnashindwa kufanya ukarabati Katibu Mkuu vipi? Mhasibu wa kijiji changu kimoja alipewa fedha za kujenga madarasa matatu na MMEM kafanya ukarabati na kajenga madarasa manne na Mheshimiwa Waziri Mkuu kasifia jana hapa. Wewe umepewa fedha za kuajiri Makatibu wa Vijiji kadhaa, kinachokushinda ni nini kufanya kama mwanakijiji huyo kufanya ukarabati vikaongezeka vijiji vitatu au vinne tatizo ni nini? Nikuletee Mhasibu yule wa kijiji msaidiane naye aliyofanya yeye kule badala ya kujenga madarasa matatu kajenga madarasa manne na Mheshimiwa Waziri Mkuu kasifia. Kwa nini wewe sasa usifanye ukarabati wa vijiji kumi basi ukaongeza na viwili kidogo pamoja na hivi ninavyoomba mimi?

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba Wizara ya TAMISEMI itoe tamko juu ya kero hii, mimi sina raha Jimboni kule kwa ajili ya hili. Lakini kero nyingine ni Mji mdogo wa Nanyamba kuna mgogoro mkubwa sana makabrasha yote ya Mji mdogo wa Nanyamba na vijiji nimempa Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa hiyo ningependa Wizara itoe tamko hapa juu ya mgogoro huu hatuna raha viongozi wa kule katika hili.

Mheshimiwa Spika, kero nyingine ni *tender* kama walivyosema wenzangu, hivi mnasema Madiwani ndiyo wenye Halmashauri, kama mtu mwenye duka na duka lake kamchukua binamu yake kumuuzia duka, hivi yule muuza duka yule afanye manunuzi na mauzo mwenye duka asijue inawezekana kweli! Halmashauri ya Madiwani watendaji ni kama muuzaji tu sasa afanye mambo yule yanayohusu fedha Madiwani wasielewe, wewe uliyeweka taratibu hizo mwenyewe unaelewa! Sisi hatuelewi labda tukuulize wewe uliyeweka taratibu hizo wewe mwenyewe unaelewa kwamba mwenye mali asijui habari fulani fulani ili ajue mtumishi wake tu maana yake nini? Tunaomba suala hili mliangalie tena.

Mheshimiwa Spika, suala lingine kumepunguzwa sana vyanzo vya mapato vya Halmashauri. Uendeshaji wa Halmashauri unategemea sana sasa fedha kutoka Serikali Kuu kwa maana ya ruzuku. Ombi langu tafadhali msicheleweshe basi ruzuku hizo, mkizichelewesha shughuli zote za Halmashauri zimesimama kungoja fedha kutoka Serikali Kuu. Tunaomba fedha hizo zisichelewe ili shughuli ziendelee kama kawaida.

Mheshimiwa Spika, kuna ujenzi wa barabara kwa maelezo ni kwamba fedha hizi zinapotoka hazitoki na fedha za mifereji kwa maana hiyo barabara inatengenezwa tu hakuna ile mifereji ya kukusanya maji na kutoa maji barabarani kumwaga porini. Kwa maana hiyo maji yanatembea mle mle kwenye barabara ndiyo kusema kila mwaka

barabara hiyo inabidi itengenezwe tena kwa sababu ikinyesha mvua inaharibika kwa sababu ya maji.

Sasa hili kama ni kweli basi nilikuwa naomba lirekebishwe na pia ujenzi wenyewe wa hizi barabara kheri tujenge kilometa 10 zitakazokaa kwa muda wa miaka miwili, mitatu, mpaka kumi au kumi na tano kuliko kujenga barabara kilometa 70 kwa mwaka mmoja tu zimeharibika na mwaka mwingine tuzitengeneze tena. Mimi sielewi katika hili. Kwa nini tusitengeneze kilometa chache lakini imara kuliko kilometa nyingi ambazo mwakani tena hazipitiki inabidi tuzitengeneze tena.

Mheshimiwa Spika, suala la uhaba wa watumishi nayo ni kero katika Jimbo langu. Katika Zahanati utakuta kuna mtumishi mmoja tu aende kuandika dawa, afunge mlango, aende akafunge vidonda, afunge mlango aende akagawe dawa, afunge mlango aende akachome mgonjwa sindano, kwa kweli ufanisi unakuwa mdogo sana.

Tulikuwa tunaomba watumishi wa Idara ya Afya kwenye zahanati wapelekwe kule kulingana na Ikama. Watumishi pia wa Idara ya Maendeleo ya Jamii kila Kata tunaomba kuwe na mtumishi wa Idara ya Maendeleo ya Jamii kwa sababu mtumishi wa Idara ya Maendeleo ya Jamii ni *researcher* anayefanya utafiti wa kwa nini kila kitu kipo pale kijijini lakini watu hawataki kufanya shughuli hizo. Njaa ipo, ardhi nzuri ipo, pembejeo zipo lakini watu hawataki kulima kwa nini? Hiyo ni kazi ya Idara ya Maendeleo ya Jamii na hutoa sababu na mikakati ya kufanya ili mambo yaweze kwenda vizuri pale. Sasa inabidi kila Kata awepo mtumishi wa Idara ya Maendeleo ya Jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia Maafisa Kilimo hawatoshi, ukienda kijijini wanakueleza sisi tuna miaka mitatu hatujapata ushauri wa kitaalamu juu ya kilimo kwa sababu Afisa Elimu wa Kata hatujamwona. Lakini walimu pia ni kero lingine kuna upungufu mkubwa wa walimu kukabiliana na hili wimbi la Mpango huu mzuri wa MMEM. Tumekarabati na kujenga madarasa vizuri, tumeondoa ada za shule za msingi pamoja na michango mbalimbali na watoto wanaandikishwa shuleni kwa wingi sasa wame-*create* tatizo la kukosa walimu wapo wachache. Nilikuwa naomba Wizara ya TAMISEMI waangalie suala hili vyema.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa shule za sekondari unaotarajiwa kuanzia kwa kipindi hiki cha bajeti ni kwamba kwa miaka mingi iliyopita Mtwara ilikuwa si rahisi kupeleka miradi ya maendeleo kwa sababu kulikuwa na vurugu ya vita ile ya Msumbiji hilo linaeleweka kila mahali palipo na vita.

Sasa vita hakuna kule kuna amani, nilikuwa naomba masuala haya ya maendeleo angalau kuwe na upendeleo maalumu kwa sababu kwa muda mrefu Mtwara kuliachwa na hasa ujenzi wa shule za sekondari zijengwe kwa wingi kule ili kutupunguzia idadi ya Wamachinga. Vijana wanaomaliza elimu ya msingi hawana nafasi ya kwenda kwenye shule za sekondari wanakuja kulundikana Dar es Salaam kama Wamachinga. Mkitusaidia kujenga shule za sekondari vijana wengi watakwenda kwenye shule za sekondari, vijana

wengi watakwenda Vyuoni na vijana wengi watakuwa maofisini watapungua kuja Dar es Salaam kwa jina la Wamachinga.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ofisi ya Mbunge nimeona hapa niko kwenye ofisi ya Mkuu wa Wilaya, ni kweli, lakini ni uwanja tu sasa sijui watanipa majamvi ili nikatandike au ndiyo mtanipa meza sasa hivi. Lakini ofisi hii ni ya muda au ni ya kudumu kwa sababu tulielezwa hapa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba katika kila Jimbo tutajengewa ofisi Jimboni. Mimi ofisi hii iko Mtwara Mjini sasa ni ya muda au ni ya kudumu na kama ni ya kudumu ile kauli ya kwamba atajengewa ofisi Mbunge Jimboni, kwangu mimi ikoje? Naomba kupata maelezo kidogo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu Makatibu tarafa wa Tarafa yangu mimi kama nilivyowaambieni kuna simba wengi, mmewapa pikipiki, lakini hawana raha. Nilikuwa naomba wapewe *Suzuki* maana sehemu yenye simba ukitembea na pikipiki ni hatari. Ni bora muwape *Suzuki* kwa sababu ya hali ya huko ya simba kila siku mnasikia simba amekamata watu huko Mtwara na Makatibu Tarafa hawa ni watu vilevile kwa hiyo pikipiki ni hatari kwa Katibu Tarafa nilikuwa naomba wapewe *Suzuki.*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa ni kuhusu Madiwani. Madiwani ningeomba kuwe na utaratibu wa kuwakopesha vyombo vya usafiri na wao kwa sababu wana wajibu wa kutembelea na kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye kila kijiji kwenye Kata zao. Sasa bila usafiri hali hii itawapa taabu kidogo.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie hapo, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Namwomba Mheshimiwa Waziri mapendekezo haya na ushauri huu na maombi haya hasa ya Serikali za vijiji na Mji mdogo wa Nanyamba tafadhali. *(Makofi)*

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika hoja iliyo mbele yetu ya Mheshimiwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, nami niwape pole wafiwa wote, Waheshimiwa Wabunge waliopata ajali na Mheshimiwa Mbunge aliyevamiwa na majambazi nawapa pole sana.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Danhi Makanga kwa kurudisha Jimbo lake. Nimwombe rafiki yake Mheshimiwa Isaac Cheyo, afuate uamuzi mzuri huo, CCM milango bado iko wazi ili naye mwakani tuwe naye vinginevyo hali si nzuri sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ninawajibika kuzipongeza hotuba nzuri sana za Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Hotuba ya majumuisho ya Mheshimiwa Waziri Mkuu jana imewafurahisha sana Watanzania na hususan walimu. Mimi naipongeza sana ilikuwa nzuri ya aina yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda sasa nijielekeze kwenye hoja ya leo na niende moja kwa moja kwenye Wizara hiyo kwa kusema kwamba mimi nina mashaka juu ya Wizara

ya TAMISEMI inawezekana Wizara hii ni kubwa sana au Mheshimiwa Waziri wa Wizara hiyo amepwaya kwenye Wizara hiyo. Nasema hivyo kwa sababu hakuna maeneo yenye matatizo kama Serikali za Mitaa kwa upande wa Halmashauri za Wilaya na Manispaa yapo matatizo mengi mno. Nianzie tu labda na tatizo la barabara. Barabara ambazo zinahudumiwa na Halmashauri na Serikali za Mitaa ni kilometa 50,000.

Katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri hapa asubuhi amesema mwaka wa fedha unaopita ni kilometa 4,328 tu ndiyo zimefanyiwa matengenezo. Lakini barabara hizi ndiyo zinaenda kwa wananchi wapiga kura, ndiyo zinasafirisha mazao ya chakula na ya biashara, ndiyo zinapeleka kule pembejeo na ndiyo hasa uhai wa nchi. Sasa zina matatizo hayo na sidhani kama Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake alivyoisema hapa nimeona ameisema kwa uepesi sana si kufanana na matatizo ya barabara zilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba hapa kuna fedha ambayo imetengwa kwa ajili ya barabara hizo, nataka kujua mimi hizo fedha ambazo amezisemea hapa kwamba kilometa 3,940 zimefanyiwa matengenezo ziko wapi? Kwa sababu sisi katika maeneo ya kwetu hazipo mimi kwenye Wilaya yangu barabara ni mbovu hizo fedha zimetengeneza barabara wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna hoja hapa huwa saa nyingine tunafanya kulalamika kwamba Serikali ina *tendency* ya kutelekeza baadhi ya maeneo ya nchi na kuangalia tu baadhi ya maeneo ya nchi. Ndiyo maana Mheshimiwa Waziri wa Fedha wakati akifanya majumuisho alijibu hoja ya Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, ambaye alikuwa amesema kwamba kuna baadhi ya maeneo muhimu katika Serikali yanapewa watendaji kutoka eneo fulani tu la Mkoa mmoja. Lakini Waziri wa Fedha alipojibu akasema kwamba yeye siyo mkabila na watu kutoka Mkoa unaodaiwa kwamba una watumishi kwenye *TRA* ni asilimia 15. Sasa asilimia 15 kwa Mkoa mmoja wakati una Mikoa 21 halafu asilimia 15 Mkoa mmoja na Mikoa 20 asilimia 85!

Mheshimiwa Spika, lakini sasa hoja hapa siyo ukabila, hoja hapa tunasema ni fursa sawa kwa wote. Tunasema hivi kwa sababu malalamiko yapo makubwa zaidi. Kuna watu wanahoji kwamba inawezekanaje Mkoa mmoja unakuwa na Wakuu wa Mikoa watatu au zaidi, Mawaziri *(Full Cabinet Ministers* watatu au zaidi na Mkoa mwingine hakuna hata Mkuu wa Mkoa mmoja wala Waziri mmoja inawezekana?

Mheshimiwa Spika, tunachosema ni fursa sawa kwa wote. Haiwezekani maeneo mengine yakawa ya wapiga kura na maeneo mengine yakawa ya wapigiwa kura. Kwa sababu athari zake ni kwamba mnapokuwa na watendaji fulani tu kwenye maeneo fulani fulani wanapoingia kwenye jiko sasa lazima watapakua na kupelekwa kwao. Ndiyo maana tunasema kwamba baadhi ya maeneo yetu pengine hayapati Mipango ya Maendeleo na hayapati Miradi ya Maendeleo kwa visingizio mbalimbali ikiwemo tunaambiwa ninyi siyo maskini, tunaambiwa ahaa wafadhili hawakuamua kwenda huko au tunajaribu kwanza katika Wilaya 45 za awamu ya kwanza, pilot arrears visingizio vinakuwa vya namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanatupa taabu hata Wabunge wa maeneo hayo mara nyingi wanakaa miaka mitano halafu kipindi cha pili hamuwaoni hapa Bungeni ni kwa sababu barabara wanazozikuta mbovu wanaziacha mbovu kwa sababu Serikali haipeleki huko fedha.

Mimi nina mifano, nimejaribu kuangalia hapa mifano kwenye maeneo ya Kanda ya Ziwa, Mkoa wa Mwanza tuna Majimbo 13 mwaka 2000 Wabunge waliorudia ni watano na waliopoteza Majimbo ni Wabunge wanane, Mkoa wa Mara una Majimbo saba, Wabunge waliorudi ni wawili na waliopoteza Ubunge ni watano, Mkoa wa Tabora una Majimbo tisa, Wabunge waliorudi ni wanne na waliopoteza Ubunge ni watano, Mkoa wa Kagera una Majimbo kumi, Wabunge waliorudi ni wanne na waliopoteza Ubunge ni sita.

Kwa hiyo, sasa Waheshimiwa Wabunge niwaambie kabisa ndiyo *trend* ya mambo mwaka kesho. Zaidi ya asilimia 50 ya Waheshimiwa Wabunge kutoka Kanda ya Ziwa, Nyanda za Juu Kusini na kwingineko kwenye matatizo kama hayo hawarudi Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunasema kwa uchungu mtuelewe, mtuletee fedha za maendeleo, wapiga kura hawatuelewi. Mimi nina barabara mbili za Halmashauri ambazo tangu niwe Mbunge ziko chini ya Halmashauri. Kila nikiomba fedha zinawekwa kwenye programu. Lakini mpaka leo bado mwaka mmoja tunamaliza iko barabara ya Kasamwa - Nyang’wale - Ibambila -Mwingilo hadi Nyamikonze. Halafu iko barabara ya kutoka Buharahara kwenda Shabaka - Ibambila - Nyang’wale. Barabara hizi nimezikuta hivyo na sasa naondoka ziko hivyo hivyo. Halmashauri inapanga fedha lakini fedha inakuwa haipo. Sasa imebakia tunatupiana mpira Diwani na Wabunge.

Mimi ninapokuwa sipo Madiwani wakifanya mkutano wakibanwa wanasema hii barabara ya Mbunge na mimi nikirudi nasema aah, hii barabara ni ya Diwani, ni ya Halmashauri. Sasa tuna hali hiyo. Tunaomba sana Serikali ilete fedha zitengeneze miundombinu zilete maendeleo ya jamii katika maeneo haya ambayo tunalalamikia wengine hamna matatizo hayo vijijini na ndiyo maana mnakaa Bungeni vipindi vitano, sita kwa sababu tu mko jikoni. *(Makofi)*

Sasa tusifanye utawala wa wakati wa wana Israel kwenye Biblia. Wakati wana Israel wanatoka kule Misri walikuwa makabila 12 . Lakini katika makabila 12 kuna kabila moja tu ndio lilikuwa limeteuliwa na Mungu lifanye kazi za ibada, kutoa sadaka likae kwenye hema takatifu .

Sasa wale 11 ndio walikuwa wanapigana, wanahangaika huko kupigana na makabila mengine maadui, kufanya kazi za mikono, kupeleka chakula kwa hawa Walawi. Musa alikuwa Mlawi na Haroun alikuwa Mlawi. Sasa tusifanye picha hapo nchi hii kwamba kuna maeneo au mikoa ya Walawi na mikoa ya Mataifa. Ni lazima tuangalie sasa tunataka fursa sawa kwa wote. Naomba sana Serikali hapo ielewe na kama imefanya makosa huko nyuma irekebishe haraka sana. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Umeshawaona, waambie.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, nikielekea sasa kwenye matatizo ya Walimu. Jana Mheshimiwa Waziri Mkuu hotuba yake ilikuwa ni nzuri sana. Nimesema ilikuwa ni ya kuvutia na ni ya Kiserikali hasa na wengi tumeipenda na tumempongeza. Kidogo nimeshtuka Mheshimiwa Waziri wa Serikali za Mitaa hajayapa uzito matatizo ya madai ya Walimu. Nilidhani kwamba yeye ndiyo angekuwa msitari wa mbele kuwasemea Walimu wake. Walimu wana matatizo makubwa na ndio wapo wengi sana nchini. Na ndio huwa wanasimamia hata uchaguzi. Lakini wana matatizo sana.

Mheshimiwa Spika, madai yao hapa Waziri Mkuu tunashukuru ameshatoa maagizo, ameshasema ziundwe Tume. Wakuu wa Mikoa waunde Tume walete ripoti mwisho wa mwezi Julai na yeye kuna Tume yake. Lakini nilikuwa nasema Tume hizi zinaweza zikapigwa rungu la fedha kwa sababu wanaowafuata wana fedha, wanazo. Kwa hiyo, watanunuliwa na ripoti hizi za Tume zitawasafisha wale itaonekana kulikuwa tu makosa ya mawasiliano au utendaji.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba Waziri Mkuu alisimamie sana hili. Kweli tukija sisi tutauliza hapa na yeye amesema atatupa ripoti. Lakini nilikuwa naomba alisimamie sana na wale Wajumbe wa Kamati wateuliwe ambao hawawezi kuhongeka. Huwa nasikia watu wa Usalama ni wazuri kwa sababu mtu wa Usalama mnaweza mkahongwa naye lakini yeye baadaye anakuripoti. Ukimwuliza anasema tumeiba wote mimi nilikuwa kazini. Sasa kama ni muhimu na yeye awekwe.

Mheshimiwa Spika, lakini nilichokuwa nataka kusema hapa ni kwamba nilikuwa nadhani ingeundwa Tume Huru ya Wabunge kufuatilia tatizo zito ili kusaidia Serikkali iliyokuwa madarakani tumalize kipindi chake kwa usafi. Iundwe Tume ya Wabunge mwezi Novemba tukija hapa kwenye Bunge ripoti ije isomwe ya Bunge ambayo itakuwa huru sidhani kama kuna mtu atahonga Wabunge. Ila hilo naomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Walimu wa Geita wanadai malipo ya likizo shilingi milioni 18, matibabu shilingi milioni 29, ajira mpya shilingi milioni 186, wanaishi kwa shida mno. Mimi nina mifano miwili ya masikitiko sana. Kuna Mwalimu mmoja mgeni alikuja kuripoti akawa anataka kuhama, baadaye nilipokwenda pale mara ya pili nikakuta ameshaoa. Mwalimu wa kike ameolewa na mzee mmoja wa miaka 60 sababu ni kwamba yule mzee ana ng'ombe wa kulima na jembe kwa hiyo, alishamlimia mpunga. Baadaye yule msichana alipovuna alifanikiwa kupata magunia 50. Basi akaomba uhamisho haraka sana akaondoka. Mwingine nimekwenda nikakuta ana shida namna ya kuishi akaniambia nisaidie nihame huku. Mimi nisingeweza kutoa Mwalimu wangu kupeleka sehemu nyingine. Lakini nilipokwenda kule mara ya pili tayari ameshaolewa na Mtendaji wa Kijiji.

Sasa tunasema kwamba hawa wanalazimika kuolewa au kufanya mapenzi kwa kulazimishwa. Kwa tafsiri ya sheria hiyo hawa wanabakwa na anayesababisha abakwe ni Serikali hawakuwa wanapenda. Tena zamani Walimu walikuwa wanakaa miaka 7, 9 kijijini hawajaolewa wala hawajaoa mbona wao wafike mwaka wa kwanza tu aje aoe,

wote mimba, asilimia 50 ya walimu wana mimba, watoto wadogo wadogo. Serikali inasababisha wabakwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema labda tatizo la Walimu haliishi, nadhani ni kwamba ni vizuri sasa waondoke Wizara ya TAMISEMI, warudi Wizara ya Elimu kwa sababu TAMISEMI imeshindwa kutatua matatizo ya Walimu. Watendaji wa Vijiji wameambiwa kwamba wataajiriwa mwezi Julai, 2003 mara Januari, 2004 sasa hivi hawajaariwa na sasa hivi ajira wamesema masharti anasema watakaotimiza masharti baada ya miaka 3, masharti hawa ni kupata Elimu ya Sekondari, kule hakuna Shule za Sekondari na hawa wamefanya kazi vizuri miaka yote. Sasa unawawekea masharti magumu hawa *Form Four* wataipata wapi na wamefanya vizuri miaka yote. Kwa hiyo, Watendaji wa Vijiji tunaomba waendelee kuajiriwa kama walivyo na sio kwa masharti. *(Makofi)*

Mwaka 2002 tuliteua Mabaraza ya Kata, Mheshimiwa Waziri hajalisema. Madiwani wakae pale na wengine walipewa takrima wakati huo Mabaraza ya Kata hayajafanya kazi Waziri mbona hajasema hapa. Tunaulizwa mambo mengi tunashindwa kujibu. Naamini kwamba ni askari wa mwamvuli, lakini askari wa mwamvuli amekwama kwa sababu mtakaporudi kikosini mkiitwa sasa na Kamanda wenu Mheshimiwa John Magufuli, funga mguu sina ganda wala risasi. Wataitwa hivyo, Mheshimiwa Jakaya Kikwete ataitwa, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya ataitwa lakini itafika wakati wa Mheshimiwa Hassan Ngwilizi funga mguu afande ninazo silaha zote ila maji kwenye kibuyu ndiyo sina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali ni mbaya sana lazima tuseme. Sasa wewe askari wa mguu. Mimi nadhani niishie hapo kwa kuwa muda unakaribia kuisha. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya TAMISEMI.

Kwanza kabisa nami niungane na wenzangu kutoa pole kwa ndugu zetu waliofiwa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na dada yetu Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na baba yao. Pia ndugu yetu Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan kwa kufiwa na binti yake, natoa pole sana na Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Pia nitoe pole kwa wale waliopatwa na matatizo ya uvamizi Mama yetu Mheshimiwa Anne Malecela, dada yetu Mheshimiwa Esterina Kilasi na kaka yetu Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa uvamizi mbaya na ni wapongeze viongozi wa Mkoa wa Morogoro jinsi walivyojipanga vizuri na kuweza kuwakamata walioweza kusababisha ajali hizo mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze ndugu yetu Mheshimiwa Danhi Makanga, ambaye kwa kweli uamuzi aliouchukua ni sahihi na nimpongeze Mzee wetu Mheshimiwa Dr. John Malecela ambaye aliamua yeye mwenyewe ainuke na kwenda kukaa kule na

kuweza kumwokoa mwenzetu. Namkaribisha sana ndugu yetu Mheshimiwa Danhi Makanga, karibu sana katika uwanja wa amani. Unaweza ukasahau ukasema CCM ooyee, lakini ni utaratibu tu siku nyingine utafanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa sasa niipongeze hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri, amesoma vizuri, imeandaliwa vizuri chini yake yeye mwenyewe, Naibu wake pamoja na Makatibu wake wanaomsaidia. Kwa kweli hotuba ni nzuri mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefanya kazi nyingi mno. Ukiingia kwenye maji sisi watu wa Misungwi sasa hivi tatizo la maji limeanza kupungua linaelekea kwisha kabisa. Kwa hiyo ,Waziri anayehusika...

*(Hapa umeme ulikatika na kurudi baada ya muda mfupi)*

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Basi wapiga kura wanaweza wakaona wewe kwamba huna shukrani. Ndiyo maana nikasema kwamba ni vyema niyapongeze maeneo ambayo yamefanya kazi nzuri na wakasifiwa.

Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kwa kweli sasa hivi mawasiliano ni kila mahali, tunakushuru sana. Lakini pia Waziri wa Ujenzi mgao wake sijui anatumia *formular* gani? Kama ni mikoa yote itapata, kama ni majimbo kila jimbo litapata kutokana na hali halisi yake katika barabara zake za Mkoa. Kwa hiyok Mheshimiwa John Magufuli pamoja na mwenzako tunawapongeza sana, kazi yenu ni nzuri inastahili pongezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zipo Wizara nyingi ambazo zimefanya kazi vizuri, lakini pia zipo nyingine ambazo zimeboronga. Ni vyema ukawa mkweli kwa sababu sisi ni watu wa kutumwa. Wizara hii ni kati ya Wizara ambazo kwa kweli zinafanya kazi yake wakati mwingine sio sahihi, haziwatendei haki wananchi. Naibu Waziri kwa kweli ni hodari anajitahidi sana kutujibu anaturidhisha.

Mimi mara kwa mara nimeingia ofisini kwake, amenipokea naye limemwuma sana lile suala la Wilaya za kwanza zilizokuwa 9 sasa hivi ni 17. Zile 9 za mwanzo kwa kweli bado zina mapungufu makubwa ambazo ni Misungwi, Ruangwa, Bukombe, Kongwa, Sikonge na zingine.

Sasa mimi sielewi sijui wanagawaje mgao huo. Tuna matatizo la Hospitali ya Wilaya kwenye Wilaya hizi. Unaambiwa kwamba wananchi wachangie, Shule za Sekondari wananchi wachangie, ujenzi wa barabara wananchi wachangie wakati Wilaya zingine zilisaidiwa na Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, Misungwi tumejenga wodi ya akinamama wanateseka kweli. Mpaka sasa hivi labda uende Sumve, Bugando, Kwimba, Ngudu, Misungwi haina Hospitali ya Wilaya nimezungumza mara nyingi sana lakini hakuna msaada huo. Napenda nipate jibu ni vipi, ni lini sasa Hospitali ya Misungwi itakuwa Hospitali ya Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika suala la barabara nimeingia mara nyingi kufuatilia barabara ya kutoka Manawa, Nduha, Kasololo mpaka Ngaya tangu mwaka 1980 haijatengenezwa. *El-Nino* imekuja kupita pale ikaacha makorongo bado yapo. Hivi wananchi wa Igongwa wanapita wapi. Wananchi wa Sumbugu wanapita wapi kwenda kupata huduma muhimu?

Wakuu wangu wa Mikoa bahati nzuri leo wako hapa ambao wamepita katika mkoa wangu. Mheshimiwa Stephen Masishanga, ameacha barabara hiyo iko hivyo hivyo na sidhani kama alipata nafasi ya kupita katika eneo hilo. Mheshimiwa Daniel Ole-Njoolay, yuko hapa kweli hajapata nafasi ya kupita eneo hilo, lakini amezunguka sana katika Wilaya yetu ya Misungwi na tunampongeza sana, kazi zake nzuri, ni mfuatiliaji mzuri na anastahili sana kuendelea kuwa katika Mkoa wetu wa Mwanza. Karibu sana. *(Makofi)*

Barabara hiyo bado ni mbaya mno, Waziri anasemaje? Waziri anatueleza nini kuhusu barabara hiyo? Ukifika Ngaya ni matatizo, Lutalutale wanalia, Mbarika yenyewe usiseme mpaka wanazunguka Nyamainza na ninampongeza Waziri wa Maji kwa kuleta wale Wachina wanaendelea kukarabati barabara ya kutoka Buhingo, Nyamainza na Seke inaendelea kuwa nzuri lakini ya kutoka Manawa kupita Nduha Kasololo ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kama ni waathirika wa barabara basi wako katika maeneo hayo niliyoyataja hao ni waathirika wana matatizo makubwa.

Naiomba Serikali ifikirie hilo, si rahisi hata kupitisha mkokoteni wa ng'ombe mfano labda kuleta mazao kwenye mnada wao Misasi. Wagonjwa ndiyo hivyo. Juzi juzi tu wamemzalisha mama mwingine kwa Mheshimiwa Diwani Gregory wa Sumbugu pale. Haiwezekani, ikabidi Mheshimiwa Diwani avae *gloves* akaingilia mambo bila aibu, baadaye mtoto akazaliwa mzima na mama akabaki salama.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Diwani wangu huyu amefanya hiyo kazi na akamwokoa mama huyo. Mama huyo anatoka kwenye kijiji cha Buhunda, ni tatizo kubwa hakuna njia. Kwa kweli niliona nilizungumzie hilo kwa uchungu kama nilivyotumwa nalifikisha kavukavu hivyo ili angalau muweze kulipokea na kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wamezungumzia masuala ya Walimu. Ndugu yangu Mheshimiwa Job Ndugai amezungumza kwenye shilingi milioni kama 80. Mimi ni balaa ni kati ya Wilaya ambayo ina matatizo kweli. Kuna *reshuffle* ambayo imefanyika ya uhamisho wa walimu zaidi ya 800 mwingine aende hapa mwingine aende hapa hakuna malipo yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, fuatilieni Misungwi ni zaidi ya shilingi milioni 700 wanadai Walimu wangu, ni matatizo makubwa mno, njooni muone. Sasa msimamizi ni wewe labda Mheshimiwa Joseph Mungai teremsha mpaka kijijini basi kama ulivyofanya

kwenye MMEM ambayo kazi imefanyika vizuri zaidi. Hivi kuna nini hapo kwenye Halmashauri?

Mheshimiwa Spika, mbaya zaidi wananchi wanauliza kwamba hivi kwa nini Mheshimiwa Rais hii Wizara aliiweka chini yake *direct,* angeiweka tu kama zingine Wizara ya Ujenzi, zote ziko chini yake lakini hii ikawa *direct* kwake. *I say* kwa kweli inajaribu kumpakapaka vijimatope kidogo Mheshimiwa Rais. Kitu ambacho kwa kweli kama ni askari wa miamvuli aidha, wamening'inia mguu mmoja uko vingine sielewi ni namna gani kwa kweli hii Wizara inatupa shida. Fuatilieni Walimu wanateseka hao ndio wadau wakubwa wa kutoa umaskini katika jamii ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaingia Waheshimiwa Madiwani. Ametaja kwenye hotuba yake vizuri, wamepewa semina vizuri tu wakapata mafunzo Madiwani 3,447 na wakajua majukumu mbalimbali ya kusimamia baada ya kujua yale majukumu ya kusimamia wakaambiwa sasa mtalinda mkiwa nje sio kuingia ndani kwenye tenda mtaona mambo mengi. Rudisheni Madiwani waendelee kusimamia haki za wananchi. Diwani ni mtu wa kujitolea. Tumejaribu kuwaombea pikipiki bado mnasema kwamba wao wana biashara zao anazifanya saa ngapi huyu Diwani biashara zake. Mheshimiwa Mbunge ana mkutano sehemu fulani Diwani lazima awepo. Tunahitaji kuboresha kila Kata iwe na Sekondari lazima Diwani awe pale posho yake ni shilingi 20,000/=.

Mheshimiwa Spika, hivi Diwani tunamtetea kweli? Madiwani lazima wafikiriwe. Utakapomfikiria Diwani *already* lazima uteremke chini mpaka kwa Mwenyekiti wa Kitongoji, ndiye anayealika mikutano yote na kusimamia shughuli zote. Wenyeviti wa Vijiji na Wenyeviti wa Vitongoji wanafanya kazi kweli. Fikirieni hilo muone kwamba kuna umuhimu hawa ndugu zetu waweze kufikiriwa. Ni kazi moja ya muhimu wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, ni mengi sana kwa kweli ambayo tunayo lakini mengi mazuri ambayo yamefanywa ila katika upande huu wanatupa shida. Wizara hii naomba iangalie sana masuala hayo. Shughulikieni suala la Hospitali yangu ya Wilaya, shughulikieni Waheshimiwa Madiwani, shughulikieni barabara ya Mbarika na maeneo mengine kama nilivyoyataja.

Mheshimiwa Spika, ukichanganya changanya mengi watu wanaweza wakashindwa kujua ni lipi. Lakini matatizo makubwa kwa Misungwi ndiyo hayo. Naomba niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Wizara ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpa pole Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa ugonjwa wake na nashukuru kwamba amepata afueni amerudi nchini na leo yuko nchini tukijadili Wizara ndani Ofisi yake.

Nampa pole pia Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda kwa kufiwa na marehemu baba yao mpendwa. Nampa pole Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, pole pia kwa Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere na Mheshimiwa Estherina Kilasi .

Naomba nichukue nafasi hii kumpongeza ndugu yangu Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kuwapeta waliotaka kumng'oa katika ulingo wa siasa, hongera sana Mheshimiwa Danhi Makanga. Najua tulikoanzia na Mheshimiwa Danhi Makanga na mikakati yake alivyoipanga nakupongeza sana kwamba ndoto zako zilifanikiwa. *(Makofi)*

Naomba nichukue pia nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Waziri Mkuu kwa hotuba yake ya jana hasa kwa maamuzi kuhusu Walimu. Nampongeza sana. Hilo nitalizungumzia baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali ya awamu ya tatu kwa ujumla kwa utekelezaji wake wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Lakini pamoja na kupongeza Serikali yetu, nianzie ukurasa wa 11 wa hotuba hii. Nianze kwa Makatibu Tarafa halafu nijadili suala la uwajibikaji. Ni kweli Serikali imeamua Makatibu Tarafa ni kiungo muhimu sana katika utekelezaji wa maendeleo ya wananchi Halmashauri na Serikali Kuu. Nimeona waraka uliotolewa na Katibu Mkuu, Utumishi. Lakini inasikitisha kwamba waraka unapotolewa inatekelezwa kwa utashi na hitaji la wale wanaopaswa kutekeleza.

Kwa mfano, Makatibu Tarafa wameambiwa wawajibike na wahudhurie vikao vyote vya Halmashauri ili waweze kutoa taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Lakini kuna Wilaya nyingine mpaka leo hawahudhurii na walipohudhuria kikao kimoja juzi mwezi Juni waliambiwa hatukuwaita kwa hivyo hamtahudhuria kikao hudhurieni kama wananchi wowote wale na hamtalipwa mafuta au nauli mliyokuja nayo mpaka hapa. Mheshimiwa Waziri hiyo ni kweli. Hiyo ni haki?

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ingetekelezwa vizuri kama Mawaziri, Makatibu Wakuu na Watendaji wote wangeamua kuwajibika. Lakini inasikitisha kwamba hata wale wasiowajibika wanakumbatiwa. Nitoe mifano tu ya Wilaya Simanjiro.

Mimi siwezi kusema Wakurugenzi wote utafikiri ni mashine moja imedurufisha. Lakini kwa robo tatu ya majimbo yetu tukiulizana Wabunge kama sio nusu wanalalamika utendaji wa Wakurugenzi. Unaweza kumkuta Mkurugenzi na *cheque* za MMEM 11 zinapelekwa Benki na Kamati husika zinaandikwa *refer to drawer,* haina fedha. Wabunge mnakuwa makachero kufichua hayo mnawafikishia Waziri mhusika na Waziri wa Elimu na Utamaduni bado sasa ni miezi mitatu hakuna hatua iliyochukuliwa.

**MBUNGE FULANI:** *Shame!!! (Makofi)*

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Utakuta *cheque* hiyo na ninazo hapa *photocopy* badala hata ya kuandika *Account* husika imeandikwa *District Road Fund* ndio muhuri uliobandikwa kwenye *cheque* inayokwenda Elimu, hapo kuna nini? Bado nina namba ya hizo *cheque* na mkihitaji nitawapa hizi hapa lakini hakuna hatua mpaka sasa iliyochukuliwa.

Mheshimiwa Spika, kuna fedha zilizotolewa na Wizara ya Maji akapewa huyo Mkurugenzi shilingi milioni 50 toka mwezi Mei, 2003 hizo fedha mpaka leo hazijafanyakazi, ziko wapi hizo fedha? Tumeeleza pia hilo Wizarani. Ukiangalia taarifa ya Mkaguzi Mkuu toka Mtendaji huyo awe pale kila siku *adverse opinion* mahesabu yake ni machafu na hii ya juzi ndiyo kabisa Kamati ya *LAAC* ilishindwa kuzikagua.

Mheshimiwa Spika, hayo yote nimekuwa nikimweleza Waziri husika, Naibu wake, Katibu Mkuu, Makatibu wanaohusika Wizara hiyo. Toka mwezi Juni, 2003 hakuna hatua iliyochukuliwa. Lakini mmoja niliwahi kumwuliza hivi huyu mtumishi angekuwa katika jimbo lako ungefanyaje, akasema ningeshamwondoa. Lakini kwa Simanjiro hamumwondoi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Waziri Mkuu alivyosifia jana Halmashauri zingine kutumia fedha kidogo kujenga madarasa mengi sisi hata yale machache ambayo wananchi wameyajenga hayajamalizika kwa sababu hakuna fedha na Serikali imetuma fedha bado Watendaji hawachukuliwi hatua.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikieleza hili, nimeeleza kwa maandishi lakini kwa masikitiko makubwa Wizara hiyo ikanijibu nisome tu aya ya 2 ya barua hiyo aliyonijibu kwamba: “Barua yako haikuambatanishwa na muhtasari wa Kamati yoyote ya Halmashauri. Kutokana na uchambuzi huo tunashauri masuala hayo yote yaainishwe na kuwasilishwa rasmi na Halmashauri husika.”

Mheshimiwa Spika, mimi niliwahi kumweleza Waziri mhusika kwamba hili mlishughulikie kama tatizo la kawaida kwa sababu mtakapolishughulikia kwenye vikao linaweza kuleta mgawanyiko ndani ya Halmashauri. Kweli hasa imetokea hivyo Madiwani wameshagawanyika na kwa hili nataka Waziri anieleze ndiyo kauli ya Wizara yake ili tukafanye kazi hilo hatutashindwa. Kwani Karatu si walifanya kazi hiyo? Korogwe si walifanya hivyo?

Kama huo ndiyo utaratibu wa Utawala Bora na sisi tutaenda kufanya hivyo, lakini mimi nilidhani utaratibu wa kuzungumza na akahamishwa uhamisho wa kawaida au akachukuliwa hatua kimya kimya ingekuwa ni Utawala Bora kuliko kwenda kufunga kufuli kwenye mlango wa Mkurugenzi. Tunaweza kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata basi kama hawamsikilizi Mheshimiwa Parseko Kone, lakini hata Rais aliyewaweka kwenye madaraka hayo hawamsikilizi? Kwa sababu kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Rais ya tarehe 16 Agosti, 2002 ninayo hapa, katika kutoa mlinganisho wa shughuli katika Halmashauri mbalimbali, nanukuu maneno yake: “Ipo tofauti kubwa sana ya hali ya Utawala Bora kwa vigezo hivi katika Halmashauri 38

zilizopo kwenye Awamu hii ya Kwanza ya Uboreshaji wa Utendaji wa Halmashauri. Katika kigezo cha ushirikishwaji Wilaya ya Simanjiro ni ya mwisho, katika kigezo cha utawala na sheria Wilaya ya Simanjiro ni ya mwisho, katika kigezo cha kuzingatia jinsia Wilaya ya Simanjiro ni ya mwisho." Mwisho Rais amesema: "Lazima changamoto hii ya uongozi ishughulikiwe haraka." Hii ndiyo haraka? Toka Agosti, 2002 mpaka sasa Juni, 2004, hiyo ndiyo haraka? Kwa kweli namwonea huruma Mheshimiwa Rais kwa sababu ni mgonjwa, lakini asikilize akiwa kitandani jinsi maelekezo yake yasivyotekelezwa. *(Kicheko/Makofi)*

Vielelezo hivyo vyote na ukaguzi wa mahesabu hayo viko hapa na Taarifa ya Kamati ya *LAAC* iliyofukuza mahesabu yetu mara ya mwisho iko hapa. Huyo huyo bado anadunda kwa Kiswahili cha mitaani. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa suala hili mimi sitangoja lile la kusema kwamba, litashughulikiwa kiutawala, ili tusisumbuane katika kifungu namba 81, naomba Waziri atakapojumuisha anipe maelezo sahihi.

Mheshimiwa Spika, lingine kwa haraka haraka, ni katika hotuba hii ukurasa wa 14 na ukurasa wa 17 kuhusu kugawanywa Vijiji na Kata. Wilaya ya Simanjiro haijawahi kugawanywa Vijiji wala Kata toka mwaka 1975. Mwaka 1999 tuliomba kugawanywa Kata, lakini nilishuhudia Waziri aliingia kuomba, Mheshimiwa Parseko Kone aliingia kuomba, za Waziri zimegawanywa, za Simanjiro zimekataliwa. Ndilo tatizo lililotupa shida, Wilaya ya Kiteto, waliahidiwa halafu baadaye hazikugawanywa hizo Kata na Vijiji. Tumeshatekeleza masharti yote mliyotupa, tumeandika kwa utaratibu mliotupatia, tumekaa kwenye Halmashauri, naomba tutakapoleta mtukubalie huo mgawanyo wa Kata, Vijiji na Vitongoji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Walimu, jana Waziri Mkuu aliliweka vizuri suala hilo. Hata Simanjiro kuna Walimu ambao hawajalipwa fedha za uhamisho, hawajalipwa mishahara na Mheshimiwa Aggrey Mwanri ni shahidi, yule hakutaka kuhama kwa sababu tu anapenda kukaribia nyumbani, ni kwa sababu hajalipwa mishahara yake toka aajiriwe miaka mitatu sasa.

Mheshimiwa Spika, hivi ukichukua mayai ya kanga akayaatamia kuku atatoka kifaranga gani?

**WABUNGE FULANI:** Kanga.

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Sasa ukiwachukua Walimu ukawaweka mahali pasipohusika hawatakuwa wa TAMISEMI. Kwa hiyo, nashauri Walimu warudishwe Wizara ya Elimu. *(Makofi)*

Kwa nini nasema hivyo? Ukirejea hotuba hii ukurasa wa 36 mpaka 40 ibara ya 53, aliisoma hiyo Mheshimiwa James Musalika, lakini ibara ya 54 inasema: "Kwa mwaka 2004/2005, mpango umelenga kutekeleza yafuatayo kwa upande wa elimu." Hakuna kuondoa kero za Walimu, kati ya kero ambayo ameona yeye Waziri ni hilo la

malipo ya mishahara ya Walimu. Kuwalipa likizo zao, hiyo haipo katika kero alizoziona yeye.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kweli jana aliokoa jahazi. Wahenga walisema: "kila kilio kina mwenyewe", tulifikiri mwenye kilio cha Walimu zaidi ni Waziri wa TAMISEMI, lakini haina! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, kwa sasa siungi mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya mwisho kwa asubuhi ya leo ili niweze kuchangia hotuba hii ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba kuungana na Wabunge wenzangu, kuwapa pole wenzetu wote katika Ukumbi huu waliopatwa na maafa ya kufiwa, waliopata ajali, waliopata matatizo ya kuibiwa na hata wengine kupigwa, tukubali kwamba hiyo ni amri ya Mungu na yote hayo yatapita.

Mheshimiwa Spika, pia, nampongeza Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa ushindi katika uchaguzi na kumkaribisha ndani ya CCM. Kidumu Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono hotuba hii ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, nikisema kwamba, ni hotuba inayogusa sehemu nyingi sana na inapaswa ifanye hivyo kwa sababu ni hotuba ambayo inatokana na Wizara katika Wizara Mama hii ikiwa ni mojawapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kusema kwamba, Wananchi wa Ngara wameniagiza kwamba, niishukuru Serikali kupitia Wizara hii kwa shughuli nyingi ambazo zimetendeka katika muda mfupi wa kuwepo kwangu katika Bunge hili kwa uongozi wa Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi kupitia Wizara hii. Kwa mfano, mwaka huu wa 2004, Wilaya ya Ngara imejaliwa kufungua Sekondari mbili ikiwa ni Wilaya mojawapo ambayo kwa hakika inahitaji Elimu ya Sekondari kwa sababu haina Shule za Sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwezi huu huu wa Juni, 2004, Wilaya ya Ngara imefanikiwa kuzinduliwa umeme, kitu ambacho kwa zaidi ya miaka mingi sana hakikuwezekana na nishukuru sana kwamba kazi hii ilifanywa na Mheshimiwa Makamu wa Rais hapo tarehe 9 Juni, 2004. Naomba niseme kwamba, kwa nguvu za Wizara hii pia Idara ya Elimu katika Wilaya ya Ngara, imeonekana kufanya kazi vizuri mno baada ya kwamba kwa miaka yote tumekuwa ni wamehezi wa elimu na pengine kuwa wa mwisho hata tusionekane kwenye chati katika matokeo ya mitihani ya darasa la saba ya Kitaifa. Lakini mwaka 2003 tulikuwa ni watu wa kwanza Kimkoa, watu wa kwanza Kikanda na ilikuwa ni Wilaya ya nne Kitaifa. Kwa hali hii na mengine mengi ambayo sikuyataja, ni kwa nguvu ya Wizara hii na usimamizi wake bora na kutoa watumishi

ambao ni mahiri na pengine kwa kutazama hizo Wilaya ambazo zimekuwa nyuma kwa miaka mingi, basi Wilaya ya Ngara ikapewa watumishi ambao walikuja wakajituma na kujua ndiyo waliokuwa wanafaa kufanya kazi Wilayani Ngara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukilalamikia watumishi kwa kiasi cha kutosha hasa katika ngazi ya Halmashauri ya Wilaya, ngazi ya Wilaya na maeneo mengine. Lakini binafsi nataka kusema kwamba, sina matatizo kabisa na *DC* wangu, ni kijana mchapakazi, ni mwanajeshi aliyeiva, sina matatizo na Mkurugenzi Mtendaji wangu, yuko pale na hizi kazi amezifanya na anashirikiana na kila mtu na sina matatizo kabisa na Chama cha Mapinduzi. Kwa misingi hii, hata Mheshimiwa Makamu wa Rais alipokuwa Ngara tarehe 8 na tarehe 9 Juni, 2004 ameambiwa habari hii na kuomba kwamba baadhi ya watumishi hao wasingeweza kuondolewa Ngara kwa haraka sana kwa sababu tunawahitaji mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hayo, ziko sehemu ambazo zinahitaji kuguswa kwa sababu ya kuishauri Serikali kufanya vyema zaidi. Naomba kuzungumzia elimu. Napenda kabisa kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake na maagizo yake ya jana kwamba, malipo ya Walimu ya Shilingi bilioni 9 yatoke mara moja katika mwezi unaokuja. Lakini bado kuna tatizo la kuboresha elimu na ninaamini ni nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, tunapokuwa tunajaribu kumaliza madai haya, Walimu wanaishi katika mazingira mabaya sana. Walimu hawana nyumba, wanasafiri mwendo mrefu sana kutoka wanakoishi kwenda vituo vya kazi, wengine imekuwa ni kama hawafanyi kazi kwa sababu muda wao unaishia katika kusafiri na pengine wanafanya kazi na matumbo matupu kiasi cha kwamba, wanapoingia madarasani hawawezi kufanya kazi inavyohitajika kwa sababu hakuna nyumba karibu na vituo vya kazi na kwa hiyo muda mwingi wanakuwa wana njaa.

Mheshimiwa Spika, kwa hali ilivyo, Walimu wanahitaji kupewa nyumba kwa sababu walio wengi sasa wanakaa majumbani kwao na wamekaa katika kituo kimoja pengine kwa zaidi ya miaka 20 hata 25 sasa wamekwishakuwa ni mangimeza na hawawezi kufanya kazi zao vizuri. Kwa upande huu, Wizara hii ikishirikiana na Wizara ya Elimu na Utamaduni, kuna haja ya kutazama eneo hili la kuwa na mazingira mazuri kwa walimu wetu kusudi kazi iweze kufanyika vizuri na hii ni kwa Elimu ya Msingi na Elimu ya Sekondari. Lakini pia Walimu wengi sasa hivi wanataka kupata masomo zaidi. Kwa sababu tunataka kujikomboa na elimu na tumekuwa tukisema kwamba elimu katika Tanzania hailingani na elimu katika ulimwengu wa sasa wa ushindani, kwa kweli Walimu wetu wengi ni lazima wapate elimu zaidi na katika hali hii kuna haja ya kuongeza Walimu kiasi cha kutosha.

Mheshimiwa Spika, Makamu wa Rais alipokuwa Ngara na kukutana na wazee, hili lilikuwa ni ombi moja kubwa kutoka kwa wazee wasomi kwamba, ingekuwa ni vizuri Wilaya ya Ngara ikapewa Kituo cha Ualimu kwa maana ya Chuo. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, ashirikiane na Waziri wa Elimu na Utamaduni katika suala hili.

Mheshimiwa Spika, nilipokuwa Bungeni hapa mwaka wa 1975 - 1985 nilishughulikia kitu hiki. Lakini kilipokuwa kimekaribia kufika mahali pake kwa bahati mbaya nikawa sikurudi kwa sababu alizozitaja pale ndugu yangu, Mheshimiwa James Musalika. Kwa hiyo, ninaomba suala hili litazamwe na ikiwezekana lifanyike.

Mheshimiwa Spika, niombe kuzungumzia suala la Madiwani. Wengi wamezungumzia suala la Madiwani, lakini mimi nasema kwamba, kama Madiwani wasipopewa nafasi nzuri ya kufanya kazi, kwa kweli maendeleo ya nchi hii yataendelea kuwa madogo sana. Diwani anafanya kazi nyingi, inawezekana siyo kazi za kitaalam, lakini ni kuliko Mkurugenzi Mtendaji, kuliko *DC,* kwa sababu wote hawa wanapoteremka kwenda kwenye Kata na kwenye Vijiji, Diwani ndiye mkaribishaji wao. Diwani ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Kata, Diwani kwa habari sasa za mipango shirikishi ndiyo Bwana Mipango Kijijini na ndiye mwandaaji. Chama cha Mapinduzi hakina mahali ambapo kinaweza kikafanya kazi yake vizuri katika Kata kama Diwani atakuwa ni mpinzani au ni mvivu au hajali. Diwani anasafiri sana kwenye Kata yake, Wilayani kwake na hata nje ya Wilaya kwa sababu ya mikutano, kwa sababu ya semina na mambo mengine kiasi cha kwamba, anayo kazi kubwa sana ya kufanya maendeleo yaonekane.

Ninaomba hawa wawezeshwe, wapewe mikopo hasa pale Diwani anapoonekana kwamba anaweza akaurudisha mkopo huo bila shida ili waweze kufanya kazi yetu vizuri. Madiwani waongezewe posho, wanafanya kazi kubwa. Posho za vikao, posho za madaraka kwa Madiwani hazitoshi, hawana muda wa kuzalisha majumbani kwao, hawana muda wa kushirikiana na familia zao kufanya kazi za maendeleo, wakati wote wanatumikia Taifa.

Kwa hiyo, hakuna sababu ya kutowapa nafasi nzuri ya kufanya kazi ikiwa kweli tumeamua kujikomboa na dimbwi la umaskini katika nchi hii. Madiwani ni watu muhimu. Mimi nimekuwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya kwa vipindi viwili kwa miaka inayofika kama 11, ninajua uzito wa Diwani na kazi anazozikabili. Ninaomba Madiwani wafikiriwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lipo suala zuri sana la Watendaji wa Vijiji kuajiriwa. Mabadiliko yaliyokuwa yametokea wakati ule hayakupata nguvu ya kutosha na iko mifano ambapo wale wengine waliojaribu kuajiriwa walishindwa. Watendaji wa Vijiji hawa kwa sababu ya elimu yao ndogo inaweza ikaonekana kwamba hawafanyi kazi zao vizuri, lakini mimi nasema wanafanya kazi zao vizuri sana na wengi wao ni waaminifu mno. Wanajua kwamba pengine ni kwa nguvu ya CCM wameweza kupata nafasi hizo kwa sababu wasomi wapo wengi, kwa hiyo, wanajitahidi kuwa waaminifu, wanajitahidi kuwa wenye bidii na wanajitahidi kwenda kazini kwao mapema kadri inavyowezekana kusudi watekeleze shughuli zao.

Sasa wote tunafahamu wako watu mashuhuri katika ulimwengu huu ambao hawakuwa na Elimu, lakini walifanya kazi za ajabu. Mmojawao ni Sir Wilson Churchill, ambaye ilifikia mahali akazikwa katika makaburi ya wafalme. Tunajua elimu ya Sir Wilson Churchill, sasa wako Madiwani wenye uwezo wa aina hiyo. Hawa

waachishwe kazi au wafukuzwe kazi kulingana na uwezo wao. Wafanye kazi, wapimwe *match* zao zinavyoweza zikafanya kazi vizuri, ikionekana kwamba hawawezi basi waachishwe, lakini si kwa sababu ya kusema tu kwamba, hawana elimu basi wote wakaswagwe. Wanasema Serikali inawafukuza kwa sababu hawakusoma. Kutokusoma si kosa lao, kutokusoma ni uwezo mdogo wa Serikali. Kwa hiyo, kwa sababu hiyo hawawezi kupewa adhabu hiyo kama wengine kazi wanaziweza. Naomba kabisa Serikali ilione hilo na waachishwe kazi watu hawa kulingana na uwezo watakaokuwa nao.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la kilimo. Ni aibu kwamba, baada ya miaka hii 43 nchi yetu inaweza kuendelea kuomba chakula. Miaka mitatu baada ya kukomboa nchi ya Uganda tulipewa chakula cha msaada, mahindi. Tulipo hapa tumekuwa tukipata chakula kutoka Msumbiji ambao bado wana vita ya ndani ya wao kwa wao, ya kisiasa. Sasa juzi tulikuwa tukiambiwa tumekwenda kupata chakula bure kutoka Ethiopia, kumbe tulikinunua, lakini ni kwa nini tunafanya hivyo?

Mheshimiwa Spika, nchi hii ina milima mikubwa inayoteremsha maji mabondeni, ina mito mingi sana mikubwa na midogo, ina maziwa mipakani mwa nchi yetu na ndani ya nchi, maziwa haya yote au maji haya yote kwa jumla sijui kwa nini tunayaacha? Ni kwa nini hatuwezi kuyatumia kumaliza mzigo huu?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala, alikuwa Ngara mwishoni mwa 2002, alizunguka Wilaya ile akayaona mabonde mazuri yenye maji mengi, akaona Wananchi wanavyojibidiisha na kilimo cha umwagiliaji. Sijui tunategemea kupewa nini? Mwaka wa 1974 Korea walianzisha kilimo cha kumwagilia maji nchini hapa na Ngara wakapewa skimu ndogo sana. Kama tulivyokuwa tukipata misaada miaka ya nyuma na inaharibika, bado na mradi huu ulikufa, lakini mpaka leo, mtu kama akienda Ngara akatazama jinsi watu walivyovamia matingatinga kwa maana ya mabonde, atafurahi sana. Nimeagizwa na Wananchi wa Wilaya ya Ngara kwamba, Serikali iwape uwezo wa kulima kilimo cha umwagiliaji. Wanachohitaji ni teknolojia ya kisasa, wanachohitaji ni nyenzo za kuendeleza kilimo hicho na ari wanayo. Ngara sisi tunavuna mara tatu kwa mwaka, tunavuna masika, tunavuna mtoni mwezi wa nane na wa tisa na tunavuna wakati wa mvua za kwanza kwanza za mwezi wa 12. Sasa, hali hii iko katika Mkoa mzima wa Kagera, iko katika Mkoa mzima wa Kigoma, sioni kwa nini tuendelee kuonekana tunaombaomba chakula katika nchi hii wakati uwezo tunao. *(Makofi)*

Hivi karibuni nilikwenda katika Mkoa wa Morogoro, nilikuwa katika Wilaya mpya ya Mvomelo. Huko kuna maji mengi na wanalima mwaka mzima, lakini bado hivi karibuni imesikika kwamba na Mvomelo nao walipewa chakula cha njaa, ni aibu sana, inasikitisha mno! Ujeuri wa Mmarekani ni chakula, Marekani inajaribu kuiogopa China kwa sababu China ina chakula. China ina watu wengi kuliko Marekani na nafikiri imejikomboa nyuma yetu, sasa inakwenda juu kwa sababu wana chakula. Leo tunaomba chakula Ethiopia, kesho tutakwenda kuomba chakula Misri ambao wanatumia maji ya Mto Nile. Wako jangwani, sisi tumebarikiwa kila kitu, kwa nini iwe hivi?

Ni kwamba, tunapanga vibaya, Wizara yetu ya Kilimo haifanyi kazi au Serikali haina nia ya kuona kwamba inazidi kujenga heshima na utu wake? Naomba mtusaidie watu wa Ngara tufanye kazi ikiwezekana mtupe Mkoa wa Shinyanga na Mwanza ambao wana matatizo ya maji basi, tunaweza tukawalisha chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru, naomba niachie hapo kwa kuunga mkono tena hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda uliobaki hautoshi kwa mchangiaji mwingine ambaye angekuwa ni Mheshimiwa Omar Chubi. Kwa hiyo, ajiandae kuwa mchangiaji wa kwanza kipindi cha mchana. Orodha ya wengine waliopangiwa siku ya leo ipo kwenye ubao wa matangazo kama kawaida.

Baada ya maelezo hayo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.57 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**MHE. OMAR S. CHUBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, nikiwa mchangiaji wa kwanza jioni hii ili na mimi niweze kusema machache juu ya hoja iliyoko mbele yetu. Kama ilivyo ada na mimi niungane na Waheshimiwa wenzangu, kwa kuwapa pole Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kutokana na msiba uliowapata wa kufiwa na baba yao mpendwa, namwomba Mwenyezi Mungu, aiweke roho ya marehemu peponi. *Amin.*

Pia nitoe pole kwa Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere na Mheshimiwa Estherina Kilasi, kwa mikasa iliyowakuta wakiwa wanasafiri kuja huku Bungeni. Nawatakia afya njema.

Baada ya kusema hayo kwanza na mimi niseme kwamba, ninampongeza sana mtoa hoja kwa jinsi alivyotoa hoja yake ya kueleweka na pia ninampongeza Naibu Waziri, Mheshimiwa Mizengo Pinda, kwa ushirikiano wake ambao ameutoa kwetu kila tunapokuwa tunamwomba msaada, kama ilivyo kawaida anavyofanya Mheshimiwa Waziri. Pia nimshukuru Katibu Mkuu, Bwana Deo Mmari, ni muwazi kila unapokwenda kumweleza shida kusema kweli unafarijika na anakupa matumaini ambayo siyo ya kubabaisha, anakupa mambo ambayo yanafaa. Kwa kweli niseme kwamba, timu ya Wizara, imekamilika na ndiyo maana mambo yao yanakwenda vizuri na kwamba hayaendi ovyo ovyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niseme neno moja tu kwamba, Wilaya ninayotoka mimi ukubwa wake ni kama Mkoa wa Kilimanjaro, kwa wale waliosomea mambo ya ardhi watajua Mkoa wa Kilimanjaro una *square meter* takriban 13,000 hivi. Sasa hapa ninachotaka kusema ni kwamba, kwa utaratibu wa kutaka kuleta maendeleo

yaliyo ya kweli, Wilaya hii inaongozwa kwa tabu sana kwa mfano, tunakopakana na Rufiji, pale ambako tunakabidhiana mwenge mpaka wa Kilwa na Rufiji, kuja Wilayani ni takriban kilometa 162. Tunakopakana na wenzetu wa Liwale kuja Wilayani ni karibu kilometa 168. Sasa kusema kweli kwa umbali huo kutokana na matatizo yaliyoko ya miundombinu katika namna fulani na kama unavyojua bado watu wanambeba mtu kwenye machela kumpeleka hospitali ukitoka kilometa moja, nafikiri ikifika kilometa 20 anakuwa ameshapoteza maisha. Sasa inapotokea haja ya kwamba, labda suala hilo mtalikuta huko Wizarani, katika utaratibu unaofuata basi nilikuwa nakuomba Mheshimiwa Waziri, usiliweke pembeni, ufanye tu kama ulivyofanya Morogoro kwa sababu misingi ambayo imefanywa kugawa baadhi ya Wilaya za Morogoro, ni ya kijiografia na hili ninalotaka kuzungumza utakapopata hilo dokezo mambo yote yanatokana na masuala ya kijiografia.

Sisi wakati tunaponadishwa kutaka kupata dhamana ya kuongoza dola, huwa anashikwa Mheshimiwa Diwani, Mheshimiwa Mbunge na anayetushika mikono hiyo ni Rais. Lakini utakuta sasa hivi kuna matatizo makubwa sana hata ya kiuhusiano kati ya Madiwani na sisi Wabunge, hasa kutokana na hali halisi kwa sababu nafasi hizi ni tofauti ingawa zote ni za kisiasa. Lakini kusema kweli Madiwani wengine hali zao nzuri na wengine hali zao ni duni. Sasa mimi nadhani siyo katika kujifagilia tu tunapokwenda kwenye uchaguzi, lakini nadhani Serikali ingeweza kutazama angalau kuongeza posho za Madiwani huko waliko ili angalau zisifanane na zetu lakini angalau wafike mahali ambapo na wao wajikute tuko pamoja. *(Makofi)*

Unajua njaa huleta chuki, hata bila kuwa na uhakika kitu gani tunapata lakini wale wasiotupenda wengine wanajaribu kuweka habari za uongo kwamba, mapato yetu ni makubwa, kiasi kikubwa sana, kiasi ambacho hata watu wanatuongezea chuki. Ndiyo maana unakuta ukitoka hapa utakuta hapo mlangoni ukiona unasubiriwa na watu sita unageuza unakuja kutokea mlango mwingine wa wageni. Hii ni kutokana na maneno ya watu wabaya ambao wanasema kwamba, sisi tunazoa pesa nyingi sana. Wanaokimbia siyo mimi tu peke yangu, tuko wengi humu kwa sababu kila siku unamkuta mwananchi ana shida. Maana yake Mbunge siyo lazima useme kwamba wewe siyo mwananchi wangu, wewe ni mtu wa Dodoma unakuja kuniomba mimi msaada mwone Mheshimiwa Hashim Saggaf, hatuendi hivyo, kama unamkuta mwananchi hali yake ni mbaya na kama unazo senti mfukoni unamsaidia. Lakini sasa kuna maneno ya hatari leo anasema mume wangu yuko Milembe, naomba unifanyie mpango, kesho anasema nimefiwa na mume wangu, yule yule uliyemkuta jana. Sasa dawa ya kufanya hapa una-*check* kwanza unabana wanapouza vifaa pale unaangalia getini kuna watu wangapi pale, kama kuna sita unageuzia huku, unakuja geti hili unakuta wamekaa sasa unabana kantini. *(Makofi/Kicheko)*

Haya maisha ya dhiki, lakini inatokana na hali yetu ya uchumi, *Inshallah* hapo baadaye nadhani hatuwezi kukimbiakimbia, lakini huo ndiyo ukweli wa mambo. Sasa kama sisi tunakwepa namna hii, je, hawa wenzetu wako vipi? Kwa hiyo, mimi kilio changu namwomba Mheshimiwa Waziri, ajipigepige angalau katika ahadi atakazozitoa kwetu na wenyewe awafikirie hawa ndugu zetu Waheshimiwa Madiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo ya kuchanganganya, pale TAMISEMI kuna mtaalam mmoja, sitaki kusema kwa ubaya, lakini kwa kutaka ufafanuzi kwa jina la Nyakilaganyi. Mheshimiwa huyu anasema katika laini fulani sisi Wabunge ni Madiwani, wakati mwingine kama kuna semina Wabunge, hatuhusiki. Sasa siyo Madiwani, sasa tatizo lake ni nini? Mimi sielewi kwa sababu kama Mbunge unatoka na gari lako umejaza mafuta *full tank* unakwenda kule unakuta posho ya shilingi 20,000/= au 30,000/=, hiyo siyo ya kumbadilisha mtu dini na wala mtu mwingine hawezi kusema kwamba, wewe ukihudhuria hiyo semina utakuwa umepata.

Lakini sasa swali hili mimi nafikiri tupate *proper definition* kama tunapoambiwa kwamba na sisi ni Madiwani kama tunavyojua basi kama kuna masuala ya Madiwani sisi wote tushiriki ili tuelezane maneno ya kweli. Lakini kama kuna sehemu ambayo sisi tunapigwa nje, halafu wanakaa wale wenzetu tu, mengi wanatusema vibaya na mfano wake utakuta vikao vyote vile muhimu vya maboresho sisi siyo Wajumbe na kule ndiyo mnaambizana ukweli kwa sababu wakati tunaponadishwa ili tuingie kwenye dola, kila mmoja anasema tutasaidiana na wananchi katika kuondoa kero moja, mbili, tatu, nne. Sasa kuna sehemu Madiwani wanageuka mwoneni Mbunge. Lakini tunapokuwa wote tunaelezana ukweli. Ninadhani *circular* zinazokuja lazima zitamke kwamba, sisi wajibu wetu ni upi, labda kama katika kusimamia maendeleo ndiyo tunajulikana kama Madiwani, lakini kwenye masuala mengine hatumo, mimi naona hilo jambo linataka ufafanuzi. *(Makofi)*

Sambamba na suala hilo kuna huu utata uliotokea wa kuondoa Madiwani kwenye Bodi ya Zabuni. Wengi wamelizungumzia hilo. Lakini kama tunataka kusema kwamba nchi hii ina sera ya uwazi *(transparent),* basi tufanye kama wanavyofanya sehemu nyingine badala ya kuajiri *cleaners* wanachukua yale Mashirika ambayo yanafanya usafi, Wizara inajiondoa na sisi hapa tuunde *Independent Board* ambayo itasimamia masuala ya zabuni. Kwenye hiyo Bodi, ninashauri awemo Mkurugenzi na mwakilishi wa Madiwani. Lakini kwa hali ilivyo sasa itakuwaje hao hao watoe zabuni, hao hao ndiyo walipe na hao hao ndiyo wasimamie, jamani tunakwenda hivyo kweli au ni tatizo gani lilijitokeza wakati sisi tunaingia kule mahali?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo lingine katika TAMISEMI juu ya kulundikana kwa Walimu, kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kusema kwamba, ataondoa kero za Walimu. Hilo sote tunaliunga mkono na Walimu tangu jana wameshapiga simu, wengine wanawake wamepiga vigelegele, wanaume wametupigia simu. Lakini namwomba Mheshimiwa Waziri, ajaribu kuliangalia suala la Walimu kulundikana Wilayani, kufuata waume zao. Wilaya ambayo ina Maafisa walioletwa Wilayani na wake zao ni Walimu inaleta *deficit* ya Walimu wanaotakiwa kwenda vijijini. Sasa maana yake kuna makabila mengine wake zao wako Moshi, wanaume wako Dar es Salaam, Krismas wanakutana mbona ndoa zinadumu, sasa inakuwaje Walimu walundikane Wilayani kwa sababu ya kumfuata mume? *(Makofi)*

Hilo Mheshimiwa Waziri, nafikiri linaturudisha nyuma, tunamwambia Mheshimiwa Joseph Mungai hapa Walimu hawatoshi, Walimu wanajazana Wilaya kufuata waume zao. Itungwe *circular* aidha mmoja achague kama anamtaka mume kazi

ya ualimu aweke pembeni tuajiri watu wengine, inatuletea matatizo sana. Sisi pale Wilayani tuna Walimu 19, lakini kwa nini Mwalimu asiende kule kijijini akafundishe mume achukue pikipiki Jumamosi amfuate wazungumze Jumapili arudi, hili si linawezekana bwana? Haya mambo ni *practical* halafu tunailetea matatizo Wizara yako kwamba, tuna shida hii na hii. Hilo Mheshimiwa Waziri naliomba ulitilie maanani na utakapojibu hoja unieleze suala hili liko vipi? *(Makofi/Kicheko)*

Mwisho, niseme tu kwamba, nimefarijika Mheshimiwa Waziri umefanya ziara kwetu, umekuwa mwanakijiji wetu na nilikuwa nawaita Mawaziri wengine kwa sababu anapokuja Waziri fulani barabara zinatengenezwa, miundombinu inakuwa sawa. Sasa ninatoa wito kwa Mawaziri, Ma-*comrade* wenzetu, mje na sisi mtutembelee kwa sababu huko Kusini mlikokuwa mnasema zamani sasa kumebadilika, hamuwezi kulala Rufiji kuna daraja, kule mbele lami inatengenezwa mpaka Lindi, kama pale Kilwa tuna hoteli za kitalii nne, *RC* yupo hapa anasikiliza kama nasema uongo, tuna *Kilwa Ruins,* tuna *Kilwa Resort* unalala dola 60, dola 100, dola 140, ndiyo sasa hoteli ya kitalii ukalale kwa Sh. 5,000/= bwana. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa tunawaomba ndugu zetu, tuendeleze ushirikiano lakini baadhi ya Mawaziri wengine ambao mlitutembelea sisi tunafarijika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia mchana wa leo. Kwanza, napenda niungane na wenzangu katika kutoa pole kwa wenzetu, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kuondokewa na baba yao. Pia napenda kuwapa pole wenzetu wote waliopata mikasa mbalimbali hivi karibuni. Ninawaomba wakumbuke kushukuru kwa kila jambo kwani hayo ni mapenzi ya Mungu kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuipongeza Wizara kwa kutoa hotuba nzuri na imeeleweka. Ningependa niwasihi pamoja na hotuba nzuri hiyo tunawaomba wakafanye kazi ili wazibe mapengo katika yale mapungufu ambayo leo Waheshimiwa Wabunge, wamekuwa wakiyazungumza. Mimi naamini timu nzuri iliyopo hapo juu inafanya kazi vizuri na tunaweza tukafikia malengo yetu na hivyo kutusaidia kutimiza ilani yetu ya uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningependa nimpongeze sana Waziri Mkuu, kwa kauli yake aliyoitoa jana, maagizo mazito na makini ambayo naamini sisi sote tutamsaidia katika kuhakikisha kwamba, maagizo hayo yanatekelezwa. *(Makofi)*

Sasa nianze kuchangia kuhusu Ofisi za Wabunge. Hili suala lilikuwa hata nisilizungumzie, lakini leo asubuhi tulipokuwa tukigawiwa hotuba kukawa na kiambatanisho kikionyesha wale wenye ofisi na wasiokuwa na ofisi. Sasa mimi nashaangaa kulikoni wengine hawana ofisi? Mimi ningependa hapa leo nizungumzie Wabunge wa Viti Maalum. Wabunge wa Viti Maalum hatuna ofisi mpaka leo, la

kushangaza kuna mikoa mingine kama Pwani nimeona wananazo ofisi, Mkoa wa Rukwa pia wanazo na sehemu chache wanazo ofisi hizo. Lakini wengine kama sisi wa Dar es Salaam, Tabora na kwingineko, hatuna. Mimi ningependa leo nitoe masikitiko yetu na mjue tunafanya vipi kazi. Sasa tunafanyaje kazi wakati hatuna ofisi? Iliyopo ni kwamba, Mheshimiwa Mbunge, unapigiwa simu nikuone wapi? Kwanza ile simu ana-*beep* hana pesa, kwa hiyo, unapata gharama ya kumpigia, ukishampigia nikuone wapi huna ofisi, ukimpeleka nyumbani lazima umpikie ugali, ukimpeleka kwenye mgahawa, lazima umnunulie chai, zote hizo ni gharama, yote haya ni kwa sababu hatuna ofisi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mfikirie kabisa kwamba na sisi tuna kazi kubwa ya kufanya na tunatafutwa. Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum, anahudumia Mkoa mzima. Sasa ataitwa Wilaya hii atakwenda na gari lake atarudi, lakini akijulikana yuko wapi atafuatwa alipo. Kwa hiyo, naamini Waziri umesikia kilio chetu na kwa vile hatupati fedha za simu na za *entertainment,* naomba mfikirie kutupatia ofisi. *(Makofi)*

Mimi nitoe mfano mmoja, nilikwenda Tabora kumwona mjukuu wangu, Mheshimiwa Said Nkumba, nilipofika ofisini kwake, nikamwuliza ofisi hii ndiyo uliyopewa na Serikali akasema hapana, bibi ujue ofisi hii mimi nalipa kodi mwenyewe, nikamwambia basi kama unalipa kodi hata Ofisi ya Ubunge, sasa sijui Wabunge wangapi hawana ofisi? Kabrasha linaonyesha Wabunge wengi hata wa majimbo hawana ofisi. Naomba hilo lishughulikiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kidogo nizungumzie elimu na hasa elimu yenyewe tutazungumzia tukipata nafasi wakati wa Wizara ya Elimu. Tatizo langu ni Walimu, pamoja na jitihada zetu zote za MMEM, MMES na nyinginezo, tunapokuwa na Walimu wasiokuwa na furaha, wasiopata mahitaji yao ya lazima, hatutafikia malengo yetu haya, hakuna haja ya kuwa na majengo wakati Walimu wakifika pale wananuna, watoto wanachapwa bila sababu, hasira yote ni kwa sababu hawana mshahara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini kwamba, agizo la Waziri Mkuu litachukuliwa ipasavyo. Lakini nina tatizo moja, Waziri wa Fedha aliposoma bajeti yake wametenga shilingi bilioni 9 kulipia madeni sugu pamoja na mishahara ya Walimu na marupurupu yao, Walimu wanadai shilingi bilioni 12, sasa nauliza tutaweza kweli kuwalipa hawa Walimu? Sasa ningeshauri sana ufanywe mkakati maalum, pesa zipatikane popote Walimu hawa walipwe upesi iwezekanavyo. Hasa kinachonishangaza na leo nilisikitika sana, kuna mtani wangu mmoja Mheshimiwa James Musalika, alizungumzia jinsi wanavyodhalilika Walimu wa kike. Hawa Walimu wanafunzi ambao wameajiriwa toka Januari mpaka leo hawajapata mshahara. Jamani hivi kweli hiyo ni haki, miezi yote bila kulipwa mshahara? *(Makofi)*

Kwanza, utaratibu ni kwamba, Mwalimu anapoajiriwa anatakiwa apate posho ya siku saba ya kujikimu, hizi siku saba hakupewa, za miezi yote hiyo toka Januari hakupewa, anategemewa aishi vipi, huu si unyama jamani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa Walimu wanafunzi wanatakiwa walipwe 80% ya mshahara wa Mwalimu wa *Grade III A,* hawajalipwa hata senti tano. Sasa nataka

niitanabaishe Serikali kwamba, imekiuka haki ya msingi ya kibinadamu. Serikali imekiuka Katiba, ibara ya 23(2), nataka ninukuu kwa ruhusa yako. Ibara hiyo inasema: "Kila mtu anayefanya kazi anastahili kupata malipo yake ya haki". Serikali mnafanya nini kwa kuwanyima hawa mishahara? Mpo tayari kupelekwa Mahakamani na Walimu kwa sababu wana-*grounds* kabisa za kuipeleka Serikali Mahakamani kwa kutowalipa mishahara yao. Tena wakienda Mahakamani watalipwa na *interest* ya pesa zao, pamoja na fedha za usumbufu. Naomba tafadhari Walimu walipwe fedha zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashauri katika hiyo Tume ambayo itaundwa ipewe muda mfupi iwezekanavyo. Tuna uzoefu Tume zinakwenda mpaka tunaweza tukakaa miezi mitatu wale vijana kule wanapata shida, wanaolewa, wanabakwa kwa sababu hawana mishahara. Kwa hiyo, naomba hiyo kazi ifanywe upesi iwezekanavyo angalau kwa muda wa mwezi mmoja na ikiwezekana wapatikane Wabunge wawili, watatu, kwa sababu wao ndiyo wenye uchungu waingizwe ndani ya Tume hiyo. Waziri Mkuu, sijaribu kukufundisha kazi yako, lakini tunakuomba katika hiyo Tume uweke na wanasiasa japo watatu, ili kazi tujue inakwenda kama ipasavyo. *(Makofi)*

Lakini ningependa pia kuchukua nafasi hii jamani kuwapongeza Chama cha Walimu Tanzania, wamefanya kazi nzuri, wametueleza matatizo yao, mimi binafsi nilikuwa siyajui. Lakini vyama vingine *(Civil Society Organizations)* nyingine zifanye kazi kama hii kwa sababu sisi kama Wabunge, tunatakiwa tufanye kazi *in partnership* na *civil society* wao wana muda wa kufanya utafiti, wana muda wa kufanya shughuli nyingi zaidi kuliko sisi kwa hiyo, wanaweza kutusaidia tukaja Bungeni, tunafanya kazi kama *partners* na siyo kama maadui na hizi *NGOs*. Nawapa hongera sana Viongozi wa Chama cha Walimu, endeleeni na tutawatetea ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sasa nizungumzie kuhusu vijana Mjini Dar es Salaam. Sisi wananchi wa Dar es Salaam na viongozi wetu hatuna matatizo na Wamachinga. Tunachotaka Wamachinga waje wafanye shughuli zao kwa utaratibu ambao tunauweka. Ningependa niupongeze sana uongozi wangu wa Mkoa na Manispaa zake kwa kuwa wabunifu wa kutengeneza taratibu mbalimbali kuhakikisha Wamachinga, Mama Ntilie, Baba Ntilie na wengine wote, wanapata nafasi nzuri za kufanya kazi. Nichukue nafasi hii pia kumpongeza Waziri wa Fedha, alipotuona tunahangaika sana alitoa shilingi milioni 100 katika fedha ambazo nadhani kila Mkoa wanastahili kupata zinapitia *SIDO* kujenga mabanda ya Mchikichini. Tunachukua zaidi ya vijana 1,000 wanafanya biashara. Naamini kama Mikoa mingine ikifuatilia hizi fedha watazuia wimbi la vijana wengi zaidi kuja mjini. Kwa sababu kule kule kutokana na fedha watakazokuwa nazo, pamoja na hii miradi mikubwa mikubwa, mikakati ya kilimo, mimi naamini wimbi la vijana kuja mjini litapungua. Hawaji kwa amri yao wanakuja kwa sababu ya kukimbia jembe la mkono kule kwenye miji midogo. Lakini yote hiyo Uongozi wa Dar es Saalam unafanya kazi nzuri namna hii ni katika kutekeleza Ilani ya CCM. CCM sisi tuko *sensitive* na wananchi wetu, vijana wetu, wazee wote tunawajali na tutaendelea kuchapa kazi. *(Makofi)*

Ningependa nitoe mfano mmoja ambao ningependa na mikoa mingine iige, katika kutekeleza hizo sera zetu, Dar es Salaam tumeanzisha Soko la Jumamosi na Jumapili,

kwa wasiolijua liko katika Mtaa wa Lumumba kona ya Mkunguni na Lumumba na kona ya Uhuru na Lumumba, pale ukifika siku ya Jumamosi na Jumapili utashangaa vijana, wazee, watu wazima, wote wako pale wanafanya kazi kuanzia saa 12. 00 asubuhi mpaka saa 5.00 usiku, hatuwatozi hata senti tano ya kodi wala nini, huo ndiyo Uongozi chini ya Serikali ya CCM. Vijana hawa hakuna anayewasumbua. Ikifika saa 5.00 watu wa Manispaa wanakuja wanafagia, asubuhi kazi zinaendelea kama kawaida. Siku mbili za wiki na tunaendelea tunaweza tukatafuta mitaa mingine pia tukaifunga kwa siku mbili. Kwa hiyo, sisi tunasema tuendelee kuwasaidia vijana wetu na Waziri wa Fedha, aendelee kutusaidia ili vijana wasisumbuke sumbuke mijini. Hata wale ambao wanakaa vijuweni msidhani kuwa hawataki kufanya kazi, wanataka kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaja hapa mimi nilipitia vijiwe vya vijana, nilienda Bungoni, Bomu, Kishamapendo, Ashanti, Mchikichini kule Kijiwe cha Simba, Chakala, Kijiwe cha Zungu, Mchichikini Bondeni, Tambaza, kote huko nilifika, vijana wanasema mama tunataka kazi tumechoka kuwa magolikipa, tunakaa tu hata Saigoni wanataka watafutieni matrekta wataenda kulima, wanashangaa mbona wenzetu wanarudi nyie mnasema sisi twende huko? Lakini sasa kwa vile tumesikia, kuna utaratibu mzuri tunategemea mambo yatakuwa mazuri na vitu kama hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba kuongelea kuhusu viwanja mijini. Wananchi wa Dar es Salaam wanaomba TAMISEMI isaidie Manispaa zake kuitafutia mikopo mahali popote ili Manispaa nazo ziweze kupima viwanja, kama vimepimwa viwanja 20,000 Manispaa iweze kupima viwanja. Katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 61 amezungumzia lakini kwa kifupi sana. Ule utaratibu wa viwanja 20,000 ni mzuri sana, lakini viwanja vile vimechukuliwa na wakubwa tu, kiwanja cha Sh. 500,000/= mpaka shilingi milioni 7 mtu wa kawaida hawezi. Ili tuondoe *squatters* na ili tuondoe watu kujenga mabondeni, tunaomba Serikali Kuu isaidie Manispaa hizi, ziweze kupima viwanja na hivyo kupunguza *squatters. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ukubwa wa Kata hili pia Waziri amelizungumzia lakini nasisitiza kwamba, tuna Kata nyingine zina watu zaidi ya laki mbili na inakuwa vigumu sana watendaji wa Kata kuweza kuhudumia Kata kubwa kama Mbagala, Mbagala Kuu, Chalambe, Kigamboni, Buguruni na kadhalika. Naomba hizi Kata zitazamwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuhusu afya jijini, utanisamehe pengine naweza nikakosa nafasi ya kuzungumzia kwingine isipokuwa naomba Dar es Salaam tupatiwe Hospitali ya Mkoa kama mikoa mingine. Hospitali ya Muhimbili ni Hospitali ya Taifa na sasa wananchi wa Dar es Salaam wanaelewa kwamba, huwezi kwenda Muhimbili, zamani walikuwa wakiingia Muhimbili kwa njia za panya. Lakini sasa hivi huwezi kutibiwa Muhimbili bila rufaa. Matokeo yake hospitali za Wilaya hizi tatu zinajaa watu sasa. Kwa hiyo, tunaomba tupate Hospitali ya Mkoa na vile vituo vya afya viwe *upgraded* ili viweze kutoa huduma bora zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kukushukuru sana wewe na Mheshimiwa Spika, kwa kuniwezesha na mimi nichangie kwenye hoja hii. Lakini pia kwa kuliongoza Bunge letu vizuri, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo ada na mimi niungane na wenzangu, kuwapa pole Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na mzazi wao, tumwombee Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema. *Amin.*

Pia nitoe pole kwa Waheshimiwa Wabunge, waliopata misukosuko mbalimbali barabarani ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela na familia yake, Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, Mheshimiwa Estherina Kilasi na wote ambao wamepata misukosuko kwa njia moja au nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana rafiki yangu, Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Mbunge na nilipomwuliza akasema bwana nilikuwa nimepitia mlango wa uwani kuja Bungeni sasa napitia mlango wa mbele. Kwa hiyo, ninampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Tawala za Mikoa, Mheshimiwa Brigadia Jenerali Mstaafu Hassan Ngwilizi, pamoja na Naibu Waziri wake na Katibu Mkuu, Ndugu Deo Mmari, kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya katika Wizara hii. Wanastahili kupewa pongezi. Naomba waendelee kuchapa kazi kama kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mnyimi wa fadhila kama sitampongeza sana Mkuu wa Mkoa wa Singida, Mama Halima Kasungu, ambaye yupo pale juu kwamba, toka amefika Mkoa wa Singida mambo yanakwenda vizuri, shughuli zinakwenda vizuri, uratibu wake unakwenda vizuri na kazi nzuri inafanywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Wasaidizi wake wawili nao pia ninawapongeza, kwanza Kada wa Chama Cha Mapinduzi, Ndugu Said Thabiti Mwambungu, ambaye sasa amehamishiwa Kibaha na tumeletewa Kada mwingine, Kapteni James Yamungu. Wote hawa wawili, ninawapongeza kwa kazi nzuri ambazo wanafanya. Ninampongeza pia *DED* wa kwetu, ndugu yangu, Ndugu Charles Mwagoha, kwa kazi nzuri ambayo anaifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri yetu ya Wilaya ya Singida inafanya kazi nzuri. *DED* na Watendaji wake wanafanya kazi nzuri. Upungufu uliopo ambao mimi ninauona kwa sasa unatokana na habari hii ya ruzuku ambayo tunasema inatoka Serikali Kuu. Baada ya kupitisha maamuzi yale ya kwamba sasa zile njia kuu za mapato kuondolewa kwenye Halmashauri na kutegemea ruzuku kutoka Serikali Kuu, ninadhani hili halijakaa sawasawa. Halijakaa sawasawa kwa sababu si kweli kama anavyosema Waziri wa Fedha, ninamheshimu sana, aliposema kwamba fedha zote zile ambazo walikuwa wanapata Halmashauri hata sasa wanapata. Mimi nasema si kweli. Uko

upungufu na hivyo unayumbisha kwa njia moja au nyingine Halmashauri yetu nina hakika hata Halmashauri nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tatizo lingine katika fedha hizi ni kwamba, zinachelewa sana hazifiki katika wakati unaohitajika. Sasa unapochelewa basi maamuzi nayo yanachelewa, *action* nazo zinachelewa. Kwa hiyo, Halmashauri inaweza ikaonekana kuwa inayumba au ina upungufu kutokana na hali hiyo. Kwa hiyo, niiombe sana Serikali hili suala la ruzuku waliangalie vizuri, wawasiliane vizuri na kuwe na mawasiliano mazuri kati ya Halmashauri na Serikali Kuu na hasa Hazina ili tatizo hili liondoke.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepitisha Bajeti nzuri sana hapa hivi karibuni. Nampongeza sana Waziri wa Fedha, kwa bajeti yake nzuri na ninawapongeza Wabunge kwa kuipitisha. Lakini kuandaa bajeti ni suala moja, utekelezaji wa bajeti ni suala la pili. Unaweza ukaandaa bajeti nzuri lakini utekelezaji ukawa siyo barabara. Kwa hiyo, ikawa ni matatizo. Kwa hiyo, niombe au niseme changamoto iliyopo sasa ni kuangalia kiasi gani nafuu inayotolewa, hasa katika vile vifungu ambavyo vimeonekana vitawasaidia sana wananchi wa vijijini. Unafuu ambao umeonekana kwenye bajeti ningeomba kweli uonekane kwa dhahiri kwa matendo huko vijijini kulikoni kubaki katika makaratasi. Uzoefu unaonyesha kwamba, Bunge hili linapitisha mambo mazuri sana ya unafuu kwa wananchi wetu lakini hayafiki kwa walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe sana suala hilo liangaliwe kwamba unafuu huu uliosemwa, kwa mfano, habari ya matrekta kwamba bei yake itakuwa nafuu na kadhalika na kadhalika. Hebu basi kweli hali hii ifanyike na wananchi vijijini wanunue matrekta kwa bei nafuu ambayo ndiyo azma ya kupitisha bajeti katika Bunge hili. Tusiwafaidishe wafanyabiashara au wenye viwanda na kadhalika. Natoa mfano, katika bajeti ya mwaka 2002/2003, Waziri wa Fedha, alitoa punguzo la kodi nadhani kwa *Furnace Oil* la asilimia 20 ili kupunguza gharama za uendeshaji kwenye viwanda na kwa ajili hiyo gharama za bidhaa zipungue. Lakini hakuna kilichofanyika, bidhaa zilizidi kupanda, *cement*, mabati yamepanda, nondo zimepanda. Lakini wenye viwanda walipata hiyo nafuu. Sasa nasema nafuu hii ambayo tumeipitisha hapa iende kwa walengwa ambao ni wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuangalia matatizo ya Walimu na kutolea maagizo. Nina hakika wote wale ambao wameagizwa watatekeleza bila matatizo. Ni tatizo kubwa sana, lakini liko tatizo nadhani linaweza likawa la kisera. Kwa mfano, *promotion* za Walimu zinacheleweshwa sana na zikishacheleweshwa maana yake ni kwamba, anakuja kuwa *promoted* baada ya miaka miwili au mitatu. Matokeo yake ni nini? Matokeo ni kwamba, wanaweza waka-*back date* hiyo *promotion* miaka mitatu nyuma, lakini Hazina hawana fedha ya mishahara ya miaka mitatu nyuma. Hapo ndipo inakuwa tatizo. Sasa ili kuondoa tatizo hili ni lazima Idara Kuu ya Utumishi, TAMISEMI na Hazina, wawasiliane vizuri ili kuhakikisha kwamba, *promotion* za Walimu zinatolewa *in time* ili kuepukana na mambo haya ya ku-*back date* na matokeo yake watasema kwamba, fedha hatuna, wataanza kulumbana. Hilo ni moja ya tatizo la kiufundi katika hiyo *issue* ninayoisema ya ku-*back date* au suala la

sera. Hivyo, suala la sera liangaliwe ili kuhakikisha kwamba, chombo cha kupandisha Walimu madaraja kinafanya kazi yake katika wakati unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa upande wa Singida naomba sana watusaidie masuala ya Walimu. Shule inatakiwa kuwa na Walimu 21 inakuwa na Walimu 9 au Shule inatakiwa kuwa na Walimu 16 ina Walimu 6 na kadhalika na kadhalika. Shule kama Matare, Ikungi, Mnang'ana, Sepuka, Nkhiree, Ihanja, zinakabiliwa na matatizo haya. Matokeo yake sisi tumekuwa Mkoa wa 20 katika kupasisha watoto kwenda *secondary schools*. Tatizo kubwa ni uhaba wa Walimu, utawapanga vipi Walimu 9 kati ya Walimu 21, utawapanga vipi Walimu 7 katika ya Walimu 17 na 18? Naomba sana suala la upungufu wa Walimu lizingatiwe ili na sisi tuondokane na aibu hii ya kunaonekana ni Mkoa wa mwisho nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utawala Bora ni pamoja na kuwa na maeneo ya Vijiji, Kata na Tarafa zenye uwiano mzuri. Jimbo langu ni kubwa mno, *three in one,* Kata ni kubwa mno na Tarafa ni kubwa mno. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri anayehusika, tayari tumekwishapeleka mapendekezo *Full Council* imekwishapitisha. Ni ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri wetu huyu kwa kweli Kata zigawiwe, vijiji vigawiwe, Kata moja kwa mfano, unakuta ina vijiji 12 au 13, wakati Kata nyingine katika maeneo mengine unakuta Kata ina vijiji vinne au vitatu. Kwa nini sisi tuna Kata moja ina vijiji 13 au 14? Mimi ningeomba sana hilo liangaliwe ili vijiji vigawiwe, Kata zigawiwe pamoja na Tarafa licha ya habari ya kugawa Wilaya.

Ukichukua Wilaya ya Singida Mjini na Wilaya ya Singida Vijijini hizo ni Wilaya mbili, tatizo inaonekana kama ni Wilaya moja. Wilaya nayo igawiwe, jimbo langu ni kubwa mno, ninapakana kule Tabora na Mama yangu Mheshimiwa Tatu Ntimizi na vile vile Kondoa, jimbo ni kubwa mno, kwa hiyo naomba nalo liangaliwe. Lakini kwa kweli Vijiji, Kata na Tarafa naomba sana viangaliwe. Tarafa kama ya Sepuka, Kata ya Sepuka, Tarafa ya Ihanja, Tarafa ya Muungaa, Kata ya Puma, maeneo yote hayo naomba yaangaliwe ili yagawiwe na Utawala Bora ndipo utakapoonekana vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inafanya jitihada kubwa sana za kuboresha maisha ya wananchi walioko vijijini. Naipongeza na ninaishukuru sana. Lakini ukweli vile vile ambao hauna ubishi ni kwamba, bado hali za wananchi wetu vijijini ni duni. Tathmini ambayo inafanywa inaonyesha maisha ni magumu kule vijijini. Umaskini umekithiri kule vijijini. Huduma za jamii ni duni kule vijijini ukilinganisha na mijini ambapo hali ya umaskini ni nafuu, huduma kama maji, afya, elimu, barabara na kadhalika ni zinaridhisha ukilinganisha na sisi. Sasa hivi hawa wananchi wa vijijini wana makosa gani? Hawa ni wazalishaji wakuu, wanaipatia nchi hii *foreign exchange* ya kutosha mpaka sasa tunaelekea kutamba, tuna *foreign reserve* ya *foreign exchange* ya zaidi ya miezi sita, lakini manufaa tunapata sisi tunaokaa mjini. Ninaiomba Serikali iliangalie kwa dhati, kwa sababu tayari wananchi wa vijijini wameanza kulalamika, imeonekana kama kuna tabaka mbili hapa. Wale waliopewa wapewe, inakuja mambo aliyoyasema Waziri wa Fedha ya Biblia kwamba, wale walionacho waongezewe na wale wasionacho wanyang'anywe wapewe wale ambao wanacho. Sasa hii sio nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba kwa kweli pawepo na *serious efforts* za kuona kwamba, maisha ya wananchi wetu vijijini yanaboreshwa. Tunalalamika vijana wanakimbilia mijini, watokosaje kukimbilia mijini wakati kule vijijini hali ni ngumu? Mambo yote mazuri, umeme upo mijini, barabara zote nzuri ziko mijini, ukitaka elimu nzuri nenda mijini, ukitaka maji kwa uhakika nena mijini, ili mradi kila kitu kinapatikana mijini. Anasema Mheshimiwa mwingine hapa kwamba, ukitaka pilau, biriani nenda mijini. Hayo mimi sijasema. Lakini nasema ili mradi kila kitu unachokitaka kizuri kiwe mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu ni kwamba, Serikali iangalie kwa dhati kabisa hii habari ya kuwajali zaidi watu wa mjini ambayo linasikitisha, lakini uwezeshaji duni wa wananchi wa vijijini. Mabenki yako mijini, wanaofaidi mikopo ni watu wa mijini. Tulitegemea kwamba, *NMB* itakuwa benki ya walala hoi au ya watu wa hali ya chini ili iwakopeshe wananchi walioko vijijini. *NMB* nayo haiwakopeshi wananchi waliopo vijijini, inawakopesha wananchi walioko mijini. *Pride* ni nzuri, imesifiwa hapa lakini iko mijini. Sasa hivi watu wa vijijini atawawezesha nani kama mabenki yoteyako mjini na *NGOs* mbalimbali zipo mjini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo haja ya kuwaangalia hawa wananchi wa vijijini ili wasije wakafika mahali wakaona kwamba wametengwa, wakati wao ndiyo wazalishaji wakubwa na wakati wao ndiyo wanatusaidia kupata *foreign exchange* nyingi, lakini wanaotumia ni watu wa mjini kwani wanaangalia TV, wanaangalia kila kitu, maji bwerere yakikatika maji Dar es Salaam Waziri Mkuu halali, Rais halali, Waziri wa Maji ndiyo kabisa halali. Sasa hilo naomba liangaliwe sana lisije likatuletea matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningeomba kushauri mambo mawili. Moja, kwa kweli pawepo na mpango wa maendeleo vijijini, mpango maalum kama ilivyo MMEM kama ilivyo MMES. Uzingatie namna ya kufanikisha mambo haya vijijini. Pawe na maji na kila kitu, hili liwe ni mojawapo. Lakini pili, Wizara hii ya TAMISEMI inafanya kazi nzuri lakini naomba kushauri kuwa, Wizara ya TAMISEMI iangalie vilevile maendeleo ya vijijini. Kwa mfano, tuna Wizara ya Ardhi, na Maendeleo ya Makazi, sasa maendeleo vijijini yako wapi? Unaona kabisa hapa kuna upungufu ambao unaonekana wazi hapa, hakuna mtu ambaye anaangalia maendeleo ya vijijini kuna maendeleo ya mijini tu. Hakuna maendeleo ya vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, angalau TAMISEMI wangeitwa Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Maendeleo Vijijini. Sasa ni kazi ya Rais kupanga Wizara hizi. Lakini pia sisi kama Washauri Wakuu, napenda nimshauri Mheshimiwa Rais na Serikali kwa ujumla, kuanzisha Wizara itakayoangalia maendeleo ya wananchi wetu huko vijijini vinginevyo kutakuwa na tabaka kati ya watu wa mijini na watu wa vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suluhisho lingekuwa ni ushirika ili kutatua matatizo ya watu wa vijijini. Napenda nikiri kabisa hapa pamoja na kumheshimu sana Waziri wa Ushirika na Masoko na rafiki yangu Naibu Waziri wa Ushirika na Masoko, lakini bado *impact* ya Ushirika Vijijini haijaonekana. Bado haijaonekana hasa Singida bado katika

Halmashauri ya Wilaya yangu wako Maafisa Ushirika wawili. Jimbo kubwa kama lile watakwenda vipi wakati wa kuhamasisha kuunda Ushirika. Mimi nilichukua wataalam kutoka Wizarani, ninamshukuru Mheshimiwa Waziri alinipa, nimetembea nao, nimehamasisha na hawa watu, sasa watu wanangojea kuanzishwa kwa Vyama vya Ushirika hakuna. Nani ataanzisha, Maafisa wawili katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida hawatoshi.

Kwa hiyo, *impact* ya Wizara ya Ushirika na Masoko na sababu za kuundwa kwa Wizara vya Ushirika mimi nasema bado haijaonekana.

Ningemwomba Mheshimiwa Waziri, pamoja na kumheshimu na Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kwa kweli wafanye jitihada wawe na Programu Maalum ya kuweza kuanzisha Vyama vya Ushirika pamoja na *SACCOS* ili kuona kwamba, wananchi ambao hawawezi kukopa kwenye mabenki, hawakopi *NMB*, hawakopi sehemu nyingine, angalau wanakwenda kwenye Chama cha Ushirika wanakopa na wanapata fedha za kuwasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 13 unazungumzia habari ya Miji Midogo. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, azingatie maamuzi ya Miji Midogo. Ikungi inastahili kuwa Mji Mdogo, Puma inastahili kuwa Mji Mdogo, Makyungu inasthaili kuwa Mji Mdogo, Ihanja na Sepuka nazo zinastahili kuwa Miji Midogo ingawa wako mbioni kupatiwa umeme. Lakini maandalizi yakianza si vibaya. Nikuombe sana uangalie na Singida ndugu yangu. Karibu kule Singida, lakini ukipita pale Ikungi utaona hali ilivyo, ukipita Puma pale utaona hali ilivyo. Njoo Makyungu, *facilities* zote na vigezo vyote ambavyo vinatakiwa kuwa Mji Mdogo vipo. Kwa hiyo, karibu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ajira ya Watendaji. Kwanza, ninashukuru kwa kuahirisha lile zoezi, maana yake lilileta vurugu na mkanganyiko mkubwa. Kule kijijini kumpeleka mtu ambaye ame-*graduate* ana digrii, mimi sijui kama atakaa kule, vinginevyo unamwajiri mtu unampa mshahara lakini kwa kweli hatakuwa *productive.* Ninasema kwamba, ajira mpya ambazo zinakuja sasa kwa wale Watendaji wetu wa Vijiji zizingatie uzoefu na uadilifu zaidi kuliko hayo mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika hotuba hii. Ningependa nichukue nafasi hii kuwapa pole wenzetu, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kumpoteza baba yao na kuipa pole familia ya Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, kwa kufiwa na binti yao mpendwa, pamoja na kuwapa pole wenzetu waliopata majanga ya kuvamiwa na wezi, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela na Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere aliyepata ajali mbaya. Namwombea Mwenyezi Mungu, ampe nafuu mapema na Mheshimiwa Estherina Kilasi aliyepata ajali. Naomba Mwenyezi Mungu awafariji na awatie nguvu ya kuweza kusahau yaliyowapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nichukue nafasi hii pia kukipongeza Chama Cha Mapinduzi, kwa njia ya pekee kwa kuweza kupata ushindi wa kishindo katika chaguzi ndogo zilizofanyika katika Mikoa ya Kilimanjaro na katika Wilaya ya Bariadi. Kwa njia ya pekee ninampongeza sana Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kuweza kufikia azma yake ya ndoto zake ambazo alikuwa anaota kumtafuta baba mwenye hekima, baba mwenye amani na baba mwenye mapenzi na watoto wake, ambaye ni Chama Cha Mapinduzi. Ninamwambia karibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa pongezi hizo, ningependa pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Brigadia Mstaafu Hassan Ngwilizi, pamoja na Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu wake na Wataalam wake kwa kutengeneza hotuba nzuri na pia kwa kutekeleza majukumu yao vizuri kama inavyoeleza hii ripoti ya kipindi cha mwaka 2003/2004 na kwa kutengeneza mikakati mizuri ya kutekeleza Sera na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa kipindi cha mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri waliyofanya, ningependa nichangie katika maeneo machache kwa nia ya kuboresha. Tatizo langu kubwa kabisa leo ningependa nimwambie Mheshimiwa Waziri kwamba, Wanawake na Wananchi wa Morogoro Vijijini wamenituma nije nimweleze kwamba, wangependa nao kupata Hospitali ya Wilaya. Kwa nini wananchi wa Morogoro Vijijini wanaomba Hospitali ya Wilaya? Hawa wananchi wanaishi mbali sana kutoka mjini na *logistic* ya kufika mjini kupata matibabu ya kitaalam inakuwa ni matatizo. Wananchi wa Dutumi, Kisaki, wananchi kuteremka kutoka milimani Kibungo Juu, Kibungo Chini pamoja na wengine kutoka Kinole, wanatokea Matombo, wanapokuwa na matatizo ya akina mama wajawazito, mama mja mzito ambaye amepata kile tunachokiita *obstracted labour* anabebwa kwenye machela, wateremke mpaka barabarani, waweze kupata gari la kwenda Morogoro Mjini, *by the time* wanafika Morogoro Mjini tunakuwa tunawapoteza hawa akina mama.

Nazungumza hivi kwa sababu hata mimi wakati nafanya *practice* hospitalini yalinikuta kwamba unaletewa mama ambaye amechoka, amesha-*rupture* kile kizazi halafu unapojaribu kumpasua kwenye harakati za kujaribu kumwokoa anafia mezani. Inafika mahali Madaktari wanakuwa *very frustrated,* wanashindwa kuwaeleza ndugu zao na inafika mahali pia wale wananchi kutoka katika haya maeneo wanafikiri kwamba, ukimpeleka mama mja mzito Hospitali ya Morogoro basi anakwenda kufa, ujitayarishe na sanda. Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, aangalie uwezekano wa kusaidia kujenga Hospitali ya Wilaya katika maeneo ya Matombo au Mvuha. Hili ni tatizo na ndiyo kilio cha akina mama na hasa Wananchi wa Morogoro Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nizungumzie kidogo tatizo la UKIMWI. UKIMWI ni tatizo na nafikiri imefikia mahali tunauita ni janga la UKIMWI. Sasa kama ni janga linakuwa pia ni maafa. Lakini ninasikitika kumweleza Mheshimiwa Waziri kwamba, watendaji wetu wengi katika miji yetu ya hapa Tanzania wamechangia sana katika ku-*facilitate* kuenea kwa maradhi ya UKIMWI. Aniulize kwa vipi? Nasema kwa sababu hawa wanakiuka Sheria za Mipango Miji. Wanawaruhusu watu wanaotaka

kufanya biashara za baa na watu wanaotaka kufanya biashara za *guest house* kununua nyumba za wanyonge katikati ya raia, wanazijenga. Wanafanya *guest house,* wanazifanya baa, mle wanachoma nyama, mle wanakaanga *chips,* mle wanapiga muziki. Sasa usalama wa vijana wanaozunguka maeneo haya uko wapi? Ninamwomba Mheshimiwa Waziri kama atapenda kuja kutembelea Morogoro, ninaomba aje Morogoro akatembelee Kata ya *Sultani Area*, Kata ya *Sultani Area* sasa hivi imejaa ma-*guest house,* imejaa mabaa, bila kuangalia maslahi ya watoto na wanawake ambao wanapenda kuishi kwa amani katika yale maeneo. Kila siku mimi ninakuwepo kwenye Kamati ya Mipango Miji, sijawahi kuona wanapitisha wapi sasa haya maombi yao ya kupewa vibali mpaka wanajenga hizi *guest house.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwauliza hawa Watendaji wa Idara ya Ardhi na Mipango Miji, wanafanyia wapi hivyo vikao, kama Kamati ya Madiwani inahusika na hiyo shughuli, hawaonyeshwi na hawajui?

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia kuzungumzia matumizi ya maeneo wazi katika miji mingi hususan Mji wa Morogoro. Naomba nieleze kwamba, vijana wengi sasa wanavuta bangi, vijana wengi wanazurura kwa sababu wanakosa burudani na hizi burudani sasa hata kama kungekuwepo na namna ya kuweza kuwatengenezea, watengenezewe wapi, kama viwanja vyote vya mpira, kama maeneo yote wazi yameshagawiwa viwanja, watu wameshajenga majengo makubwa makubwa. Hata tukiamua kwamba tuwabomolee hela za kuwalipa hatuna. Kwa sababu huyu mtu hakuvamia, huyu mtu amepewa barua, amepewa *offer* na *by the time* anapewa *offer* unakuta kwamba, ile *letter of offer* inakuwa tofauti na *Title Deed* ambayo anayo lakini naomba kusema kwamba, hii tabia chafu ya Watendaji kuanza kufanyia biashara ardhi ya wananchi ambayo imetengwa kwa ajili ya burudani ni tabia chafu. Naomba ikemewe na Serikali kwa nguvu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia kumweleza Mheshimiwa Waziri, ujumbe ambao wamenipa wananchi wa Kata ya Kilakala. Kata ya Kilakala ina maeneo ya milimani inaitwa Nogutu, Bong'ola, Visiga kule juu, kuna watoto wengi sana hawaendi shule na hawaendi shule kwa sababu shule hazitoshi. Sasa kwa nini shule hazitoshi? Hazitoshi kwa sababu kiwanja pekee ambacho Serikali ilikuwa imetenga eneo lile kwa sababu ya shule, Watendaji wa Manispaa kwa njia zisizoeleweka, walikigawa kwa Shirika moja la Dini linaloitwa *Islamic Foundation*. Wamejenga shule ambayo walitudanganya mwanzoni watasoma watoto wa itikadi zote, lakini sasa hivi hata mtoto wa Kiislamu ambaye hatavalishwa ushungi na ambaye baba yake hatafuga madevu hatasoma katika ile shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wale wanalalamika sana. Tunaomba Serikali iangalie mambo haya. Kama ni watendaji wanadanganya kwamba, wananchi wa Kilakala wanataka kuchukua kile kiwanja kwa ajili ya kujenga Shule ya Kikristo, ni uongo. Wananchi walishaanza kuchangisha pesa. Watoto wanazurura, watoto wanapata mimba, watoto wanakuwa chokoraa kwa sababu ya mtu mmoja tu ambaye ana pesa, ameidanganya Manispaa, amechukua kile kiwanja amejenga wanasoma watoto wasiozidi 45 *in place of thousands of children.* Haki iko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba hilo uliangalie kwa jicho la uzalendo na mapenzi kwa wananchi wa Kilakala. Pia ningependa kuzungumzia haki za Walimu. Wenzangu wamezungumzia mishahara, wamezungumzia malimbikizo mengine ya posho. Lakini naomba nizungumzie kwamba hawa Walimu wetu wamepangwa kwenda kwenye stesheni zao za kazi, anapewa barua ni mtoto wa mkulima au ni mtoto yatima, lakini haulizwi kwamba wewe nauli yako ya kwenda kule ulikopangwa kazi unayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa vijana hawana nauli ya kwenda mpaka kule walikopangwa. Mtu ambaye yuko Morogoro anapangwa kwenda Shinyanga. *You can immagine,* atahitaji *resources* kiasi gani aweze kuchukua treni kutoka Morogoro mpaka Shinyanga afike Shinyanga aanze kuitafuta shule hana nauli ya kwenda huko na hana namna yoyote ya kwenda kuanza maisha, hana kitanda, hana godoro hana shuka. Sasa huyu tunamtaka akafanye kazi kwa motisha ya namna gani? Tunaomba hawa vijana wanapopangwa kwenda kwenye kazi zao apewe nauli ya kumfikisha mpaka kule anakokwenda, apewe na hela za kuanza maisha aweze kununua basi angalau godoro la sufi anunue na shuka la mtumba, aweze kuanza maisha. Sasa utakuwa unapikia kwenye kiganja, hata kama atakipata hicho chakula ambacho sijui kama atakipata, hapikii kwenye kiganja, anahitaji kununua angalau sufuria, anahitaji kuwa na kikombe cha kunywea chai, lakini hawa watoto wanakwenda wanakuwa kama ombaomba halafu tunasema kwamba, tunawataka wafundishe watoto wengine kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hili liangaliwe na tuambiwe kabisa katika bajeti hii kwamba ni nani atakayeshughulika kuhakikisha kwamba, hawa vijana wanapewa nauli na fedha za kuanzia maisha. Ningependa pia kuzungumzia tatizo la barabara. Kuna tatizo la barabara katika Wilaya ya Morogoro Mjini, barabara za Mjini zinakuwa chafu na mbaya kuliko barabara za vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo linakuja pale ambako Wakandarasi wa kutengeneza hizo barabara wanakuwa wanateuliwa na Watendaji. Kwa hiyo, sisi kama Madiwani, kama Wabunge, tunastukia wakiwa wanatengeneza. Sasa suala linakuja unakuta barabara imetengenezwa kama tuta. Tuta tu limetengenezwa anakuja anamwaga kifusi, anatengeneza tuta, anaondoka. Sana sana pale ambako anaweka kalvati la maji machafu limeelekea kwenye *Feeder Road* ambako inaelekea nyumbani kwa wakazi wa eneo lile?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mfano kuna barabara iliyojengwa katika eneo la Kilakala, kuna makalvati kama matatu ambayo yamewekwa yameua *feeder roads* ambazo zinakwenda kwenye nyumba za familia zaidi ya 50. Hao ndio *engineers* wetu, ambao tunawapa majukumu na madaraka ya kuweza kuwateua makandarasi. Makandarasi wengine unamkuta kwamba ni mtu mwenye meza yake sokoni lakini ana *register* ya *construction company* kwa kutumia *certificate* ya *engineer.* Lakini yule *engineer* yupo Dar es Salaam anakuja tu siku ambayo wanazungumzia hizo tenda. Naona hili liangaliwe kwa sababu ni jasho la wananchi linatumika kutengeneza hizi barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuzungumzia pia shule. Ni vizuri tumejenga shule nzuri, lakini unakuta maeneo mengi hizi shule hazina walinzi na unakuta hela inayotolewa ya *capitation* haitoshi kumlipa mlinzi, kulipa *bill* ya maji, kulipa *bill* ya umeme, kulipa *bill* ya simu, pamoja na kufanya zile shughuli za kila siku za kuendesha ofisi ya Mwalimu Mkuu na kufanya mazingira ya kazi yawe mazuri. Ninaomba Wizara hii iangalie namna ambavyo inaweza ikatoa angalau mshahara mmoja tu kwa ajili ya Walinzi. Nitoe mfano wa Shule ya Kilakala ni ya zamani sana. Kuna Kitengo cha Viziwi. Kile kitengo kimepewa vyombo vya kufundishia wale watoto vinavyozidi shilingi milioni 50.

Lakini vile vitu vimo mle shuleni hakuna mlinzi, wamekuja wameiba na zile *ear phones* wakifikiri kwamba ni *ear phones* kwa ajili ya muziki. Unazikuta zinauzwa sokoni na mjini. Sasa hata wale wafadhili wanakata tamaa wanasema *are you serious* tunawasaidia kwa ajili ya watoto wenu walemavu. Sasa ninyi mnashindwa kuweka mlinzi. Sasa tukisema tuwaambie hawa wazazi wachangie, kuna wakati tuliitisha kikao tukaomba wachangie Sh. 50/= tu, mwingine akasema mama mimi hata chai ya asubuhi sijanywa, sasa Sh. 50/= nitaipata wapi, hata mguuni hajavaa kiatu, amevaa kanda mbili za rangi mbili na amezifunga na kamba. Sasa mimi kwa sababu Serikali hii ya Awamu ya Tatu imeamua kuwapunguzia wazazi mzigo katika shule za msingi, ninaomba hilo liangaliwe.

Mwisho, ni mpango huu unaoitwa MEMKWA. MEMKWA itasaidia sana kuondoa vijana wanaozurura mitaani, itasaidia sana kuondoa ujinga miongoni mwa vijana wetu kwa sababu mjinga ni mtu anayeweza kutumiwa kufanya fujo bila kuwa na *reasoning capacity*. Kuna *NGOs* ambazo zimeanzisha mpango huo tangu mwaka 1998 na *NGOs* ya Faraja ndio ya kwanza katika Mkoa wa Morogoro. Tumeweza kutoa watoto zaidi ya 10 kwenda *Secondary School* kupitia hiyo shule yetu ya MEMKWA na mmoja amekwenda *special school* ya Mzumbe. Ninachosema ni hivi, kama *NGOs* zimejitokeza Serikali ifanye kazi *in partnership* na hizi *NGOs* kwa kuzipa ruzuku au kwa kupeleka Walimu *on secondment basis* ili kuwapa moyo na kupanua huduma zile kwa sababu kila mtoto ana haki ya kusoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema kwamba, namtakia Mheshimiwa Waziri, kazi njema na napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuanza mchango wangu, naomba nitoe pole kwa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na dada yake, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na baba yao. Namwomba Mwenyezi Mungu, aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi, *amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nichukue nafasi hii nimpe pole Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, kwa kufiwa na mwanawe. Namwomba Mwenyezi Mungu, aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi, *amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapa pole Waheshimiwa Wabunge wote, ambao wamepata ajali mbalimbali akiwemo Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, ambaye alivamiwa na majambazi, Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere na Mheshimiwa Estherine Kilasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii, nimpongeze ndugu yetu, Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kuchaguliwa tena kuwa Mbunge wa Bariadi Mashariki. Ushindi wa Mheshimiwa Danhi Makanga ni mtamu na wa aina yake kwa sababu amemwangusha Mwenyekiti wa Taifa wa *UDP* maarufu kama "Bwana Mapesa" tena baada ya kuungwa mkono na nguvu zote za Upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ninapenda nitumie nafasi hii nimpongeze Mheshimiwa John Samwel Malecela, Makamu Mwenyekiti wa CCM, Tanzania Bara, kwa kuhakikisha CCM inapata ushindi wa kishindo huko Bariadi. Juhudi za Mheshimiwa John Samwel Malecela ni kubwa mno hadi kupelekea kigogo mmoja wa Upinzani kukiri hadharani kuwa kweli Mheshimiwa John Samwel Malecela hawezekani katika kampeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nieleze tu kwa ushindi mkubwa wa Chama cha Mapinduzi huko Bariadi hizo ni mvua za rasharasha masika yenyewe wasubiri mwaka 2005. Wale wote ambao wanaogopa kunyeshewa mvua hizo, naomba watafute hifadhi ndani ya Chama cha Mapinduzi kwa sababu milango iko wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nitumie nafasi hii nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa hotuba yake nzuri. Hali kadhalika nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kumsaidia sana Waziri katika kuiendesha Wizara hii vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nitumie nafasi hii kuwapongeza wafanyakazi wote wa Wizara hii wakiongozwa na Katibu Mkuu, kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya ya kuhudumia wananchi, Wilayani hadi Vijijini. Mafanikio tunayoyaona sasa hivi huko vijijini ni ishara kuwa Wizara hii imeshiriki kikamilifu kwa sababu ndio Wizara yenye mtandao wa watendaji kuanzia ngazi ya Taifa, Mikoa, Wilayani na vijijini. Mafanikio hayo ni ishara kuwa Wizara hii inafanya kazi yake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Wizara hii iweze kufanya kazi zake vizuri, kila wakati imekuwa inagawa maeneo makubwa ili yawe madogo ambayo yanaweza kufuatiliwa kwa makini zaidi ingawa safari hii Mheshimiwa Waziri ametamka wazi kwamba, wameshindwa kugawa yale maeneo ambayo ni makubwa kwa sababu gharama ni kubwa. Mimi binafsi ningefurahi zaidi kama maeneo yale ambayo ni makubwa kiutawala yangegawanywa katika maeneo madogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu zilizotolewa naona hazina uzito kuliko zile sababu za kuhakikisha kuwa maeneo haya yanatawalika vizuri na yanapata maendeleo ambayo yanahitajika. Naomba Serikali ifikirie upya uamuzi huo wa kutogawa maeneo yale ambayo yanaonekana makubwa sana kiutawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nizungumzie suala la vijiji kupewa hati. Suala hili ni la siku nyingi na nakumbuka huko nyuma nimezungumzia sana kuhusu vijiji vyangu kadhaa vilivyopo kwenye Jimbo langu ambavyo tangu wapeleke maombi ya kupatiwa hati ni miaka mingi imepita hawajapewa, tatizo ni nini? Wakati naiuliza Wizara walisema walikuwa hawajapata maombi toka Wilayani lakini tuliporudi Wilayani wanasema maombi yamepelekwa Wizarani, leo Mheshimiwa Waziri amekiri kuwa maombi yaliyopokelewa ni mengi, sasa yanachambuliwa, yanahakikiwa ili vijiji viweze kupatiwa hati na ametuambia kuwa watahakikisha kuwa kazi hiyo inakamilika kabla ya Agosti, 2004. Naomba basi vile vijiji ambavyo niliomba vipatiwe hati na ambapo maombi yalikwishatumwa vipatiwe hati. Vijiji hivyo ni kama Mtawatawa, Kazamoyo, Mchenjeuka, Changwale, Mkoromwana na Wawaje. Naomba sana Mheshimiwa Waziri vijiji hivi vipatiwe usajili wa kudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ninataka nilizungumzie ni kuhusu barabara. Kwa kweli barabara za vijijini ni muhimu sana katika kusukuma maendeleo ya vijiji, naomba ile kasi ya utengenezaji iongezwe. Barabara nyingi zinatengenezwa baada ya miaka mingi kupita hivyo huwa sawa kabisa na kujenga upya barabara lakini kama matengenezo yangekuwa yanafanywa mara kwa mara, nina hakika gharama ambayo ingetumika ingekuwa ndogo zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ninapenda niliongelea ni kuhusu Maafisa Watendaji wa Vijiji. Ni kweli Serikali baada ya kupata maombi mbalimbali ilitoa tamko kwamba, wale Watendaji wa Vijiji wote waendelee na kazi zao kwa kipindi cha miaka mitatu. Lakini uamuzi huu ulitolewa wakati baadhi ya Wilaya zilikwishateua Watendaji wapya wa Vijiji. Inasemekana kuwa wale walioteuliwa wengine waliteuliwa kwa kupitia mlango wa nyuma. Sasa watendaji wa zamani wana wasiwasi kuwa inaweza hii ikawa njia ya kuwalaghai lakini nafasi hizo zina wenyewe. Kwa hiyo, wanafanyakazi kwa wasiwasi na kwa kweli wale ambao hawajiamini, wanadhani kuwa hawawezi kufika miaka hiyo mitatu bila kuondolewa kwa mizengwe na kwa sababu ambazo sio za msingi. Ninaomba Serikali itamke wazi kuwa Watendaji wa Vijiji wa zamani ambao wanaendelea na kazi wataendelea na kazi hiyo hadi miaka mitatu ipite na katika kipindi hicho watendaji hao wasaidiwe kujiendeleza maana imeelezwa wanatakiwa wajiendeleze lakini ukweli ni kwamba, wao wenyewe hawana uwezo wa kujiendeleza. Kinachotakiwa ni Serikali kuwaendeleza Watendaji hawa ili waweze kupata sifa zinazotakiwa. *(Makofi)*

Baada ya kusema haya, naomba nimalizie kwenye suala la Kituo cha Afya cha Mangaka. Kwa kweli kituo hiki kimemalizika kujengwa au kina majengo ya kutosha kuanza kutoa huduma. Tangu kipate majengo ya kutosha mpaka leo inakaribia miaka miwili hakijaanza kutoa huduma kama Kituo cha Afya kinavyotakiwa. Naomba Serikali ihakikishe kuwa, Kituo cha Afya cha Mangaka ambacho ni kikubwa na kinategemewa na watu wengi katika Jimbo langu, kinaanza kazi mara moja. Cha msingi ni kupeleka

wataalam na vifaa vinavyotakiwa ili kianze kufanya kazi. Kwa hivi sasa kituo kile kinafanya kazi kama zahanati, sina uhakika kwa nini tulitumia pesa nyingi kujenga majengo mazuri halafu baadaye tuifanye zahanati. Naomba Serikali ihakikishe Kituo hiki cha Afya mwaka huu au kwenye bajeti hii kinapewa pesa za kutosha ili kianze kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naomba nirudie tena kusema kuwa, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa asilimia 100. Vile vile ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kunisikiliza, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kutoa pole sana kwa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na dada yake, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa msiba mkubwa wa mzee wetu uliouwakumba na tunamwomba Mwenyezi Mungu, ailaze roho yake mahali pema peponi, *amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika nimpe pole sana Mheshimiwa Parmukh Hoogan Singh, kwa kufiwa na binti yake, tunaomba Mungu ampe moyo wa kujua kwamba kila mtu ana muda na nafasi yake ya kuaga dunia hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe pole kwa Waheshimiwa Wabunge mbalimbali, ambao wamekumbwa na matukio mbalimbali yaliyowaathiri kwa njia moja au nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nimpongeze Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote, kwa kutuletea bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nimpongeze Naibu Waziri wa Wizara hii, Mheshimiwa Mizengo Pinda. Kama walivyosema Wabunge wenzangu wengi, kwa kweli Mheshimiwa Mizengo Pinda amekuwa mtu wa kutoa ushirikiano mkubwa kwa Wabunge wote na hata Jimbo langu la Hai amelitembelea na ni mmojawapo wa Mawaziri waliotembelea Jimbo langu na kutoa ushirikiano bila ya kuwa na ubaguzi wa aina yoyote, ninampongeza sana . *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda na leo nimpongeze Waziri Mkuu, nimpongeze kwa kitu kimoja cha msingi alichokifanya jana. Leo nilikuwa nimepania kabisa nitazungumza kwa hasira sana kuhusu Walimu lakini nakiri Waziri Mkuu jana alini-*pre-empty. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri Mkuu alitoa agizo ambalo mimi naweza kusema lilikuwa ni *bold* na *authoritative*. Tunamtaka Mheshimiwa Waziri Mkuu, pongezi tunazompa leo ahakikishe sasa kero za Walimu zinakwisha na sio utaratibu wa kurudia kila mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema ikaeleweka kwamba, hizi kero za Walimu ambazo zimelalamikiwa sana na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali ndani ya Bunge hili

hususan katika Kikao hiki cha Bajeti zimefumuka na kupanuka zaidi baada ya Mpango mzima wa Kuboresha Elimu ya Msingi. Hizi kero zitaendelea kuwepo kwa sababu bado Walimu wanaajiriwa kwa wingi na wanaendelea kuhamishwa kwenda maeneo mbalimbali. Kuna masuala mengi ambayo ni ya kiutendaji ambayo tunaiomba Wizara inayohusika, kwa kushirikiana na TAMISEMI, iweke utaratibu ambao utahakikisha kwamba, Mpango mzima wa Kuboresha Elimu ya Msingi na sasa kwenda katika Kuboresha Elimu ya Sekondari, inawekewa mipango ambayo inasimamiwa na kutekelezeka kuliko kila wakati kuja kungoja tamko la Waziri Mkuu kufanya maamuzi katika upande wa dharura kama ilivyokuwa jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nizungumzie Jimbo langu la Hai. Katika Jimbo langu la Hai tuna hali mbaya na labda niseme katika Wilaya nzima ya Hai, mimi na *homeboy* wangu hapa, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, tunapokuwa tunazungumzia masuala ya Hai tunazungumzia masuala ya Hai kama Wilaya na sio kama Jimbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwetu Hai, ninaomba nitangaze rasmi kuwa, hali ya chakula kwa mwaka huu ni mbaya sana. Tumepata hasara kubwa kwa sababu hali ya mvua imekuwa mbaya, mvua imepatikana kwa siku 20 katika mwaka huu mzima kati ya siku 46 ambazo zilitegemewa. Wilaya yetu ina wakazi takriban 259,000, kati ya hawa wananchi 132,000 hawatakuwa na mavuno yoyote ya chakula. Kati ya hawa watu 132,000 watu 64,000 hawatakuwa na uwezo wa aina yoyote wa kununua chakula. Tunaomba hili Mheshimiwa Waziri na Serikali ilichukulie kama ombi maalum la kujua mapema kabisa kwamba, hali ya wananchi wa Wilaya yetu yaHai ni mbaya. Shule nyingi ambazo zinategemea nafaka kutoka kwa wazazi, watoto wanashindwa kwenda shule kwa sababu hakuna chakula. Serikali ilitupa msaada wa tani 100 za chakula ambazo kwa kweli hazikutosheleza hata kidogo kutokana na mahitaji ya wananchi kuwa makubwa sana. Naomba kwa kipekee kabisa, Serikali ilione hili kwamba hali ya Wilaya ya Hai, Jimbo la Siha na Hai yenyewe kuna upungufu mkubwa sana wa chakula na wananchi walipata hasara kubwa sana kwa sababu asilimia 60 ya mahindi katika Wilaya nzima pamoja na maharagwe yalikauka kwa sababu ya kukosa mvua, hapo ni baada ya wananchi kununua mbolea kwa gharama kubwa sana ya Sh.20,000 ambayo kwa kweli iliongeza sana gharama za uzalishaji na bado juu ya hapo tukakosa chakula kutokana na kukosa mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la chaguzi za Serikali za Mitaa ambazo baadaye mwaka huu zitakuja. Ni vema sisi kama viongozi wa watu, viongozi wa siasa, tunapokuwa tunafanya maamuzi tusiwe tunaangalia maamuzi ambayo yanatuathiri leo tuangalie maamuzi na *repercussion* zake katika siku za usoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku za karibuni viongozi mbalimbali wa Vyama vya Siasa walikaa wakazungumza, wakaona kuna umuhimu wa kutoingiza siasa katika ngazi za vijiji. Masuala ya siasa yakiingizwa sana katika misingi ya maendeleo ambayo ni kwa wananchi vijijini ni rahisi sana kuwagawa wananchi katika makundi na hapo mipango mbalimbali ya maendeleo inashindikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kikao cha viongozi wale ambacho vile vile kilijumuisha viongozi kutoka Chama cha Mapinduzi, kiliona kuna umuhimu wa pengine kutoingiza siasa katika chaguzi na kilitoa mapendekezo kwamba pengine chaguzi za kuhusisha Vyama vya Siasa zianzie ngazi ya Madiwani kwenda juu. Tunasikitika kwamba, Serikali haikuona umuhimu wa hili na pengine ni kwa sababu labda leo vijiji vingi katika nchi yetu vinaongozwa na Chama cha Mapinduzi, lakini siku itakapotokea vijiji vingi vikaongozwa na Vyama vingine kukawa na fukuto la siasa katika ngazi ya vijiji, maendeleo ya wananchi yatakuwa katika wakati mgumu sana. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Haitokei.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni utaratibu tu wa kawaida kwamba, watu wanapenda kuvutia kwao lakini ukweli unabaki kwamba tuna matukio mengine ya kisiasa ambayo yanadhihirisha kabisa wananchi kutengana, hii sio *healthy.* Tunaona mfano wa Karatu, Kigoma Ujiji, tunaona jinsi mahali ambapo Upinzani unakuwa na nguvu panapoanza kutokea matatizo ya kiutawala na kiutendaji. Sasa haya ni matukio ambayo lazima yatufundishe na baada ya kutufundisha yatuandae katika kufanya maamuzi ya siku za usoni tusibweteke kwamba hali itabaki hivi milele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoka hapo, nizungumzie suala la Watendaji wa Vijiji. Masuala ya vijiji ni masuala ya msingi sana kwa sababu naamini kabisa kule ndiko wanakoishi Watanzania maskini zaidi na kule kama hakuna Utawala Bora basi ni tatizo kubwa. Chimbuko la maendeleo ya nchi hii hata Rais Mkapa, Waziri Mkuu, Serikali yake ikipiga kelele kiasi gani, ama ikifanya juhudi kiasi gani, kama Utawala Bora hautakwenda mpaka kwenye ngazi ya kijiji na ukawepo usimamizi wa haki katika maamuzi ya wananchi, bado tatizo la maendeleo ni kubwa. Kwa misingi hii, sasa naomba nizungumzie suala la umuhimu wa nafasi ya *VEO.* Kwa nia njema Serikali ilikusudia itoe vigezo na sifa za watu ambao wanaweza kuwa *VEOs* katika maeneo mbalimbali ya vijiji vyetu. Bahati mbaya na ilikuwa pengine ni ushuhuda kwa Serikali kwamba, wananchi wake wengi elimu hawana, kile kigezo cha kuweka Elimu ya Kidato cha Nne pamoja na nia njema ambayo ilikuwa imechukuliwa katika ujumbe ule katika maeneo mengi ya nchi ilishindikana na hapo Serikali ikatoa tamko kwamba, wale Watendaji waliopo ambao hawana sifa zile waendelee kwa kipindi kingine cha miaka mitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalolizungumza hapa ni moja kwamba, kuna baadhi ya Wilaya ambazo zina Watendaji wenye sifa hizi kwa hiyo ni vema sasa Wizara yetu ya TAMISEMI ikaangalia uwezekano Wilaya ambazo zina Watendaji wenye sifa hizi waruhusiwe kuajiri Watendaji. Lakini mimi ninapenda ku-*declare* hapa kwamba, Wilaya yangu ya Hai ina watu wenye sifa za Kidato cha Nne na hata Kidato cha Sita wengi sana kwa hiyo turuhusiwe tuajiri ili tuweze kuongeza kasi ya maendeleo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie suala la Madiwani. Kama hatukuwa waangalifu dhana nzima ya Utawala wa Serikali za Mitaa tutaiua. Mgawanyo wa mamlaka na madaraka kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ni jambo ambalo sasa tunapaswa kuliangalia kwa makini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanasema siku yoyote ukitaka kumnyima au kumtawala mtu kwanza mnyime uwezo wa kifedha, mfanye awe ombaomba. Leo tunachokifanya katika nchi yetu tunafanya Halmashauri zetu zinakuwa ombaomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na nia njema ya Serikali Kuu kuondoa mzigo kwa Halmashauri, tunataka isiue uwezo wa Halmashauri wa kubuni na kufikiria vyanzo vyake vya mapato na pale Serikali Kuu inapoona inataka kuisaidia mzigo fulani Halmashauri, wafanye mawasiliano mapema na Halmashauri zetu hizi ili nao wenzetu wajiandae. Kufanya maamuzi ya ghafla kila siku wakati wenzetu tayari wameshatayarisha bajeti zao, kunawaathiri kwa kiwango kikubwa sana.

Kwa mfano, Halmashauri yangu ya Wilaya ya Hai mwaka huu ilikuwa inategemea mapato ya zaidi shilingi milioni 54 kutoka kwenye kodi mbalimbali kutokana na leseni za biashara, sasa kile chanzo cha mapato kimefutwa ni kwa nia njema ya kuwasaidia wananchi lakini tunafanya utaratibu ule uwasumbue Watendaji wetu wa Halmashauri wakiwepo Madiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni hili la kuwanyima Madiwani nafasi za kushiriki katika tenda. Sidhani kama katika Wilaya kuna mtu muhimu kama mwakilishi wa wananchi kuliko Diwani. Hata Mkurugenzi wa Halmashauri hawezi kuwa na mamlaka juu ya Diwani. Sasa mnapowanyima Madiwani wasihusike katika kugawa au kusimamia tenda mnawapa Watendaji, mnategemea nini? Huku ni kuondoa nguvu ya Madiwani na kwa kweli tunataka Serikali ibadilishe uamuzi huu mara moja, Madiwani wapewe nafasi ya kuwasimamia watu wao waliowachagua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Madiwani wetu wanaishi maisha magumu sana, Madiwani wanapata posho nafikiri ni Sh.30,000/=. Kwa kweli hatutegemei wale watu waweze kusimamia kazi za maendeleo hasa tukiangalia kiwango cha pesa kinachopelekwa kwenye Halmashauri zetu kwa ajili ya shughuli za maendeleo, kuwalipa Madiwani Sh.30,000/= ni kuwanyima haki hawa wananchi. Madiwani wana kazi nyingi za kusimamia uongozi, Madiwani hawapewi nafasi. Kama Serikali iliona umuhimu wa kuwapa Makatibu Tarafa vitendea kazi, mimi nasema Madiwani wana kazi kubwa kuliko Makatibu Tarafa.

**MBUNGE FULANI:** Kweli.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Makatibu Tarafa zaidi ya kuwa Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Wilaya, hawana kazi, Madiwani wana kazi kubwa na nzito kuliko Makatibu Tarafa. Kwa hiyo, ni vyema badala ya kuendelea kung'ang'ania mfumo wa Makatibu Tarafa tuwawezeshe na Madiwani wetu waweze kufanya kazi za maendeleo na kuzisimamia kama inavyostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ninajua muda utakuwa unagomba sana, vile vile niombe hizi Halmashauri zetu zinapopelekewa pesa zipewe na mamlaka ya kujipangia matumizi. Nimesema Serikali Kuu pamoja na nia njema ya kupeleka misaada

kwa wananchi, inapokuwa inapeleka misaada na masharti ya kutumia misaada ile moja kwa moja inakuwa inawakwaza wale wananchi wenyewe. Nitoe mfano wa *Basket Fund,* inakwenda kwa nia njema ya upande wa afya lakini vile vile ile *formula* ya mgao wa zile pesa inatoka Serikali Kuu matokeo yake kule wanaweza kuona mahali fulani panahitaji msaada kuliko pengine, hawana ruksa kubadilisha tena maagizo kutoka ngazi za juu. Kwa hiyo, tunaomba Halmashauri zikipelekewa pesa ziruhusiwe kuwa na uhuru wa kuzitumia pesa zile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoongea kuhusu *solidarity* yangu na Mheshimiwa Aggrey Mwanri hapa, kule kwake ana shule mbili za msingi shule moja inaitwa Wesendo na nyingine inaitwa Simba ziko katika eneo la Londrosi ambapo ni sehemu ya hifadhi ya mlima Kilimanjaro. Hizi shule mbili zina watoto zaidi ya 700 wanaosoma lakini ninavyokuambia leo ni shule zilizojengwa kwa mbao hata mpango mzima wa MMEM haukuweza kuwasaidia watoto hawa kwa sababu haikuwezekana kuwajengea madarasa ya kudumu kwa sababu lile eneo linasemekana ni eneo la hifadhi ya mlima wakati huo huo hawawezi kujenga majengo ya kudumu lakini ukweli unabaki kuwa wananchi bado wanaishi mle. Tunaiomba Serikali ambayo ndiyo hiyo hiyo inajua ni wananchi wake, ikubali kwamba sasa itoe kibali maalum katika eneo hili la hifadhi ya mlima ili watoto hawa zaidi ya 700 tuweze kuwajengea madarasa ili waweze kusoma watoto wengine Tanzania. Hili nalizungumza kwa sababu imekuwa ni kero ya muda mrefu na Serikali imeshindwa kutoa maamuzi. Serikali hiyo hiyo ambayo inashindwa kutoa maamuzi ndio hiyo hiyo inatutaka tujenge shule, jambo ambalo ni jema. Sasa Serikali itoe kibali maalum ili wanafunzi hawa 700 wa shule za Wesendo na Simba kule Londrosi, Jimbo la Siha, Wilayani Hai wapewe nafasi ya kusoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru mengine ni kwenye majukwaa huko huko. *(Makofi)*

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii. Pia, ningependa kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kutoa salaam za pole kwa Wabunge waliopatwa na misiba, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda na Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan na vile vile ninapenda kutoa pole kwa wenzetu waliopatwa na mikasa mbalimbali wakati wa kipindi cha Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ningependa kutoa pongezi kwa Waheshimiwa Wabunge, waliopata nafasi za uongozi katika mashirika mbalimbali ya ndani na nje ya nchi yetu bila kumsahau Mheshimiwa Danhi Makanga, aliyepata ushindi katika Jimbo la Bariadi Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kusahau ningependa kusema jambo moja ambalo nimeliona hapa nalo ni kumpongeza Mheshimiwa Freeman Mbowe, kwa kuchambua vizuri hotuba hii. Lazima nikubali kwamba, ni mara yangu ya kwanza kumwona akizungumzia mambo kwa hekima na kwa uchambuzi wa hali ya juu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mawazo mazuri katika nchi yetu siyo lazima yatoke CCM tu, yanaweza yakatoka popote pale na mambo mazuri lazima tuyathamini. Kwa hiyo, ninasema kutoka rohoni na kwa nia nzuri kwamba tofauti za sera katika nchi maskini kama za kwetu hakuna. Ni mikakati tu. Aliye nje atataka aseme maneno ili aingie lakini kwamba kuna tofauti hakuna, hata huko Ulaya ni hivyo hivyo. Kwa hiyo, ninasema nafurahi kuona jinsi alivyoonyesha kukomaa katika kuchambua mambo na kuthamini mchango wa Serikali katika mambo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa kuunga mkono hoja na kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tukubali kwamba, Wizara hii ni kubwa mno. Kitu gani cha Serikali hakipo chini ya Wizara hii; maji, mifugo, kilimo, kila kitu kipo chini ya Wizara hii. Wizara hii ndiyo Serikali yenyewe na ndiyo watu wenyewe. Hii ni Wizara kumbakumba. Ingawa hatuhusiki kuunda Serikali lakini nadhani ni vizuri Serikali ikatazama uwezekano wa kuongeza Manaibu Waziri kusudi wasaidie kuisimamia Wizara hii. Kwa mfano, suala la walimu pamoja na matatizo yote halikusema siyo kwa sababu wamesahau au kwamba hawajui, ila mambo ni mengi mno. Mambo ya Vijiji, mambo ya elimu, tunazungumzia mishahara na matatizo ya Walimu lakini nani anasimamia? Waziri wa Elimu, yeye anahusika na mambo ya taaluma lakini haya matatizo ya ujenzi wa madarasa, matatizo ya nyumba za Walimu, matatizo ya Walimu ni Wizara hii ingawa katika hotuba yake hakusema lolote juu ya matatizo ya Walimu. Nadhani hii ni dalili kwamba, hapa mahali panahitaji askari wengi zaidi wa aina ya Mheshimiwa Mizengo Pinda. Mheshimiwa Mizengo Pinda, ninampongeza sana, anafanya kazi nzuri na anastahili pongezi zetu sisi sote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, nia yangu ni kuchangia katika Ibara ya 7, 14, 20 na 22 za hotuba hii. Lakini kwa sababu muda hauruhusu labda nitoe mapendekezo ya ujumla kwanza kabla ya kuingia katika eneo hili. Moja, kutokana na ukubwa wa Wizara hii kama nilivyosema mwanzo, huenda ni vizuri Serikali ikaangalia uwezekano wa kuwa na Mawaziri Wasaidizi kwa upande wa Vijiji kwa sababu huko ndiko ambako asilimia themanini ya Watanzania wanaishi na huko ndiko hawa Walimu ambao ndiyo watumishi walio wengi zaidi kuliko watumishi wote katika nchi hii, wanakoishi. Sasa kwa eneo kama hili kuwa chini ya Naibu Waziri mmoja ni kazi ngumu na ndiyo maana baadhi ya maswali hapa anajibu Waziri wa Elimu na Utamaduni lakini hahusiki. Kama anahusika, anahusika kwa sababu yeye ndiye msimamizi wa taaluma. Ni vizuri tukachambua kwa undani kusudi tuisaidie Wizara hii ili iweze kumudu mambo yake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu ndio jeshi kubwa la watumishi katika nchi hii. Zaidi ya asilimia hamsini ya watumishi wa nchi hii ni Walimu, wanaishi huko Vijiji, katika kila Kijiji na katika kila Mji, lakini maisha yao na kazi yao ni ngumu sana. *These are the silent majority,* wako wengi lakini hawasikiki. Kwa hiyo, kujaribu kupuuza matatizo ya Walimu walio wengi namna hii na wanaofanya kazi muhimu kama hii ni

kujipuuza wenyewe. Tunaweza tukajificha lakini hatuwezi kukwepa. Ni wajibu wetu kujali matakwa ya wengi. Sauti ya Walimu ni sauti ya wananchi, ni sauti ya demokrasi, ni sauti ya watu wanaofanya kazi ya kulea watoto wetu. Kwa hiyo, ninapendekeza kwamba, kutokana na kazi muhimu wanayofanya Walimu ya kulea watoto wetu huenda tusipowajengea mazingira mazuri tutasababisha wasifanye kazi nzuri ya kulea watoto wetu. *A hungry man is always an angry man* na hawa Walimu wengi ni *hungry.* Pale Njombe kila mwisho wa mwezi Walimu hujaa kwenye Ofisi ya Mkurugenzi wakisubiri mishahara. Inaumiza sana. Wakati mwingine huwa kuna mvua na hakuna mahali pa kujificha. Kwa hiyo, hukaa kama wafungwa wanaosubiri kupewa posho na hawa ndio watumishi wanaolea watoto wetu. Ni vizuri tuharakishe zipelekwe benki Vijijini ili kupunguza matatizo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ufalme wa matumaini hakuna kipupwe, Walimu hawa ndiyo tumaini letu, tukipoteza matumaini kwa watu wengi kama hawa tumekwisha. Katika shule yangu moja ya sekondari ya Lupembe Walimu wamekaa zaidi ya mwaka mmoja bila kupewa mishahara. Mwalimu kama huyo unategemea afanye kazi vizuri darasani kwa miujiza gani? Nashukuru Wizara imeahidi kufupisha njia na kuchukua hatua za haraka ili kurekebisha hali hii. Lakini ni tatizo ambalo linapunguza hata hadhi ya Walimu. Kuwapuuza Walimu ni kujipuuza wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili katika mapendekezo ya ujumla, nasema kwamba, utaratibu wa kujenga nyumba fupi, *bungalow,* katika nchi yetu utamaliza nchi yetu. Katika Miji kupanua majengo haya, kujenga nyumba nyingi za aina hii ni kuongeza umaskini, ni kupunguza maeneo ya kulima muhogo na mchicha, sasa tutaendelea kujenga nyumba za aina hiyo mpaka wapi? Hofu yangu ni kwamba, nchi hii baadaye itajaa nyumba bila mashamba. Je, ndiyo lengo letu? Wakati sasa umefika wa kutazama upya sera ya ujenzi wa nyumba katika Miji yetu. Vinginevyo tunajidanganya wenyewe. Miji itaungana. Tanzania nzima itakuwa Miji na kilimo kitakufa na watu watazidi kuwa maskini zaidi. Sidhani kwamba hili ndilo lengo letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu katika mapendekezo yangu ya ujumla ni kuomba mwongozo. Hivi pale palipo na Serikali zaidi ya moja ya Miji kama vile Njombe ambako unaweza ukaunda Miji mingi, kama vile Makambako, Njombe Mjini, Ilembula, Uwemba, Lupembe, Kifanya, ikawa Miji Midogo kwa sababu ya idadi ya watu kuwa wengi, je, muundo wake utakuwaje? Watawajibika vipi? Nadhani ni vizuri kutazama mbali. *When leaders have no vision, the people perish.* Ni lazima tutazame mbali, maana Vijiji hivi siyo *static* wala Miji siyo *static* kwa sasa hivi tunasubiri Vijiji vikue ili tubatize viwe Mji. Tunasubiri wakati inazidi kuendelea au kujengwa vibaya lakini ikishakuwa na watu wengi tunabatiza na kuwa Mji kama Kibaigwa au kama Ikwiriri. Ikwiriri ni Kijiji kimoja katika Mkoa wa Pwani chenye watu zaidi ya elfu kumi lakini kina Vijiji tisa katika eneo moja na Kata tatu katika eneo lililoungana. Lakini vile Vijiji tisa vyote vina Serikali zake. Sasa unauliza hapa unaongoza vipi! Keshokutwa Serikali itakubali Ikwiriri uwe Mji lakini huku ni kubatiza *chaos.*

Ninapendekeza kwamba katika hili wakati umefika wa kupanga Vijiji vyetu katika ngazi nane zifuatazo: Kitongoji, Kijiji, Kijiji Mji, Mji Kijiji, Mji Mdogo, Mji, Manispaa na Jiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa njia hii tutazuia kukua kiholela kwa Vijiji vyetu na kuzuia kukua kwa Miji kusiongeze umaskini katika nchi yetu. Eneo hili la Vijiji na Miji linahitaji *thrust* ya aina yake. Kwa sasa hivi Vijiji havina mwenye navyo. Kwa mfano, hivi sasa tumeamua kubatiza Vijiji 88 vikubwa kama vile Makambako kuwa Miji Midogo. Mwaka 2005 tutabatiza vingine tena. Kwa hiyo, ni vizuri tukaanza kuwa na sera itakayotusaidia kukagua na kupanga Vijiji katika ngazi kadhaa na kila mwaka kuwe na wakaguzi kama wanavyokagua shule na kuweza kupandisha masharti yatakayotawala kila ngazi ya Kijiji ili kuepusha ghasia hii ambayo inaendelea. Natumaini ninaeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ninalopendekeza hapa linahusu lile alilosema Mheshimiwa Mbowe kuhusu vikao vya Vyama. Hivi karibuni kumekuwa na Vikao vya Viongozi wa Vyama vya Siasa chini ya Wizara hii ya TAMISEMI. Kwa kuwa sote tunakubaliana kwamba, rushwa ni adui wa demokrasi na ni adui wa haki, ninapendekeza kwamba suala la rushwa lifanyiwe kazi na Viongozi wa Vyama vyote, yaani wakae pamoja, waweke mwongozo utakaotawala nchi nzima kwenye uchaguzi wa kila aina. Mwongozo huo upelekwe katika kila Kijiji na katika kila Mji anapokamatwa mwanachama wa Chama chochote awe anatawaliwa na taratibu ambazo zimekubaliwa na Vyama vyote na chini ya wasimamizi wa Tume ya Uchaguzi ili kuepusha jambo hili. Vinginevyo tutaendelea kuimba wimbo tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya makosa ya rushwa yanahalalishwa na baadhi ya Vyama kwa sababu wanasema mimi nikiwa mkali wakati mwenzangu anaendeleza rushwa, nitakosa kura! Kwa hiyo, wote wanaendeleza rushwa kwa sababu hakuna mwongozo unaotawala Vyama vyote, je, si vizuri basi wazo kama hili likaletwa mapema na kwa vile Vyama vyote vinachukia rushwa na sasa tunakwenda kwenye uchaguzi? Hili ni pendekezo kwa Wizara hii kwa vile inahusika na uchaguzi wa baadhi ya viongozi wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ninapendekeza hapa na limesemwa kwenye Sera ya Vijiji, hivi Kijiji ni nini? Tusipoangalia Vijiji kama vile vya Ikwiriri ambavyo vimejaa pamoja Vijiji tisa, halafu tunaamua kwamba, kila *VEO* alipwe isipokuwa Mwenyekiti, wakati wote wanafanya kazi ile ile, tunaongeza matatizo zaidi, hakuna uwezekano wa kukua kiuchumi. Wakati umefika sasa kwa Serikali kutazama upya dhana ya Kijiji kwa lengo la kurekebisha baadhi ya dosari hizi badala ya kuendelea kubatiza na kuandikisha Vijiji. Uamuzi wa Serikali wa kulipa mishahara *VEOs* ufanane na mikakati ya kuendeleza Vijiji. Vinginevyo sielewi hii *manna* inayo-*fall freely from heaven*, inatoka wapi, kumlipa mtu kwa kukaa kijiweni tu wakati kiuchumi hakuna maendeleo ni kudhoofisha nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vijiji vinatofautiana, mahali pengine Kijiji kina watu 1,500, mahali pengine Kijiji kina watu zaidi ya 4,000. Makambako bado ni Kijiji mpaka

sasa, Ilembula ni Kijiji, Lupembe ni Kijiji, Mtwango ni Kijiji, Lima nacho ni Kijiji chenye watu labda 800. Vijiji visipopangwa katika ngazi kwa lengo la kuviendeleza tutakuwa kila wakati tunafanya kazi ya zimamoto, vikishakuwa na watu 40,000 tutageuze Miji, wakati tabia yote ni ya Kijiji. Natumaini naeleweka katika hili. Dhana ya Kijiji haiko wazi. Kutokana na maeneo ya nchi yetu hivi sasa kwa mfano, ukitoka Njombe kuelekea Makete ni mnyororo wa Vijiji hadi Moronga. Pia kutoka Makambako kwenda Njombe ni Vijiji mpaka Njombe, vinatengwa tu na ile miti ya miwati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii na naomba nianze kwa kuwashukuru Waziri, Naibu Waziri wa Wizara hii na Katibu Mkuu wake Ndugu Mmari, ambao kwa kweli wametembelea Wilaya yangu na wameona hali halisi ilivyo na wamejaribu sana kutushauri na kwa kweli ndilo hilo lililotusaidia sisi kwenye mpango wa mahindi ya njaa, hatukudai kitu. Ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri bado, nadhani hana nafasi nitaomba naye atakapopata nafasi aje aione hiyo Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbozi inapakana na Malawi na Zambia. Tunduma ni Mji Mdogo wala siyo Kijiji, lakini hauna hata kituo cha afya. Watu wanachotegemea ni kwenda Zambia kudoea doea dawa. Sasa mimi nilikuwa naomba Wizara hii ilione hili kwani ni fedheha kwa watu wetu kudoea katika nchi ya watu wengine. Ni aibu kubwa sana na nadhani Waziri amelielewa hilo na hataliacha katika mawazo yake ya kumalizia pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Wilaya yetu hii ni kubwa kwa kweli. Jimbo la mwenzangu ukitaka kwenda kutoka Wilayani mpaka mpakani na Sumbawanga ni maili tisini, siyo kilomita, ni maili tisini na akienda kule lazima arudi Wilayani aende Kamsamba maili tisini tena. Sasa hili tumekwishalisema na kuomba msaada, lakini Waziri leo sikuona aliposemea na nimeona hela za barabara ni kama kidogo sana na hili nadhani ataangalia, atakwenda achambue chambue kilichosalia, aokoteze, angalau tujaribu. Wananchi wapo tayari kutafuta mawe na kupiga kokoto, Serikali iwasaidie kuwawezesha kujenga daraja ili waunganishe angalau kutoka Kamsamba kwenda Ndarambo na hata wenzetu wa Rukwa watapata nafuu sana kwa sababu mnada wa mifugo upo kwetu, wanapata shida kubwa sana watu wa Sumbawanga. Hilo litatusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kwamba, tunashukuru tumepata hizi mashine za *Ultra Sound,* lakini hatuna wataalam. Kuna mhisani amejitolea, yuko pale Kilimanjaro, amejitolea kwa gharama zake anawafundisha watu hawa kuitumia *Ultra Sound* lakini watu hawa hawana *scheme of service,* wapo tu, hii maana yake nini? Yule mhisani nilikutana naye akasema mimi siwaelewi, mlisema hamna uwezo wa kufundisha, nimewaletea chuo, nawafundisha kwa kiwango cha shahada, leo hamtaki kuwatambua wala *scheme of service* hawana maana yake nini? Sasa naomba hili Wizara pia ilitolee maelezo ya kueleweka hapo baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mmoja hapa anaposimama anadai hela. Hela hakuna, hata mimi nadai hela, hela zitoke wapi, nani alete hela, kama si sisi. Tatizo la umaskini ni letu wala tusifikiri kuna mahali hela zitadondoka kama mvua kwa rehema ya Mungu tutajirike nchi hii, hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tufanye kazi na lazima kila mtu ahakikishe katika eneo lake wanafanya kazi. Namshukuru sana Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, alikuja kule kwangu, alikwenda ndani kabisa, aliwakuta watu wanafanya kazi bila kuambiwa na mtu, wanazalisha wenyewe. Ndio maana sisi suala la njaa kule hatulizungumzii sana. Liwe ni bahati mbaya tu ambayo hata mtu anaweza akaanguka hata hapa Bungeni bila kutegemea. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kila mara tunapofanya mipango yetu hivi tunafanya watu wazalishe kwa utaratibu gani? Hakuna uzalishaji usio na mpango na utaratibu wa kueleweka. Wakati ule wa siasa ya ujamaa, kulikuwa kila Wilaya, kila Kijiji kinafanya mipango yake na wanatekeleza kulingana na malengo ambayo yanakuwa yamekusanywa na wanafuatiliwa kwa malengo yale kama wamehitimisha au vipi na kama hawakuhitimisha walikuwa wanaulizwa na kwa kweli siku zile za siasa ya ujamaa na kujitegemea hakukuwa na njaa. Watu wanaosema ujamaa ndiyo uliorudisha uchumi ni wale wachoyo, walafi, wanaotaka wajinufaishe wenyewe na ndilo tatizo tulilonalo. Leo hii tunaajiri watu wanahitaji fedha, zitoke wapi, badala ya kusema tuwe na utaratibu kila Kijiji kiwe na malengo na kisimamie kwa mazao ya chakula na mazao ya biashara ili wainue uchumi wao pale. Ule wakati wa ujamaa Vijiji vilikuwa vinalipana posho, lakini wamepita watu humu wamevuruga vuruga, sasa hakuna hiyo na leo tunazungumza kwamba eti tutaendelea, tutaendelea vipi? Kila mmoja humu anaomba hela, ziko wapi? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho tutakwenda kuomba hata kwa watu ambao hawastahili. Kwa kweli ni aibu, hivi kweli hata chakula cha kumsimamia mtu azalishe chakula chake mwenyewe tushindwe mpaka twende Ethiopia, ingawa mnasema tumenunua! Hizo hela za Ethiopia mngetuletea sisi kule Mbozi ili tuwape chakula na hata sasa mnazidi kuchelewa, Waziri juzi alisema sijui zitanunuliwa tani nyingi tu kama laki moja, sasa zitanunuliwa wapi. Anasema tungoje mpaka kwanza mahindi yakauke zaidi. Nani atakusubiri akaushe mahindi pale wakati watu wanahitaji hela. Mimi nadhani miradi hii ya kununua haya mahindi ya *SGR* ni miradi ya watu. Kwa hiyo, wanaweka kila vipingamizi ili msifanikiwe, wao wafaidike. Ni hatari sana, hatuendi mahali. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kila Wilaya na kila Kijiji wasimamie malengo yao kwanza, watoe malengo kuanzia sasa na Wakuu wa Mikoa waende huko wawaambie Viongozi wa Wilaya watayarishe malengo mwezi wa nane yafike Mikoani ili tuanze kufuatilia nani anatekeleza na nani hajatekeleza. Sio watu wakae kungoja posho na mishahara kupanda, inatoka wapi? Zalisheni ndiyo mdai posho na nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema kila Wilaya iwe na mpango wa mazao, zao moja la chakula na zao moja la biashara, mazao gani? Maana tunasema ukame umeharibu kila kitu. Kuna mmoja alikuwa ananiambia anasema sisi hatujapata ukame, ukame hauwi hivi, angalia nyasi zilizopo nje, zimeota na zimekomaa. Ukame gani wakati mahindi ulilima umechelewa! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alituambia kwamba, mvua za kwanza ni za kupandia, lakini watu mvua za kwanza ndiyo za kuangalia, je, itarudia tena. Matokeo yake ndiyo maana tunachelewa, mazao hayakomai. Hata hapa Dodoma watu wamepanda, wamevuna kweli kweli. Naishi na Masista pale, wamevuna mahindi ya kutosha kabisa hapo Ipagala, lakini watu wananung'unika tu njaa, Dodoma njaa, iko wapi? Lazima watu tubadilike na tuzingatie kazi na tuheshimu kazi na kila mtu aishi kwa kazi. Tusimamiane siyo suala la kuoneana aibu, siyo suala la kudanganyana danganyana. Kwa hiyo, vile Vijiji ambavyo vitafanya kazi nzuri vitaondoa njaa katika Vijiji vyao.

Ninaomba Wizara hii itenge zawadi hata ndogo ndogo vipewe vile Vijiji kama shukrani ya juhudi yao, wengi wataibuka na watafanya kazi kwa wingi, lakini maneno matupu, haya limeni, jipangeni, zalisheni kwa msingi upi na sheria ya Nguvu Kazi mmeshaifuta, nani atamsukuma mwenziwe? Kwa hiyo, ninasema Serikali ianze mara moja suala hili na malengo yote ya nchi hii yaletwe na tuwapime watu kwa malengo yao waliyoweka, ambaye hakutimiza hana maana ya kuwepo hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu kumpa Mtendaji wa Kijiji mshahara na Mwenyekiti ambaye kwa kweli ndiye msimamizi wa Kijiji pale asipate hata sabuni ya kufulia shati lake, nayo itakatisha tamaa. Ni afadhali tungesema tunawapa posho, Watendaji wapate posho ya shilingi hata 20,000/= na Mwenyekiti hata shilingi 50,000/= kwa mwezi, wangefanya kazi hii kwa moyo zaidi na wangefanikisha kwa mafanikio. Lakini tabia ya kupendelea mishahara ya fedha msizonazo, hatuwezi kwenda mahali. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu huko Wilayani mimi sijui kama Wizara hii inaelewa. Wilayani huko nani amdhibiti nani kati ya *DC* na Mkurugenzi. Mimi nilikuwa *DC* na nilikuwa naandika ripoti ya Wakurugenzi. Kwa hiyo, Mkurugenzi nikimwambia bwana tunafanya hili twende Kijijini, tulikuwa tunakwenda maana aliogopa mimi ndiye nitakayemwezesha aeleweke vizuri katika kazi. Lakini leo *DC* hana mamlaka na hela hana na lofa hana amri, hana nguvu. *DC* ni kiasi cha kumwambia umekosa safari bwana mafuta haya, basi atamkaripia vipi *DED*. *DEDs* wengi ni Mangimeza hawaendi Vijijini, nendeni Vijijini mkaitishe vitabu vya Vijiji, mwone walichoandika mle kama waliwahi kwenda. Lazima tubadilishe, tugeuze, haya ni mapinduzi kwa uchumi wetu na kwa uzalishaji wetu. Hili ndilo jambo ninalosisitiza tuanze nalo na bila kuchelewa na Waziri hili wala usione aibu kumwambia mtu, watu wabanwe kwa misingi hiyo na Mkuu wa Mkoa wabane Wakuu wa Wilaya. Sasa Mkuu wa Mkoa anamwuliza *DC*, Mkurugenzi anasema mpaka Madiwani wakubaliane na hili, tunakwenda wapi? Lazima upate mtu mmoja mwenye amri ya wote Wilayani pale.

Kwa hiyo utaratibu huu ubadilike kabisa hautatupeleka mbali. Tutakufa maskini. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. FRANK G. MAGHOBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Ninachukua nafasi hii kuwapongeza Viongozi wa Wizara ya TAMISEMI, Mheshimiwa Brigadia Jenerali Hassan Ngwilizi, Naibu Waziri, Mheshimiwa Mizengo Pinda, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu bajeti yao imeletwa leo na kuwasilishwa kwetu hapa, wote tumeisoma na kusikia, ni nzuri na yenye mwelekeo wa kutosha, lakini ina mambo mengi ambayo inabidi tuyafanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue nafasi hii nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa agizo lake la jana ambalo alisema kwamba, Walimu watekelezewe haki zao mara moja. Hiyo kwa kweli inabidi nimpongeze kwa sababu ndiyo tulikuwa tunahitaji na tunahitaji viongozi kama hao ili wawe na agizo la kufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nichukue fursa hii kumpongeza Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mheshimiwa Luteni Yussufu Makamba, ninapongeza kwa sababu nyingi tu kwanza, ni mchapakazi, pili, amekuwa mstari wa mbele kusimamia maendeleo ya Mkoa wa Dar es Salaam na maeneo yake. Mheshimiwa Yussufu Makamba, amekuwa karibu sana na mimi pamoja na kwamba ninatoka upande wa pili, kwa kazi zote za maendeleo amekuwa ananishirikisha kwa namna moja au nyingine kuhakikisha ninafanya kazi pamoja na Serikali. Lazima nimpongeze kwa sababu hiyo ndiyo tunaihitaji na ndiyo tunaiita demokrasia. Kwa sababu nia yetu Watanzania wote ni kusimamia maendeleo na siyo vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninampongeza Mheshimiwa Edson Halinga, kwa mchango wake mzuri aliyouchangia sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kidogo kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na hasa pale aliposema kwamba, demokrasia na Utawala Bora katika ngazi ya vijiji, mimi ninakubaliana na hilo. Lakini nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri labda kuna mambo mengi yanampita pembeni na naomba nimsaidie nimwambie kuwa, hivi karibuni kwenye kijiji kimoja cha Mkuranga kuna wakazi ambao wanaishi katika kijiji cha Ahsante Mwinyi, wakazi hao walikuwa kwenye Jimbo la Kigombani lakini baada ya mipaka kusogezwa wakasogezwa wakawa eneo la Mkuranga kwa Mheshimiwa Dr. Hussein Mwinyi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi hao wamekaa takriban miaka zaidi ya 15 au 20 hivi lakini hivi karibuni wananchi hao wameambiwa waondoke katika maeneo yale na kupelekwa mahali ambapo hapajulikani. Wananchi hao walipotaka kupata haki yao kilichotokea ni kwamba, wamechomewa moto nyumba zao na sasa hivi wananchi hao

hawana mahali pa kuishi. Wananchi hao hivi sasa ninapozungumza, hawana mahali pa kuishi wanaishi kwa ndugu zao, zaidi ya watu 200 hawana mahali pa kuishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaposema Utawala Bora katika vijiji lazima tuwe wakweli, yale ambayo tunaona kwamba kuna makosa lazima tuyafanyie kazi haraka ili wananchi wasiwe na malalamiko inapofikia mahali wananchi wanakuja mpaka Dodoma kufuatilia suala ambalo liko wazi mimi sioni kama kuna sababu ya msingi. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwamba, afuatilie na anipe maelezo ya hao watu waliochomewa moto nyumba zao, Serikali imechukua hatua gani mpaka sasa hivi. Wananchi hao wanaambiwa waondoke katika eneo lile waende wapi wakati hao ni Watanzania siyo wakimbizi. Ingekuwa ni wakimbizi hata wakimbizi wana haki yao kama binadamu. Kwa hiyo, ninaomba tunaposema Utawala Bora lazima tujali wananchi wetu ambao wametuweka madarakani. Hatuwezi kuimba Utawala Bora wakati kuna watu wanaumia na wana matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba suala hili lipatiwe majibu haraka sana kabla hatujamaliza Bunge hili. Ninasema hivyo kwa sababu ni suala la msingi na ni suala la kusikitisha kwa sababu kama Watanzania leo tunawafukuza kwa madai kwamba yale maeneo ni maeneo ya utalii, mimi sina uhakika sana na hicho kitu. Lakini naamini kijiji kile kiitwacho Ahsante Mwinyi baada ya Rais Mstaafu, Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi kuwapa na kuwaruhusu wakae pale leo unapowaambia waondoke waende wapi? Naomba Serikali itoe ufafanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachangia kwenye suala lingine la hospitali, ninazungumzia Hospitali ya Temeke. Labda tu niwapongeze Waganga wa Hospitali ya Temeke kwa kazi kubwa wanayoifanya katika hospitali ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Temeke inahudumia wagonjwa wengi wa maeneo mengi, wanaotoka Mkuranga, wanaotoka Ilala na wanaotoka katika sehemu mbalimbali na imetokea baada ya Hospitali ya Muhimbili kuweka utaratibu mwingine, kwa hiyo, watu wanashindwa kwenda Hospitali ya Muhimbili wanaamua kwenda Temeke na katika hospitali nyingine. Kwa hiyo, matokeo yake wagonjwa wengi wanashindwa kupata huduma kwa sababu hospitali ile kwanza ni ndogo na pili ina Waganga wachache na manesi wachache. Kutokana na hali hiyo kuna msongamano na lazima kuna watu wataathirika katika suala la kutaka wapewe huduma. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali kwa makusudi kabisa, Mheshimiwa Sophia Simba amesema, tunaomba ikiwezekana tupate Hospitali ya Mkoa ili iweze kupunguza idadi ya wagonjwa katika hospitali zetu, hilo litapunguza malalamiko ambayo yanatokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mama mmoja alifariki pale baada ya kukosa huduma ya haraka na hiyo ni kutokana na msongamano wa wagonjwa wengi katika wodi ya akinamama na Tume iliundwa ili kuchunguza suala hilo, lakini ikaona kwamba, kweli pale kuna watendaji wazuri isipokuwa tatizo ni watumishi wachache katika hospitali ile. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali kwa makusudi kabisa kutokana na hali ilivyo, kwanza, iongeze Waganga katika Hospitali ile ili iweze kutoa huduma kama inavyotakiwa na pili

iongeze manesi wa kutosha katika hospitali ile ili wagonjwa wale wahudumiwe ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ninaomba Serikali kwa kushirikiana na Manispaa yetu, waongeze ukubwa wa Hospitali ya Temeke na ikiwezekana hospitali ambazo ziko kwenye Kata zipewe hadhi kama alivyosema Mheshimiwa Sophia Simba, ili ziwe hospitali ambazo zinaweza kuhudumia wagonjwa katika Kata zao na kupunguza idadi ya wagonjwa wanaokwenda katika Hospitali ya Temeke. Itasaidia sana kupunguza malalamiko na kuona kwamba, Serikali haifanyi vile inavyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakuja kwenye suala la kodi. Juzi nilikuwa ninazungumzia suala la kodi wakati nikichangia katika Wizara ya Fedha, niligusia kidogo suala la kodi. Nakumbuka mwaka 2003, Waziri wa Fedha alisema kwamba, Serikali imefuta kodi zote za majengo pamoja na kodi zingine zilizokuwa zimejitokeza na ilisemwa kabisa kwamba, wale ambao hawana hati za nyumba hawataguswa katika suala la kodi. Sasa naiomba Serikali ifafanue hilo. Wananchi wangu kule sasa hivi wamekwenda Mahakamani kwa sababu ya kodi ya majengo wanachanganyikiwa ni watu gani wanatakiwa kulipa *property tax* na ni watu gani ambao hawatakiwi kulipa. Sasa Serikali itoe ufafanuzi ili watu wajue kama kuna kulipa wajue walipe na kama hakuna kulipa wajue wasilipe. Kwa sababu sasa ni mkanganyiko mtupu. Sasa leo wananchi wangu wananipigia simu kusema kuwa sisi tunapelekwa Mahakamani. Sasa mlituambia kodi mmefuta kama kero lakini bado kuna tatizo hilo. Kwa hiyo, ninaomba Serikali itoe ufafanuzi juu ya suala hili ni kodi gani zilizofutwa ili wananchi wajue na waweze kulipa kodi panapotakiwa kulipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja kwenye suala la elimu. Jana Mheshimiwa Waziri Mkuu, alisema kwamba, katika ujenzi wa shule lazima wananchi wachangie na ndivyo nadhani nilikuwa naelewa mimi siku za nyuma na mimi nilikuwa mstari wa mbele sana kuhakikisha kwamba, nawashawishi wananchi wangu wachangie panapotakiwa na kuanzisha ujenzi wa shule na mwisho Serikali inakuja kumalizia pale tutakapokwama.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kilichotokea hivi karibuni Wenyeviti wa Kamati za Shule waliitwa Wizara ya Elimu na Utamaduni wakaambiwa kwamba ni marufuku kuwachangisha wananchi katika ujenzi wa shule, Serikali itatoa fedha na jana Mheshimiwa Waziri Mkuu alitamka kwamba, wananchi wachangie. Sasa mimi ndiyo hapo ninashindwa kuelewa tunatakiwa kufuata lipi? Leo hii wananchi wanashindwa kuchangia kwa sababu kwanza walikuwa na mori tayari kwa sababu michango wamechangia katika shule nyingi tu kule kwangu Zansa B, Zansa A, Kichemchem, wamechangia nguvu zao katika ujenzi wa shule kufikia mpaka kwenye renta, Serikali ikaja kumalizia kwa kuezeka na kufanya *finishing,* lakini leo hii unaposema wananchi wasichangie tunafanya nini na unaposema wasichangie matokeo yake sasa tunashindwa kuendeleza kujenga shule kwa sababu fedha zinazotolewa zinatolewa kwa ajili ya ukarabati au kuanzisha shule, kitu ambacho Serikali ikitoa fedha haitoi za kumalizia shule yote kuanzia chini mpaka juu. Kwa hiyo, ninaomba Serikali pia itoe ufafanuzi katika masuala hayo. Kwa sababu sasa kuna mkanganyiko badala ya sisi kuonekana

tunashawishi wananchi ili wajiletee maendeleo wenyewe. Maana yake nadhani katika Chama cha Mapinduzi mnasema kabisa kwamba, wananchi watasimamia miradi yao na kuchangia miradi wao wenyewe leo hii mbona mnabadilika tena mnasema kwamba wasichangie! Toeni ufafanuzi tuelewe kwamba tufuate lipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, lazima tuwe wakweli na tunapofanya kazi tufanye kazi kama timu moja, tusifanye kazi kila mtu anatoa maamuzi yake yanatuchanganya na siyo kutuchanganya sisi tu yanawachanganya hata wananchi ambao wako tayari kuchangia. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa unaikubali? Sasa Mheshimiwa Waziri naona amekubali taarifa yako.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimsaidie kidogo Mheshimiwa Mbunge, kwa kumpa taarifa kwamba, michango inayokatazwa ambayo hairuhusiwi ni ile inayotozwa wazazi wa wanafunzi peke yao kwa sababu hiyo italeta athari katika uandikishaji na mahudhurio ya wanafunzi. Lakini michango inayochangishwa Jumuiya nzima kwa shughuli za kujitegemea kama kujenga shule hiyo inaruhusiwa. Kwa hiyo, ninapenda Mheshimiwa Mbunge, ajue hiyo tofauti. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Baada ya taarifa hiyo Mheshimiwa Mbunge endelea.

**MHE. FRANK G. MAGHOBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa ufafanuzi huo, kwa sababu nilishachanganyikiwa tayari kwa jinsi ilivyokuwa kama ni hivyo basi ninashukuru. Lakini taarifa zilizokuja kwangu nadhani zilikuja vibaya kwamba, walikuwa wamezuiliwa kutoza michango ya aina yoyote. Nashukuru kwa hilo. Nadhani Vyombo vya Habari vitatoa taarifa hizo wataelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niko hapo hapo, juzi Mheshimiwa Waziri katika swali moja aliulizwa kwamba, kuna watoto ambao ni yatima, ambao hawana uwezo wanatakiwa kusaidiwa kusomeshwa kwa mfano, elimu ya sekondari na vitu kama hivyo. Nadhani Mheshimiwa Waziri alisema kwamba ni kweli Wilaya ya Temeke kuna nafasi kama 33 ambazo hazijajazwa, ni kweli kabisa. Ni kweli nafasi zile hazikujazwa kwa sababu utaratibu nadhani haueleweki vizuri. Aidha, watu wanapokwenda pale hawajui wafuate utaratibu gani mpaka kuchaguliwa au kuteuliwa kusomeshwa bure na Serikali. Kwa hiyo, ninaomba pia Serikali hilo ilifafanue ili wananchi wafaidike na huo msaada wa MMEM ambao Serikali imeutoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakuja kwenye suala la barabara vijijini. Katika Jimbo langu la Kigamboni kuna vijiji vingi ambavyo barabara zake bado si nzuri na wananchi wengi wanalima katika Jimbo langu mazao mengi ambayo ni ya biashara. Kwa

mfano, Kimbiji, Tuangoma, Mwongozo, Yaleyale, Puna na sehemu kadhaa. Lakini kuna maeneo ambayo magari yanapita kwa tabu hasa wakati wa mvua. Kwa hiyo, ninaiomba Wizara ya TAMISEMI itupie macho maeneo ya Jimbo ya Kigamboni kwa sababu ni eneo ambalo tunaamini kwamba, sasa ni eneo ambalo viongozi wengi wana maeneo ya kujenga nyumba zao na siyo hilo tu lakini wale wananchi wanahitaji kufaidika kwa kupeleka mazao yao kwa urahisi Sokoni Kariakoo.

Kwa hiyo, ninaomba sana barabara hizo ziangaliwe ili angalau tupate msaada na kama Mheshimiwa Waziri akitaka maelezo zaidi basi niko tayari kumfuatilia ili nimpe maelezo zaidi tuone jinsi ambavyo anaweza kutusaidia tufanikishe suala hilo. Kwa sababu nia ni kujenga na siyo kubomoa na nia ni kujenga na kuboresha maisha ya wananchi wetu ambao tunawawakilisha hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda pia nije kwa ndugu yangu, Katibu Mkuu wa Wizara ya TAMISEMI, ninataka kumpa ushauri tu kwa sababu nia yangu ni nzuri. Katibu Mkuu anafanya kazi zake vizuri, ninadhani anafuata taratibu zao zote zinazotakiwa kufanya kazi. Lakini tunaposema matumizi mabaya ya fedha lazima tuwe wazi katika kusimamia matumizi ya fedha za Serikali na mbaya hasa ni fedha za walipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema hivyo kwa sababu inawezekana Katibu Mkuu hajapata washauri wazuri na hasa ninazungumzia kwenye kitengo cha kutengeneza magari ya Wizara. Katibu Mkuu anafanya vizuri kupeleka magari Dar es Salaam kufanyiwa matengenezo ya kawaida na makubwa. Lakini Katibu Mkuu ninataka nimshauri kwamba, magari kuyapeleka Dar es Salaam kutengenezwa kilomita 500 kwenda na kumpa dreva fedha za mafuta na fedha za matumizi na kupeleka gari gereji ukipiga hesabu gharama za matengenezo ya gari hilo ni kubwa mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninampa ushauri kwamba, apate wataalam waweze kumsaidia katika kusimamia magari. Dodoma kuna gereji nzuri ambazo zinahitaji kusimamiwa katika suala la matengenezo ya magari. Kwa hiyo, ajitahidi kuhakikisha vijana wetu ambao ni *Transport Officers,* wasimamie kazi hiyo, yale magari ambayo yako kwenye mkataba yapelekwe Dar es Salaam kama inavyokusudiwa. Lakini yale yanayohitaji matengenezo ya kawaida, kwa sababu ukiangalia malipo kwa *dealers* ni *very expensive* kutengeneza gari moja. Gari moja kwa mwaka mmoja ukija kulitengeneza unaweza kujikuta unanunua gari lingine la pili kwa gharama za matengenezo ya gari moja kwa mwaka au kwa miezi sita.

Kwa hiyo, ninamshauri Katibu Mkuu aangalie matumizi ya matengenezo ya magari kwa faida ya umma kwa sababu fedha zinazotolewa ni kodi za wananchi na walalahoi. Matumizi yake tuyaangalie tusiseme tu kwa sababu labda kuna matatizo ya namna hiyo lakini tuangalie matumizi yako vipi na kwa faida ya nani. Huo ni ushauri wangu kwa Katibu Mkuu kwa sababu ni moja ya matumizi mabaya ya fedha za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli katika yote ambayo nilitaka niyaseme nimeshayasemea. Lakini moja la mwisho, nitazungumzia suala la Madiwani.

Wenzangu wengi wamezungumzia suala la hili,Madiwani wanapata tabu sana katika utendaji kazi wao kwa sababu hawana vitendea kazi, posho yao ni ndogo na wanafanya kazi kwa muda mwingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. AARON D. CHIDUO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie machache katika kuijadili hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, ninasema kwamba, nimeipokea hoja hii kwa mawazo mchanganyiko. Kuna sehemu za hotuba hii zimenikatisha tamaa. Nitaanza na eneo la maeneo mapya ya utawala. Katika ibara ya 20 imetamkwa kuwa: "Katika mwaka huu wa fedha wa 2004/2005, Serikali haikusudii kuanzisha maeneo mapya ya utawala." Nimeichukulia kauli hii kuwa hakuna Wilaya, Tarafa au Kata zitakazogawanywa wala vijiji vipya vitakavyoandikishwa. Kwa baadhi yetu kauli hii ni kutuua kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikichukulia Wilaya yetu ya Kilosa ambayo ni Wilaya kongwe, maombi ya kuigawa Wilaya ya Kilosa ni ya siku nyingi. Suala la kuigawa Wilaya ya Kilosa lilianza mwaka 1965, mwaka 1975 Wilaya hii ilitazamiwa kugawanywa kuwa Wilaya mbili bila mafanikio, mwaka 1980 suala hili liliibuka tena, mwaka 1994 maombi yalipelekwa tena Serikalini, mwaka 1999 suala la kugawa Wilaya kwa lengo kuu la kuboresha huduma na kuharakisha maendeleo lilipelekwa kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ili lilishughulikiwe kabla ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa matokeo yake yakawa patupu. Nilipata uchungu sana wakati Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa katika hotuba yake kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 30 Januari, 2002 alipotangaza kuzigawa Wilaya sita mpya za Iringa, Morogoro, Mwanza, Shinyanga, Songea na Tabora na baadaye ya saba ni Wilaya ya Handeni, kila moja kuwa Wilaya mbili. Wilaya ya Kilosa haikuwemo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata sikuelewa sasa tufanye nini? Kwa kuelewa kuwa ombi hili tayari lipo kwa Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, nilimwandikia Mheshimiwa Waziri barua tarehe 6 Agosti, 2003 kumkumbusha ombi letu na nikatoa hoja za utetezi ambazo nilikuwa nina hakika ombi hili litazaa matunda. Barua yangu ilijibiwa tarehe 11 Novemba, 2003 kuwa hoja niliyowasilisha ilikuwa inafanyiwa kazi na ningejulishwa maamuzi. Nikawa na matumaini. Sikujulishwa maamuzi hadi leo kwenye hotuba kuwa: "Serikali haikusudii kuanzisha maeneo mpya ya utawala." Nimechanganyikiwa nitakwenda kusema nini kwenye Jimbo langu la Gairo kwa kuelewa kwamba, suala hili sasa limekuwa nyeti kabisa kisiasa. Kila kiongozi wa Serikali aliyetembelea Gairo ombi la kuigawa Wilaya ya Kilosa limekuwa likitolewa. Alipotutembelea aliyekuwa Makamu wa Rais, Marehemu Dr. Omari Ali Juma, wakati wa kampeni za uchaguzi za mwaka 2000, ombi lilitolewa. Alipotutembelea Mheshimiwa Waziri Mkuu mwaka 2003 hapo Gairo ombi hili lilitolewa, alipotutembelea Mkuu wa Mkoa wa sasa Mheshimiwa Stephen Mashishanga, Wazee wa Gairo walitoa ombi lao walimsihi sana kwamba Serikali ifikirie kuigawa Wilaya ya Kilosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kilosa ni kubwa ina eneo la kilomita za mraba 14,225, ni kubwa kuliko eneo la Kilimanjaro, hakuna jangwa. Idadi ya wakazi ni 489,513 kwa sensa ya mwaka 2002 idadi hii ni kubwa kuliko Wilaya tatu za Mkoa wa Tanga, Kilindi, Handeni na Pangani zenye jumla ya wakazi 438,038. Vilevile ni wengi kuliko Wilaya za Liwale, Nachingwea na Kilwa katika Mkoa wa Lindi zenye wakazi 406,483, Wilaya tatu za Kisarawe, Kibaha na Rufiji katika Mkoa wa Pwani zenye wakazi 430,761 na Wilaya tatu za Kilolo, Ludewa na Makete katika Mkoa wa Iringa zenye wakazi 439,662. Kutoka Makao Makuu ya Wilaya hadi mwisho wa Wilaya upande wa Kaskazini kuna umbali wa kilomita 210 kupakana na Kiteto na Kilindi. Kwenda hadi mwisho wa Wilaya upande wa Kusini kilomita 230 kupakana na Iringa na Mpwapwa. Kwenda upande wa Magharibi ni kilomita 340 kufikia kijiji cha mwisho ambacho ni cha Chanjale ambapo ni lazima upite Wilaya ya Kongwa kwenda Wilaya ya Mpwapwa mpaka kwenda kwenye kijiji hicho ambacho ni kijiji cha Wilaya ya Kilosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi ni vigezo gani vinavyotafutwa ili na sisi tukubaliwe ombi letu la kuigawa Wilaya. Hoja ya Serikali wakati wote ni hali ya uchumi itakapoimarika, lakini katika hali hii hii ya kutoimarika uchumi wetu Wilaya saba ziligawanywa mwaka 2002. Tumeikosea nini Serikali, hivyo vigezo havitoshi? Kwa hili natumaini ujumbe wangu umefika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nisingelileta hapa. Katika majedwali yaliyoambatanishwa katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri tumeelezwa juu ya Ofisi zetu za Wabunge. Taarifa ya fedha zilizotolewa mwaka 2003/2004, kwa ajili ya Ofisi za Wabunge, kwa Gairo imeandikwa jengo liko katika jengo ambalo tunatumia na Katibu Tarafa wa Gairo ambayo ni kweli. Maelezo yametolewa kwamba, ukarabati umekamilika na samani zote zimenunuliwa na hivi sasa ufungaji wa simu unaendelea. Hakuna lolote lililofanyika. Tumeelezwa hapa zimetolewa fedha shilingi 1,500,000/= hata senti moja haikutumika katika jengo lile. Mbaya zaidi ambayo imenisikitisha sana naletewa taarifa inabadilisha kusema kwamba, siyo katika jengo lako lililoko katika Jimbo lako Gairo bali ni katika Makao Makuu ya Wilaya huko ndiko kwenye ofisi inayokarabatiwa na huko nako hakuna ofisi hiyo. Mimi nimetoka huko wiki iliyopita sijaonyeshwa ofisi hiyo. Sasa ninajiuliza sababu ya kudanganywa ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli wakati mwingine tunaonyesha uungwana lakini uzalendo utatushinda. Si haki hata kidogo kudanganywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ninataka kusema la mwisho, naomba msaada wa Serikali. Iko barabara ya kutoka Gairo kwenda Nongwe, barabara hiyo ni muhimu sana kwa Tarafa ya Nongwe kwa miezi sita ya masika siwezi kufika kwenye Tarafa hiyo. Alipewa mkandarasi anayeitwa *Chrome Limited* wa Morogoro badala ya kuitengeneza barabara ile ameiharibu na si hivyo tu sasa anaishtaki Halmshauri ya Wilaya ya Kilosa kwamba, mkataba wake umesitishwa kwa hiyo alipwe fidia zaidi ya shilingi milioni 100 kwa barabara aliyoiharibu. Barabara hiyo ni muhimu, kuna vijiji katika Tarafa hiyo, hakuna Mkuu wa Mkoa yeyote au Mkuu mwingine yeyote wa Serikali ambaye amefika katika baadhi ya vijiji tangu tupate uhuru. Kuna kijiji cha

Mtega, Mheshimiwa Stephen Mashishanga ndiye alikuwa Mkuu wa Mkoa wa kwanza kufika katika kijiji hicho. Kuna Kijiji cha Nongwe, Mheshimiwa Anna Abdallah, alipokuwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro ndiye alikuwa Mkuu wa Mkoa wa kwanza kufika katika kijiji kile na Mheshimiwa Stephen Mashishanga akawa wa pili, sababu kubwa barabara mbovu. Hali ya hewa kule ni nzuri kweli kweli na mazao mengi yanastawi lakini barabara ni mbovu. Kwa hiyo, ninaomba msaada wa Serikali watusaidie kutengeneza ile barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninapata shida sijui niunge mkono hoja au nikatae kuunga mkono hoja, lakini kwa uungwana wangu, ninaunga mkono hoja hii kwa shingo upande. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nichangie.

Kwanza, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mwenyekiti wa Kamati za Huduma za Jamii na Kamati yake ambayo mimi ni Mjumbe, kwa kupokea malalamiko ya Chama cha Walimu Tanzania na kwa kweli kujaribu kuzunguka kwenye Wizara na kuiambia Serikali ili yaweze kushughulikiwa. Vile vile ninawapongeza Viongozi wa Chama cha Walimu Kitaifa kwa juhudi zao walizozifanya kuhakikisha kwamba, wanasafiri wanakuja Dodoma na wanatoa ushirikiano na kutoa takwimu ambazo zimetusaidia kwa pamoja na Wajumbe wengine waliohudhuria kuifikishia Serikali ili iweze kufanya maamuzi muafaka na ya hekima na busara. Kwa maana hiyo, mtiririko huo basi umfikie mpaka na Waziri Mkuu, ambaye amekubali. Nimesema hivyo kwa sababu ilikuwa inapotosha sasa kwamba, pongezi hizo zimwendee Waziri Mkuu tu peke yake, kumbe watu wengi wamefanya kazi kubwa kwa ujumla wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali ilivyo bado kuna lawama kwa Wizara hii ya TAMISEMI. Lakini mimi ninataka kuweka mambo mawili wazi. La kwanza, kuna mambo ya kiutendaji, kiutawala na kiutekelezaji yanayohusu Wizara hii, ikilaumiwa katika hayo ndiyo sahihi kabisa. Lakini kuna mambo mengine ya kiraslimali *(resources)*. Kwa uchambuzi wa kwangu ukiilaumu Wizara hiyo pengine tunakuwa tunakosea. Kama Wizara haitaki kuwasimamia Wakurugenzi, haitaki kuwaadhibu Watendaji wanaovuruga wanastahili hizo lawama. Lakini kama Wizara haikupewa fedha za kupeleka kutengeneza barabara halafu tukawalaumu kwamba hawajafanya kama Wizara ya Elimu nadhani tunawadhulumu na tunakosea na tunakuwa hatujiweki sawa katika kutaka kuishauri Serikali ifanye kazi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema hivyo kwa sababu tunaposema MMEM, kuna majukumu ya Kimataifa ya *millennium challenges* wamekubaliana na kanuni za migongano ziko tatu, *the Law Contradiction, the External Contradiction, the Internal Contradiction, the Basic Contradiction* na nyingine anazijua Mheshimiwa Aggrey Mwanri. Sasa *external contradiction* zile watu wamesha-*assess the millennium goals* wakasema tutawapa fedha kwa Elimu za Msingi. Kwa hiyo, hata *internal contradiction* kwa ninyi Taifa mnapopanga mkitaka kukopa fedha Benki ya Dunia, mnakopa mnapewa. Mnapeleka kujenga hayo mashule ya MMEM na wamekopa kweli kweli. Sasa tatizo la

watu hapa hawataki kusema kwamba hizo fedha wamekopa na Watanzania watalipa. Sasa Wizara hii inapopewa, Mheshimiwa Joseph Mungai, ninamshukuru kwa utekelezaji, anafanya lakini zile fedha alizopeleka sio za kwake kutoka mfukoni ni fedha za Taifa, watu wameomba wamepeleka pale. Kwa hiyo, lazima tuone hiyo tofauti. Sasa ikija kwenye Wizara ya TAMISEMI, ambayo mimi nitakwenda huko kwenye barabara baadaye ukanung'unika ukalaumu tunakuwa hatumtendei Waziri haki kwa sababu atakwenda kugombana na bosi wake, wewe unaniaibisha. Sasa unaniabisha hoja ni kwamba, Wizara hii inahitaji vitu gani? Inahitaji *resources,* inahitaji fedha kwa ukubwa wake na mambo ambayo inapaswa kuyafanya. Hilo ndilo moja la msingi. Kama hatuwezi kuliona hilo tutakuwa tunapiga kelele isiyokuwa ya msingi hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sijui kama ninaeleweka maana yake ninasikia mwingine huko sijui anasema nini, sijui kama ninaeleweka? *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Tunakuelewa

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninachosema ni suala la *resources* kwenye Wizara hii. Maana Wizara hii ukienda ngazi ya chini ndio tunazungumza Madiwani walipwe mishahara. Sasa sijui kuna bajeti imepitishwa hapa watu wanawanyima, mimi sielewi. Lakini kiutendaji wao wanapaswa kuleta sheria hapa kubadilisha. Tunazungumzia Wenyeviti wa Vitongoji walipwe mshahara. Sasa huwezi kumtaja mtu ambaye hukumtengea bajeti. Hoja lazima tu-*address* kwamba, bajeti iwepo. Unajua mtu mzima ukimsimamisha hivyo ukinitoa mimi utumbo, utumbo wangu ukiurefusha hivi ni mrefu kuliko mimi.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako masuala ya barabara. Ndugu yangu, Waziri wa Ujenzi, kila mwezi tunajua zinatengwa shilingi ngapi za Kitaifa kwa ajili ya barabara kuu za Serikali na za *Trunk Road,* pamoja na za wafadhili. Lakini ule mtandao wa Kijiji kwenda Kijiji, Kata, Tarafa, Kitongoji kwenda za Mheshimiwa hapa Brigedia Mstaafu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), vile vile viutumbo utumbo ni vingi, ninajua kuna watu hawataki kunisikiliza kwa sababu zao, lakini ukweli unawasha. Lazima tukubaliane hapa kwamba, *resources* za Wizara hii tuziweke ziwe nyingi kwa sababu barabara ziko pale na hazitengenezwi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, nirudi kwangu. Katika Mkoa wa Kagera, Wilaya ya Karagwe ndiyo yenye watu wengi kuliko Wilaya nyingine kwa mujibu wa sensa iliyofanyika mwaka 2002 na ndiyo Wilaya ambayo wakazi wake hawajui miradi. Sasa ninajiuliza tunafanyaje? Tulikuwa na miradi kama *Kagera Agricultural and Environmental Management Project (KAEMP),* kwa sababu za kihistoria na kwa sababu zingine ambazo siwezi kuzitaja katika Bunge, wahusika wakatudhulumu Wilaya ya Karagwe na Wilaya ya Ngara hawataki kutujengea barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu anayekimbia kwao kwa sababu kuna matatizo ni mjinga. Tulikuwa na Waholanzi katika Wilaya hii wakajitoa hawasaidii barabara ya upande wa *DRDP.* Nimesoma takwimu za Mheshimiwa Waziri hapa kwa mwaka unaoishia mwezi Juni, 2004, ninapozungumza wamepeleka shilingi milioni 133 kwa

ukubwa wa Wilaya ile, sasa ziko barabara hawakutengeneza. Wafadhili wameondoka, hakuna chanzo kingine na zile barabara ziko pale. Sasa bahati nzuri nilipokwenda jimboni nikakuta watu wamejipitisha pitisha pale huyu Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi hakutengeneza barabara anasema maneno. Nikawaambia wapumbavu sana.

Sasa maneno haya sio ya humu nikawaambia wapumbavu wanaosema Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi hakutengeneza barabara kwa sababu yeye hakusanyi kodi wala hakopi kutoka Benki ya Dunia, wala hajakataa kutengeneza barabara. Nashukuru wananchi walinielewa. Lazima tufike mahali tuseme ukweli kwamba, barabara haikutengenezwa kwa sababu fedha zilikuwa kidogo. Sasa mtu unajipitisha pitisha hapa unasema mambo ambayo hayapo tukikujibu halafu unalalamika.

Sasa ninachotaka kusema Mheshimiwa Waziri ni kwamba, kuna barabara kutoka Kigarama kupita Mabira kwenda Rwenkorongo hazikutengenezwa. Kuna barabara kutoka Nkwenda kupita Mabira haikutengenezwa. Kutoka Kakanja, Kikuhuru, Kitwe haikutengenezwa. Kagenyi Nyaruzumbura haikutengezwa na nyingine. Sisi pale wala hazihitaji fedha nyingi kwa sababu udongo wa kwetu ni mgumu kidogo. Lakini fedha hizi mlizopeleka hazitoshi tungeomba mjaribu kufikiria kupeleka kule fedha, *KAEMP* wamekula wale wanaozijua. Waholanzi wamejitoa.

Sasa nilichokuwa ninaomba ni kwamba, katika makundi yenu mlianglie hilo. Kunapokuwa kumekwama basi tuelezeni ukweli sio mtu anapita huku anasema fulani amekataa kutengeneza barabara, ameidhulumu, kitu ambacho si kweli. Kama hilo halitoshi sasa tunachosema wale ambao wanapiga kelele kuna fedha zimeletwa za *STABEX* na sisiti kuzisemea fedha za *STABEX* mpaka nikiondoka kwenye Bunge hili. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Charles Keenja, Waziri wa Kilimo na Chakula, nilipomwuliza hapa fedha akaniambia zipo kwa Waziri wa Ujenzi. Nimemwuliza Waziri wa Ujenzi akasema mimi sijui na hizo fedha zilitakiwa kwenda kutengeneza barabara hizi. Sisi Kagera tunazalisha kahawa zote za robusta za nchi hii nazo ni zaidi ya nusu ya Kahawa tunazozalisha. Sasa tupelekeeni fedha hizo zikatengenezwe barabara hizi ambazo ni *feeder roads,* hamna.

Sasa mimi nitakuwa sina akili nikija kuanza kugombana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) hapa, kwa nini hukutengeneza barabara wakati chanzo ninakijua! Ndiyo maana kama tuna-*attack system, we are attacking the system.* Kama tunam-*attack an individual,* tunam-*attach an individual.* Sasa watu wengine hapa wanakaa tu wanacheka halafu basi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tungeomba na juzi nilikuwa nauliza swali nikamwuliza Waziri wa Ujenzi, atuambie Waziri wa Kilimo yeye akajibu. Jana nikamwuliza hapa Waziri Mkuu ajibu tusikie kauli, yeye akajibu tena. Kuna nini? Kwanza, watu umewanyima fedha eti wanalewa, walevi wanalima Kahawa! Kwa nini kama sio dharau mbona mnataka kuunda Benki ya kuwakopesha hiyo mikopo ndiyo

hawatakula. Mtu analima kahawa hapewi fedha zake eti atalewa, sasa tengeneza barabara haipo.

Sasa mimi ninataka kuiambia Serikali kwamba, watu wa Kyerwa waliponichagua hawakuwa wajinga. Nitakwenda kuwaeleza na wanaelewa kwamba mlikula fedha zao na mkasema wao ni walevi na barabara hawakutengeneza hata moja halafu mje muone kama hawatawanyima kura. Acha kushangilia hapa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ndio ukweli. Sasa hii kazi ya watu wengine kuwafanyia wengine kwa kweli sio vizuri. Wamesema hapa Madiwani, wamesema Wenyeviti wa Vijiji na Wenyeviti wa Vitongoji. Nilikwishakusema kule mwanzo Watendaji katika Serikali na sio kwa Wenyeviti wa Vijiji, kuna tabia mimi sijui *mind set* yetu sijui ikoje. Mtu akishakoma kuchaguliwa basi yeye hafai. Yaani Afisa Mtendaji analipwa mshahara kwa nini yaani kazi anayoifanya kuliko Mwenyekiti wa Kijiji ninyi mniambie hapa kwamba anafanya hivi, anafanya hivi.

Sasa Mwenyekiti wa Kijiji achaguliwe pale lawama zote kwake, yeye ndiye anatuliza watu msiwapige ikija kukamatwa ndiyo anafanya. Sasa yeye hapa mpe shilingi 10/= hamna kwa sababu yeye sio mtendaji. Tukija kwa Diwani mmeelezwa. Pikipiki zinapokuwepo Afisa Mtendaji wa Kata mnampa pikipiki. Diwani mpe pikipiki aah huyo tulisema awe anajitosheleza.

Ni sheria gani kwani Bush ana fedha nyingi. Yaani wale matajiri wanaoongoza dunia hawapewi mshahara kwa mujibu wa sheria za nchi. Sasa tunaomba kwamba tabia ya Watendaji kujipendelea iachwe na hao waliochaguliwa wana haki pia kuhakikisha kwamba, wanawezeshwa na wanafanya shughuli zao.

**MBUNGE FULANI:** Na Wabunge pia.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** EEh!!! Hata Wabunge hapa. Sijui mshahara wa Rais ni shilingi ngapi. Hivi yeye angekula mshahara wake angeweza kuishi. Mimi sielewi nadhani ni tabu tu. Nadhani ni matatizo tu. Kwa hiyo, wala siyo suala la kucheka hapa, *it is a problem.*

Mheshimiwa Naibu Spika, huwa ninasafiri nakwenda pale Ubungo. Ubungo ni Dar es Salaam na mimi huwa ninasafiri, kwa hiyo nina haki ya kusafiri kwenda huko. Sasa ukifika pale wananyang'anya na shilingi 200/=, ukipanda teksi nataka kuingia kumchukua mteja amsafirishe kwa sababu kile kituo kiko pale kusafirisha watu eti ulete shilingi 500/=. Hapa mlitueleza mlifuta kodi zenye kero. Hivi kuna kero kuliko hii ya kunyang'anyana na teksi dreva shilingi 500/=. Sasa sijui ni mfumo upi.

Hapa kuna kudhulumiana hapa. Mtu anaingia pale unasema lete shilingi 500/=, mnanyang'anyana na kinachofanyika hakipo. Ukiacha wakati ule Mheshimiwa Charles Keenja, akiwa hafanyi kazi kwenye *system.* Ninadhani mtanisamehi jinsi ninavyotamka vibaya lakini nadhani anajulikana Mheshimiwa Charles Keenja. Kwa hiyo, hicho kituo cha teksi na hapo pengine tunawaomba hizo dhuluma wanazozifanya waziache.

**WABUNGE FULANI:** Unga mkono, unga mkono!

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani baada ya kuyasema hayo, kuunga mkono ni suala la Mbunge anaamua namna gani aunge mkono ama akatae. Sasa kwa sababu tulishasema hapa kuna mambo mazuri ambayo

Serikali walipoyasikia wakayafanyia kazi na mengine hawajayafanyia. kazi, bahati mbaya kwamba katika nchi ya Tanzania huyu akisema nimeleta barabara kutoka Mutukula mpaka Mtwara wanataka wambebe, lakini nchi zingine ukienda Marekani barabara inapita juu inapita chini inakuwa kero.

Ukiingia majini ukienda huko chooni yale maji ya kuoga hata unaweza kunywa. Hakuna anayedai simu, shule na nini. Hoja ni kwamba, wewe umeingia madarakani, swali ni kwamba, mshahara wangu, kipato changu kiko namna gani mfukoni, kikipungua wanakutimua.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la mwisho ningeomba wewe unayesimamia mpaka Vijijini wanakosimamia na umaskini wa kipato cha watu wa kawaida kule ni tabu sana. Watu hawana fedha. Sasa Serikali imeanzisha utaratibu kwamba, Halmashauri zote tutakuwa tunawagawia kama watoto wadogo na ukitaka kumtawala mtu wewe unamgawia fedha bwelele hivi kama mtoto mdogo.

Halmashauri lazima zipewe njia za kupata mapato zenyewe. Kama ni *registration* ya magari tukae tukubaliane kwamba, kwa utaratibu huu Halmashauri hata zile kodi ambazo tunasema ni za Serikali Kuu tuzipunguze zingine ziende Halmashauri.

Mimi sipendekezi kurudisha kodi ya kichwa au ya maendeleo, lakini hii tabia ya Serikali kukaa pale ikaanza kujisifu tumeleta shule hapo, tumeleta hospitali, tutafika mahali tutakwama wakati mambo yatakapotanuka. Kama tatizo hilo hamuwezi kuliona hapa basi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, tunapeleka watoto shule, tunajenga shule sasa hivi za Sekondari watakapokuwa asilimia 50 ya Watanzania wameelimika wakajua haki zao na ajira hakuna na wakati tumepuuza kilimo hapo watawatimua. Muda wangu umekwisha. Kwa hiyo, kama nilivyosema mimi sina ugomvi na Wizara.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Hapo ndio tumefikia mwisho wa Shughuli za Bunge leo, sasa naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.44 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa tarehe 25 Juni, 2004 saa tatu asubuhi)*